

**TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU
YA BUNGE YA SHERIA NDOGO KWA KIPINDI CHA
JANUARI 2021 HADI FEBRUARI 2022**

*[Imetolewa chini ya Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni
za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020]*

YALIYOMO

IKISIRI	iii
SEHEMU YA KWANZA	1
1.0 UTANGULIZI	1
1.1 Maelezo ya Jumla.....	1
1.2 Muundo wa Taarifa.....	2
1.3 Msingi wa Shughuli za Kamati	2
1.3.1 Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.....	3
1.3.2 Kanuni za Kudumu za Bunge.....	3
1.3.3 Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1	4
1.4 Njia na Mbinu Zilizotumika	4
SEHEMU YA PILI	6
2.0 UFAFANUZI WA SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA	6
2.1 Maelezo ya Jumla.....	6
2.2 Ufafanuzi wa Shughuli zilizotekelezwa.....	6
2.2.1 Mafunzo ya awali.....	6
2.2.2 Uchambuzi wa Sheria Ndogo	11
2.2.3 Uchambuzi wa Taarifa za utekelezaji wa mapendekezo ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa wakati wa Mkutano wa Pili wa Bunge.....	13
2.3 Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Mapendekezo ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa wakati wa Mkutano wa Pili	14
2.3.1 Hatua ya Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo iliyohakikiwa na kusubiri Namba ya Tangazo la Serikali	16
2.3.2 Hatua ya Maandalizi ya Rasimu ya marekebisho ya Sheria Ndogo kwa ajili ya uhakiki na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali ...	17
SEHEMU YA TATU	19
3.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO AMBAZO ZILIWASILISHWA KATIKA MKUTANO WA TANO	19
3.1 Maelezo ya Jumla	19
3.2 Matokeo ya Uchambuzi	19
3.2.1 Kukinzana na masharti ya Mama na sheria nyingine za nchi.....	20
3.2.2 Kutoendana na Misingi Bora ya Uandishi wa Sheria	21
3.2.3 Kukosa Uhalisia	21

SEHEMU YA NNE	23
4.0 MAONI NA MAPENDEKEZO.....	23
4.1 Maelezo ya Jumla	23
4.1.1 Sheria Ndogo Kukinzana na Masharti ya Sheria Mama	23
4.1.2 Sheria Ndogo kutozingatia Misingi ya Uandishi bora wa Sheria .	23
4.1.3 Sheria Ndogo kuwa na Masharti yasiyozingatia Uhalisia	24
4.1.4 Sheria Ndogo kukosa Usahihi na ufasaha katika uandishi wa majedwali.....	24
4.1.5 Uchelewaji katika kutekeleza Mapendekezo ya kurekebisha Sheria Ndogo.....	25
4.1.6 Kutokutekelezwa kwa Mapendekezo	25
4.1.7 Ushirikishwaji hafifu wa Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria katika mchakato wa uwalishaji wa majibu mbele ya Kamati.....	26
4.1.8 Ushirikishwaji wa Wadau katika Utungaji wa Sheria Ndogo	26
4.1.9 Utozaji wa ada zinazofanana unaotekelezwa na mamlaka zaidi ya moja.	26
4.2 Mapendekezo.....	27
4.2.1 Kukinzana na masharti ya sheria inayotoa mamlaka ya kutungwa kwa sheria ndogo au sheria nyingine za nchi.....	27
4.2.2 Kutozingatia Misingi ya Uandishi Bora wa Sheria.....	28
4.2.3 Masharti yasiyo na uhalisia.....	28
4.2.4 Dosari ya Uandishi wa Majedwali	28
4.2.5 Uchelewaji katika kutakeleza Mapendekezo ya kurekebisha Sheria Ndogo.....	29
4.2.6 Kutokutekelezwa kwa Mapendekezo	29
4.2.7 Ushirikishwaji hafifu wa Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria katika Mchakato wa Uwalishaji wa Majibu mbele ya Kamati	29
4.2.8 Ushirikishwaji wa Wadau katika Utungaji wa Sheria Ndogo	30
4.2.9 Utozaji wa ada zinazofanana unaotekelezwa na mamlaka zaidi ya moja	30
SEHEMU YA TANO	32
5.0 HITIMISHO.....	32
5.1 Shukrani	32
5.2 Hoja	34

IKISIRI

Taarifa hii inawasilishwa kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 (Kanuni za Bunge). Madhumuni yake ni kuliwezesha Bunge kuijadili na hatimaye kuamua kutokana na mapendekezo yanayotolewa. Ili kufanikisha hilo, Taarifa imegawanyika katika sehemu kuu tano ambapo, Sehemu ya Kwanza ni maelezo ya jumla inayofuatiwa na Sehemu kuu za msingi tatu na Sehemu ya mwisho inahitimisha. Sehemu ya Kwanza inabainisha msingi wa shughuli za Kamati kutoka kwenye Katiba, Kanuni za Bunge na Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1. Aidha, sehemu hiyo inabainisha njia zilizotumika.

Sehemu ya Pili inafafanua shughuli zilizotekelezwa. Shughuli hizo ni mafunzo ya awali, uchambuzi wa Sheria ndogo na uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Mapendekezo ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo. Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za utekelezaji yameonesha hatua kuu mbili zilizofikiwa katika utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwishatolewa kuhusu Sheria Ndogo. Hatua hizo ni kuwa na Rasimu ya marekebisho ya Sheria Ndogo iliyofanyiwa uhakiki na kusubiri kuchapishwa na kutangazwa. Hatua nyingine ni kuwa na Rasimu iliyopatikana lakini haijafikia uhakiki. Aidha, ufafanuzi unatolewa kuhusu mapendekezo ambayo hayajafanyiwa kazi.

Sehemu ya Tatu inaonesha matokeo ya uchambuzi wa Sheria Ndogo 130 zilizowasilishwa wakati wa Mkutano wa tano wa Bunge. Matokeo ya uchambuzi yanabainisha dosari 21 katika Sheria Ndogo hizo. Dosari hizo zimeainishwa katika namna kuu tatu ambazo ni kukinzana na masharti ya sheria mama na sheria nyingine za nchi (Sheria Ndogo 1), kutoendana na misingi ya uandishi (Sheria Ndogo 8) na kuweka masharti yasiyo ya uhalisia (Sheria Ndogo 2).

Sehemu ya Nne ambayo ni msingi wa mapendekezo imebainisha maoni kuhusu mambo makuu manane (8). Mambo hayo ni: Sheria Ndogo kukinzana na masharti ya Sheria mama, kutozingatia misingi ya uandishi bora wa sheria, kuwa na masharti yasiyozingatia uhalisia na kukosa usahihi na ufasaha katika uandishi wa majedwali. Mengine ni uchelewaji katika utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwisha tolewa na Bunge kuhusu Sheria Ndogo, Kutokutekelezwa kabisa kwa mapendekezo ya Bunge, Ushirikishwaji hafifu wa Wadau kwenye mchakato wa utungaji Sheria Ndogo pamoja na utozaji wa ada zinazofana katika chanzo kimoja unaofanywa na mamlaka zaidi ya moja. Kwa muhtasari, sehemu hii inapendekeza Bunge likubali mapendekezo yafuatayo:

- (a) Mamlaka zilizotunga Sheria Ndogo zenye kukinzana na masharti ya sheria mama na sheria nyingine za nchi, zirekebishe sheria ndogo hizo;
- (b) Mamlaka zilizokabidhiwa madaraka ya kutunga Sheria Ndogo zilikutwa na dosari ya kutozingatia misingi ya uandishi bora wa sheria, zirekebishe dosari hiyo;
- (c) Mamlaka zinazohusika na kutungwa kwa Sheria Ndogo zilizobainika kuwa na masharti yasiyozingatia uhalisia, zifanye marekebisho haraka;
- (d) Mamlaka zilizotunga Sheria Ndogo na kubainika kuwa na dosari katika uandishi wa majedwali zifanye marekebisho;
- (e) Mamlaka zilizobainika kuwa zimechelewa kutekeleza mapendekezo ya kurekebisha Sheria Ndogo zilizokutwa na dosari, zikamilishe haraka mchakato wa marekebisho;
- (f) Mamlaka zilizobainika kutokuwa zimeanza utekelezaji wa mapendekezo ya Bunge yaliyohusu kurekebisha dosari katika sheria ndogo:
 - (i) zitekeleze mapendekezo hayo haraka; na
 - (ii) zitoe taarifa kwa Kamati ya Sheria Ndogo kuhusu ya hatua inayofikiwa, kabla ya kuahirishwa kwa Mkutano wa Saba wa Bunge.
- (g) Taasisi zinazotunga au kufanya marekebisho mbalimbali katika Sheria Ndogo, zishirikiane inavyostahili na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;
- (h) Mamlaka zinazohusika na Sheria Ndogo zilizobainika kutoza kwa pamoja ada zinazofanana katika chanzo kimoja:
 - (i) zikamilishe mchakato wa kupitia Sheria Ndogo hizo ili kuhuisha viwango vya ada; na
 - (ii) Zizingatie umuhimu wa kuweka masharti yasiyoweka ugumu wa utekelezaji wake kwa watu wenye kipato cha chini.
- (i) Mamlaka zilizokabidhiwa madaraka ya kutunga Sheria Ndogo, zizingatie umuhimu wa kuwashirikisha wadau kikamilifu katika mchakato wa utungaji wa sheria hizo.

Sehemu ya Tano na ya mwisho ya Taarifa, inahitimisha na kutoa hoja kwamba Bunge liipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo pamoja na maoni na mapendekezo yaliyotolewa.

TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO KWA KIPINDI CHA JANUARI 2021 HADI FEBRUARI 2022

[Imetolewa chini ya Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni
za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020]

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

1.1 Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 (Kanuni za Bunge) naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo. Taarifa hii inaelezea kwa shughuli mbalimbali zilizotekelezwa na Kamati zinazohusu uchambuzi wa Sheria Ndogo kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Januari, 2021 hadi Februari, 2022

Mheshimiwa Spika, majadiliano ya Bunge kuhusu Taarifa hii yataliwezesha Bunge kufuatilia na kudhibiti madaraka yake yaliyokasimiwa kwa mamlaka nyingine kutunga sheria Ndogo. Kwa kufanya hivyo, litakuwa limetekeleza wajibu wake unaozingatia nafasi yake katika utungaji wa Sheria za nchi. Aidha, Bunge litaweza kujiridhisha na namna sheria ndogo zinavyochangia kuboresha maisha ya watanzania na kushauri hatua zinazostahili kuchukuliwa kuhusu sheria ndogo nchini.

Taarifa hii pia imeainisha matokeo ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo mbalimbali zilizowasilishwa katika Mkutano wa Tano wa Bunge tarehe 9 Novemba, 2021 pamoja na maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusu dosari zilizobainika wakati wa uchambuzi wa Sheria Ndogo hizo.

1.2 Muundo wa Taarifa

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha ufuatiliaji wa Bunge lako tukufu na kurahisisha majadiliano ya hoja na hatimaye uamuzi wenye tija, naomba kuonesha muundo na mawanda (*scope*) ya taarifa hii. Kwa madhumuni hayo, nitangulie kueleza kuwa, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tano:-

- (i) Sehemu ya kwanza ambayo ni ya utangulizi inatoa maelezo ya jumla kuhusu kuhusu taarifa hii ili kuandaa muktadha wa majadiliano;
- (ii) Sehemu ya pili inafafanua shughuli zilizotekelezwa inayohusu shughuli zilizotekelezwa inafafanua ili kuonesha msingi wa matokeo;
- (iii) Sehemu ya Tatu inafafanua matokeo ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa wakati wa Mkutano wa tano wa Bunge;
- (iv) Sehemu ya Nne inafanya majumuisho wa maoni kutokana na Shughuli zilizotekelezwa ili kujenga msingi wa mapendekezo katika hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo inayojadiliwa leo; na
- (v) Sehemu ya Tano na ya mwisho inayohitimisha hoja ili kuliomba Bunge lifanye uamuzi.

Mheshimiwa Spika, ili kumbukumbu za majadiliano ya Bunge ziwe katika mtiririko unaoeleweka kwa urahisi, Taarifa hii inasomeka kwa pamoja na majadwali Na. 1 na Na. 2 ambayo yameambatishwa. Naliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili Taarifa hii ili hatimaye lifanye uamuzi unaostahili.

1.3 Msingi wa Shughuli za Kamati

Mheshimiwa Spika, msingi wa shughuli za Kamati unatiririka kutoka Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Jumhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 (Katiba), Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 (*The Interpretation of Laws Act, Cap.1*) na Kanuni za Bunge. Katika mtiririko huo, madaraka ya kutunga

Sheria, masharti ya kutunga Sheria Ndogo, utekelezaji wa madaraka ya Bunge na majukumu ya uchambuzi wa Sheria Ndogo vimeanishwa kama ifuatavyo:-

1.3.1 Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Mheshimiwa Spika, Katiba ya nchi ni hati kuu inayotoa idhini kwa mambo yote ya kisheria, kisiasa na kijamii katika Taifa. Ibara ya 8(1) inaonesha kuwa, msingi wa mamlaka yote ya nchi ni wananchi. Aidha, Ibara hiyo inaonesha kuwa, lengo kuu la Serikali ni ustawi wa wananchi. Hivyo, Bunge, mamlaka ya utendaji na mamlaka ya kusimamia haki, kamwe havitatekeleza madaraka yao kwa namna tofauti na kuwezesha ustawi wa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 4 ya Katiba imeweka mgawanyo wa madaraka na kulitambua Bunge kama chombo cha kutunga sheria na kusimamia shughuli za umma. Aidha, Ibara ya 97 ya Katiba imelipa Bunge uwezo wa kukabidhi madaraka kwa mtu au mamlaka nyingine kutunga sheria ndogo.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 96 ya Katiba imelipa Bunge uwezo wa kuunda Kamati za namna mbalimbali kama zitakavyofafanuliwa katika Kanuni za Bunge kwa ajili ya utekelezaji bora wa madaraka yake. Kamati ya Kudumu ya Sheria ya Ndogo kama zilivyo Kamati zingine, imeundwa kutokana na mamlaka ya Bunge kikatiba na madhumuni yake ni kuwezesha utekelezaji bora wa madaraka ya Bunge ya kutunga Sheria zote nchini.

1.3.2 Kanuni za Kudumu za Bunge

Mheshimiwa Spika, Kanuni za Kudumu za Bunge lolote katika demokrasia ya kibunge kama Tanzania, zinaelekeza utekelezaji wa madaraka ya Bunge na uendeshaji wa shughuli zake kwa mujibu wa Katiba ya nchi inayohusika. Kanuni za Bunge la Tanzania zimetungwa chini ya Ibara ya 89 ambayo ni Sura ya 2 ya Sheria za Tanzania. Kanuni

hizo zimezingatia masharti ya Ibara ya 96 (2) kwa kuanzisha Kamati za Kudumu za Bunge kama ilivyoelekezwa katika Kanuni ya 135 ikisomwa kwa pamoja na Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge. Aidha, kifungu cha 11 (1) cha Nyongeza ya Nane, kimefafanua majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo. Majukumu hayo ni kuchambua Sheria Ndogo ili kujiridhisha iwapo hazikiniani na Katiba ya nchi, Sheria inayoruhusu kutungwa kwa sheria ndogo zinazohusika na Sheria zingine za nchi.

1.3.3 Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Tafsiri ya Sheria, inayosimamia masuala yanayohusu uandishi, matumizi, tafsiri na uzingatiaji wa Sheria za nchi, imeweka masharti mbalimbali ikiwemo uwekaji Mezani Bungeni na madaraka ya Bunge katika Sheria Ndogo. Kifungu cha 38 cha Sheria hii, kinaweka sharti la kuweka Mezani Sheria Ndogo zote ndani ya siku 6 za Mkutano wa Bunge unaofuata baada ya kuwa zimechapishwa na kutangazwa kwenye gazeti la Serikali. Aidha, kifungu hicho kinaruhusu Bunge kuona kama Sheria Ndogo inayohusika inaweza kubadilishwa, kurekebishwa au kuongezwa masharti mengine.

1.4 Njia na Mbinu Zilizotumika

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge inaitaka Taarifa hii kubainisha njia na mbinu zilizotumika wakati Kamati ilipotekeleza majukumu yake. Naomba kulijulisha Bunge kuwa, njia na mbinu zilizotumika ni kama ifuatavyo:-

- (i) Kupitia orodha ya Sheria Ndogo zote zilizowekwa mezani Bungeni. Lengo la mbinu hiyo ni kupata wigo wa kazi ya uchambuzi na kufahamu sekta zinazohusika;
- (ii) Kupitia neno kwa neno katika uchambuzi wa awali ili kubaini masharti yanayowekwa na Sheria Ndogo inayohusika. Aidha,

mbinu hii iliwezesha Kamati kubaini iwapo kuna jambo la kulihakiki kulingana na majukumu ya Kamati;

- (iii) Kuhakiki mtiririko wa maudhui kwa kulinganisha masharti yanayowekwa katika Sheria Ndogo ikiwa ni pamoja na Majedwali kama yapo;
- (iv) Kuainisha maudhui ya Sheria Ndogo na madhumuni ya Sheria Kuu iliyoruhusu kutungwa kwa Sheria Ndogo inayohusika;
- (v) Kuoanisha masharti ya Sheria Ndogo inayochambuliwa na misingi iliyowekwa katika Katiba, Sheria Kuu (Sheria Mama) na Sheria Nyingine za nchi;
- (vi) Kutafakari uhalisia wa masharti yanayowekwa na Sheria Ndogo inayohusika. Lengo ni kubaini uwezekano wa kutekelezeka;
- (vii) Kufanya upembuzi wa kina wa Sheria Ndogo kwa kutathmini masharti ya Sheria Ndogo inayohusika yanavyozingatia Katiba, Sheria Kuu na Sheria nyingine za nchi; na
- (viii) Kufanya mahojiano na mamlaka iliyotunga Sheria Ndogo kwa idhini ya Bunge. Madhumuni yake ni kuwa na uelewa unaofanana kuhusu matokeo ya uchambuzi na kupata majibu au ufafanuzi wa ziada. Aidha, njia hii iliwezesha Kamati kuchuja hoja zilizotokana na uchambuzi kabla ya kutoa Taarifa hii Bungeni.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge kuwa, njia hizo zilizohakikishia Kamati uthabiti na uhakika wa matokeo ya uchambuzi kwa namna inayotoa matumaini. Niwashukuru Mawaziri waliohusika na Sheria Ndogo katika kipindi hicho, kwa kutoa ushirikiano mkubwa. Ushirikiano huo ulichangia kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Kamati pamoja na kukidhi matarajio ya kuchambua Sheria Ndogo.

SEHEMU YA PILI

2.0 UFAFANUZI WA SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA

2.1 Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, sehemu hii ya Taarifa ni kiini cha msingi wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Bunge. Kanuni hiyo inaweka sharti kwa kila Kamati kuwasilisha Taarifa ya mwaka ya shughuli zake. Hivyo, katika sehemu hii, Kamati inatoa maelezo kuhusu shughuli zote zilizotekelezwa. Lengo ni kuliwezesha Bunge kubaini mafanikio na changamoto kwa muktadha wa majukumu yake ya kutunga Sheria, kuisimamia na kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ili kuliwezesha Bunge kutekeleza madaraka yake, sehemu hii inahusu ufafanuzi wa mambo makuu matatu yafuatayo:-

- (i) Mafunzo ya awali kwa Wajumbe wa Kamati, kuhusu maeneo yanayohusika na uchambuzi wa Sheria Ndogo;
- (ii) Uchambuzi wa Taarifa za utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa wakati wa Mkutano wa Pili; na
- (iii) Uchambuzi wa Sheria Ndogo kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, ufafanuzi huo unaonesha yatokeanayo na uchambuzi. Madhumuni ni kulieleza Bunge, mambo yaliyobainika kuhusu Madaraka ya kutunga Sheria, yanayokabidhiwa kwa mtu au mamlaka nyingine kwa njia ya kukasimu. Naliomba Bunge lako tukufu, lifuatilie maelezo hayo yanayojenga msingi wa maoni ya Kamati.

2.2 Ufafanuzi wa Shughuli Zilizotekelezwa

2.2.1 Mafunzo ya Awali

Mheshimiwa Spika, utaratibu uliowekwa na ofisi yako pamoja na usimamizi wako mzuri, uliwezesha Kamati kupata mafunzo. Kupitia mafunzo wajumbe waliweza kuelewa muktadha wa majukumu ya Kamati. Manufaa

makubwa yamepatikana katika kufanikisha dhamira ya Bunge kufuatilia na kudhibiti Sheria Ndogo kwa kutumia Kamati hii. Aidha, utaratibu huo uliwaandaa wajumbe kutekeleza jukumu la uchambuzi wa Sheria Ndogo na kuwapa hali halisi ya mchakato wa Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Spika, kwa faida ya Bunge hili, naomba kueleza kwa muhtasari uelewa uliopatikana kuhusu dhana ya Sheria Ndogo kama ifuatavyo:-

Kwanza, Sheria Ndogo si sheria zenye umuhimu mdogo au zenye thamani ndogo katika utekelezaji wa Sheria. Aidha, Sheria Ndogo si sheria ambazo zinatumiwa kwa umuhimu wa mwisho wala si sheria zinazotumiwa kwa nadra au kwa mazingira zinapokosekana Sheria kuu. Sheria Ndogo, si sheria zinazotumiwa baada ya kukosekana kwa sheria za msingi au sheria kuu. Maelezo hayo yanasahihisha uelewa usiostahili kuhusu Sheria Ndogo. Ufafanuzi huo unazingatia ukweli kwamba, uelewa potofu kuhusu Sheria Ndogo unaathiri nguvu ya Bunge katika himaya ya utungaji wa Sheria. Hivyo, kuna kazi ya kufanya kuweka hali hiyo katika usahihi wake.

Pili, Sheria Ndogo ni matokeo ya Sheria ya Bunge kukabidhi kwa mtu au mamlaka nyingie jukumu la kufafanua Sheria kwa kutunga Sheria zinazojulikana kwa jina la jumla la Sheria Ndogo. Matokeo ya Jukumu la mtu au mamlaka iliyokabidhiwa jukumu hilo yana uzito uleule wa Sheria ya Bunge. Kwa maneno mengine, Sheria Ndogo ni Sheria ya nchi inayotokana na kutumiwa kwa madaraka ya Kutunga Sheria yaliyokasimiwa kwa mamlaka nyingine.

Tatu, Katika mfumo wetu wa Sheria uliofafanuliwa na Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sheria Ndogo ni Maagizo (*Order*), Matamko (*Proclamation*), Kanuni za

Uendeshaji (*Rule*), Kanuni za Mahakama (*Rule of Court*), Kanuni za Wizara (*Regulations*), Hati (*Notice*), Sheria Ndogo za Halmashauri (*By Laws*) au Hati Rasmi (*Instrument*) iliyotungwa chini ya Sheria yoyote ya nchi au Mamlaka nyingine ya Kisheria. Katika mfumo wa Sheria za nchi, Sheria Ndogo zina uzito sawa na Sheria za Bunge, hivyo ni Sehemu ya Sheria za nchi. Kwasababu hiyo, ni hatari sana kutoangalia eneo la Sheria Ndogo kwa umakini na uzito unaostahili.

Nne, kuwa na Sheria ndogo katika mfumo wa Sheria za nchi ni jambo linalojitokeza katika uendeshaji wa nchi zote za kidemokrasia duniani. Kwa msingi huo, hakuna chombo cha kutunga Sheria katika nchi hizo kinachopaswa kuthubutu kuliacha eneo la Sheria Ndogo bila jicho lake makini. Sababu ni kuwa, dhima ya kutunga sheria si ya chombo chochote katika nchi bali ni ya Bunge la nchi inayohusika. Sheria Ndogo zikiwa na madhara, Bunge haliwezi kukwepa lawama hata kama zitakuwa zimetungwa na mtu au mamlaka nyingine iliyokabidhiwa jukumu hilo.

Tano, Sehemu kubwa ya Sheria za nchi ni Sheria Ndogo, ambazo zinagusa moja kwa moja maisha ya kila siku ya wananchi. Bunge ambalo ni chombo cha kutunga Sheria, na ni chombo cha uwakilisha wa wananchi, linatarajiwa kuangalia Sheria Ndogo inavyostahili.

Sita, mfumo wa utungaji wa Sheria Ndogo uliwekwa na Bunge kwa kuzingatia Ibara ya 97(5) ya Katiba. Ibara hiyo inatambua kwamba, Bunge linaweza kumkabidhi mtu au mamlaka nyingine madaraka ya kutunga Sheria Ndogo.

Saba, Kutokana na sababu mbalimbali za msingi, Bunge linaweza kukasimu kwa mamlaka nyingine jukumu la kufafanua masharti ya sheria. Utaratibu huo, unalipa Bunge nafasi ya kujielekeza kwenye ufafanuzi wa masharti ya jumla ya Sheria kuu. Desturi hiyo ya kibunge inatumika duniani kwa kiasi kwamba hakuna Bunge la nchi ya kidemokrasia duniani lenye ukiritimba kwa madaraka ya kutunga Sheria. Kwa hali hiyo Sheria zote za Bunge kwa pamoja haziwezi kufafanua masharti yake ipasavyo isipokuwa zikisomwa kwa pamoja na sheria Ndogo. Yote hii inatokana na ukweli kuwa Sheria Ndogo zinatokana na mambo makuu mawili (2):-

- (i) Mamlaka au mtu anayetunga Sheria Ndogo kukabidhiwa jukumu hilo na Bunge; na
- (ii) Mamlaka au mtu aliyekabidhiwa jukumu hilo kutumia madaraka hayo yaliyokasimiwa kwake.

Nane, Maagizo, Matamko, Kanuni za uendeshaji, Kanuni za Mahakama, Kanuni za Wizara , Hati, Sheria Ndogo za Halmashauri au Hati Rasmi inahesabika kuwa Sheria Ndogo iwapo:-

- (i) itakuwa imetungwa na mtu au mamlaka iliyokabidhiwa na Bunge madaraka ya kuitunga;
- (ii) madaraka hayo yatatokana na Sheria kuu ya Bunge; na
- (iii) inayo nguvu ya kisheria.

Mheshimiwa Spika, Mambo hayo kwa pamoja yanatukumbusha kuwa, siyo kila Kanuni ya uendeshaji au tamko la kiutawala au hati nyingine ni Sheria Ndogo. Kama kanuni au tamko la kiutawala au hati nyingine haina nguvu ya kisheria au haitokani na madaraka yaliyokasimiwa na Bunge, haijumuishwi katika orodha ya Sheria Ndogo na

hivyo si sehemu ya jukumu la Kamati hii kuifanyia uchambuzi.

Mheshimiwa Spika, mazingatio hayo yamekuwa ya msingi na muhimu kwa wajumbe katika kuhakikisha kuwa jicho la Bunge linamakinika katika Sheria Ndogo nchini. Wajumbe walipata mtazamo sahihi kuhusu kusimamia madaraka ya Bunge yaliyokasimiwa kwa mamlaka nyingine. Lengo ni kujiridhisha jinsi madaraka hayo yanavyotumika kuweka uhusiano wa kisheria baina ya mamlaka za Umma na watu au taasisi binafsi au baina ya mamlaka ya umma moja na nyingine.

Mheshimiwa Spika, mafunzo ya awali kwa Wajumbe yaliwezesha uelewa wa jumla kuhusu usahihi, uhalali na uthabiti wa Sheria Ndogo kwa vigezo vifuatavyo:-

a) Kutangaza Rasmi

Mheshimiwa Spika, Sheria Ndogo zote zinapaswa kukidhi sharti la kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Lengo la sharti hili ni kuhakikisha kwamba, umma kwa ujumla wake unajulishwa kutungwa kwa sheria ndogo inayohusika.

b) Kufuata na kuzingatia utaratibu uliowekwa katika Sheria Kuu

Mheshimiwa Spika, Sheria Ndogo zinatakiwa kufuata utaratibu na hatua zote zilizotakiwa na sheria kuu (Sheria Mama). Sababu ni kuwa, sheria ndogo inatokana na sheria ya Bunge na inatungwa ili kufanikisha lengo la Sheria ya Bunge. Tofauti na hivyo, itakuwa ni kuwa kinyume na lengo la Bunge.

c) Uhakika wa kutekelezeka

Mheshimiwa Spika, Sheria Ndogo zina kazi ya kuwezesha utekelezaji wa Sheria Kuu. Dhima yake ni kufanikisha malengo ya Sheria Kuu. Malengo hayo hayawezi kufanikishwa iwapo Sheria Ndogo haioneshi

uhakika wa kutekelezeka. Bunge linapokasimu madaraka ya kutunga sheria, halitarajii itungwe sheria ndogo isiyokuwa na tija katika mfumo wa sheria za nchi. Kwa sababu hiyo, Bunge linapaswa kujiridhisha kama sheria ndogo iliyotungwa inatekelezeka.

d) Kuwa ndani ya wigo wa madaraka uliowekwa na Sheria Kuu (*Intra Vires*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Sheria Ndogo zinawezesha utekelezaji wa Sheria Kuu, zinapaswa kuzingatia wigo wa mamlaka uliowekwa na Sheria Kuu. Bunge halitarajii kuwa, mamlaka inayokabidhiwa wigo uliobainishwa itatunga Sheria Ndogo inayovuka wigo huo. Dhamira ya Bunge kubainisha wigo ni kuzuia Sheria Ndogo isivuke upeo uliowekwa. Kwa msingi huo, Sheria Ndogo inayovuka ukomo wa mamlaka itakuwa imekiuka Sheria Kuu. Hali hiyo ni dosari isiyoweza kuachwa na Bunge.

e) Kuendana na masharti ya jumla ya Sheria Kuu

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sheria ndogo ni zao la Sheria Kuu, itapaswa kuendana na masharti ya jumla ya Sheria Kuu. Haitarajiwi Sheria Ndogo iharamishe au kukataza kilichohalalishwa (kilichoruhusiwa) na Sheria kuu. Aidha, Sheria Ndogo haitarajiwi kuhalalisha kilicho haramishwa na Sheria Kuu. Vile vile, Sheria Ndogo hazipaswi kuweka jambo linalotoka nje ya mfumo wa usimamizi wa sheria. Kwa msingi huo, Bunge hupaswa kujiridhisha kama mamlaka iliyokabidhiwa madaraka, inayatumia kwa namna isiyokuwa na dosari hizo.

2.2.2 Uchambuzi wa Sheria Ndogo

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa hapo juu, mamlaka ya kutunga sheria ni himaya ya Bunge. Mfumo wa Sheria za nchi huwekwa na mamlaka inayohusika na utungaji wa sheria. Mamlaka zingine katika nchi, zinaweza

kuchangia katika sheria za nchi kwa kuruhusiwa au kukabidhiwa na Bunge kiwango fulani cha madaraka ya kutunga sheria. Bunge ambalo ni mamlaka kuu ya kutunga sheria nchini, linapaswa kujiridhisha kuhusu kuzingatiwa kwa vigezo na masharti yake.

Mheshimiwa Spika, katika kufanikisha hilo, utaratibu wa Bunge lako tukufu umeweka masharti yanayoweza sheria ndogo zilizotungwa kuwekwa Mezani Bungeni kama ilivyofafanuliwa katika Kanuni ya 43 (2) ya Kanuni za Bunge pamoja na masharti ya Kifungu 38 (1) cha Sheria ya Tafsiri. Utaratibu huo unafanikisha azma ya Bunge kudhibiti Sheria Ndogo kupitia Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, Ili kutekeleza utaratibu huo, Kamati ilichambua Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika vipindi vitatu vifuatavyo:-

- (i) Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Pili zilichambuliwa na Taarifa ya Uchambuzi wake iliwasilishwa Bungeni tarehe 28 Juni, 2021;
- (ii) Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Tatu na wa Nne na Taarifa ya Uchambuzi wake kuwasilishwa Bungeni tarehe 10 Novemba, 2021; na
- (iii) Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Tano ambazo Uchambuzi wake ni sehemu ya Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kulihalikishia Bunge kuwa matokeo ya uchambuzi wa Sheria ndogo uliofanyika yamekuwa na tija katika kufanikisha utekelezaji bora wa madaraka ya Bunge. Kwa msingi huo, utaratibu uliowekwa na Bunge hili umekuwa na ufanisi kama ilivyokusuidwa.

2.2.3 Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Mapendekezo ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo Zilizowasilishwa wakati wa Mkutano wa Pili wa Bunge

Mheshimiwa Spika, katika kujiridhisha na utekelezaji wa madaraka ya Bunge ya kutunga sheria yaliyokabidhiwa kwa mamlaka zingine, Kamati ilifuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo zilizowekwa Mezani tarehe 9 Februari, 2021. Lengo ni kufuatilia hatua za kuondolewa kwa dosari zilizobainika katika Sheria Ndogo zilizohusika. Sababu ya kufanya hivyo ni kuhakikisha kuwa Bunge linaendelea kuzingatia mamlaka yake ya asili (*Original Authority*) bila kuathiriwa na utekelezaji wa mamlaka yaliyokasimiwa (*Delegated Authority*) ya kutunga Sheria.

Mheshimiwa Spika, Msingi wa nia hiyo ni nafasi ya Bunge katika Sheria za nchi. Kwa kuwa Sheria Ndogo ni sehemu ya Sheria za nchi, na kwamba Bunge ndiyo mamlaka kuu ya kutunga sheria nchini, hatua ya kufuatilia utekelezaji wa matumizi ya mamlaka ya kutunga Sheria Ndogo ni muhimu. Ufuatiliaji huo unahitajika zaidi pale ambapo zimebainika dosari katika Sheria Ndogo, na hasa dosari zinazoleta kero au mazalio ya kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu huo, Kamati ilizingatia nafasi yake ya kulisaidia Bunge kufuatilia utekelezaji wa madaraka ya Bunge yaliyokabidhiwa kwa mamlaka zingine. Katika kutekeleza azma hiyo, Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Mapendekezo ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa wakati wa Mkutano wa Pili wa Bunge. Madhumuni ni kufuatilia hatua iliyofikiwa katika kurekebisha dosari zilizobainika kwenye Sheria Ndogo Ishirini na Tatu (23). Sheria Ndogo hizo zilizokuwa na jumla ya hoja mia moja kumi na nane (118) za kiuchambuzi.

Mheshimiwa Spika, naomba kulihakikishia Bunge kuwa utaratibu wa kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo, umekuwa na manufaa makubwa. Aidha, utaratibu huo unazidisha ufanisi wa Bunge katika kuchukua nafasi yake stahifuu ya utungaji wa Sheria. Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa hizo kama yanavyooneshwa katika taarifa hii yanathibitisha jambo hilo.

2.3 Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Mapendekezo ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa wakati wa Mkutano wa Pili

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha madaraka ya kutunga Sheria yaliyokabidhiwa kwa mamlaka nyingine yanatumika inavyostahili, ni wajibu wa Bunge kufuatilia ipasavyo. Katika kutekeleza wajibu huo, Bunge halipaswi kuishia kubainisha dosari katika Sheria Ndogo bila kujiridhisha iwapo dosari hizo zimerekebishwa. Dhima hiyo inatokana na mamlaka ya asili ya Bunge kutunga sheria za nchi. Kwa kuwa Sheria Ndogo ni sehemu ya Sheria za nchi, dosari zinazojitokeza katika Sheria Ndogo, zinapaswa kufanyiwa kazi kwa utaratibu unaoendana na desturi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, Utaratibu wa Bunge kufanya kazi kwa kutumia Kamati za Bunge, ndio unaoiweka Kamati ya Sheria Ndogo katika nafasi ya kuliwezesha Bunge kufuatilia Sheria Ndogo na urekebishaji wa dosari zote zilizobainika. Kwa msingi huo, uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Mapendekezo kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa wakati wa Mkutano wa Pili ulifanyika. Madhumuni ya uchambuzi huo ni kubaini hatua iliyofikiwa katika kufanya marekebisho kwa lengo la kundoa dosari.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilianza kwa kudurusu mapendekezo ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo yaliyopitishwa na Bunge tarehe 28 Juni, 2021. Tangu tarehe hiyo hadi wakati Kamati inapokea Taarifa ya utekelezaji ni takribani miezi saba. Muda huo, ulitarajiwa kutosha kurekebisha dosari zilizobainika.

Mheshimiwa Spika, kwa madhumuni ya kulikumbusha Bunge hili Sheria Ndogo zilizowasilishwa wakati wa Mkutano wa Pili na kuchambuliwa zilikuwa ishirini na tatu (23). Uchambuzi wake ulibainisha jumla ya hoja mia moja kumi na nane (118) na Bunge likapitisha Mapendekezo yake kutokana na hoja hizo.

Mheshimiwa Spika, katika kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo hayo, Kamati ilipima na kutathmini hatua iliyofikiwa. Vigezo vya upimaji na tathmini vilijumuisha sababu za hatua iliyofikiwa. Aidha, njia ya kulinganisha hatua iliyofikiwa na athari za dosari zilizobainika, ilisaidia tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo ya Bunge. Jambo kuu la muhimu lililozingatiwa ni suala la madhara ya kutozingatia mapendekezo katika maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, Matokeo ya uchambuzi yalionesha kwamba, hatua za utekelezaji zilizoripotiwa zinagawanyika katika makundi makuu matatu yafuatayo:-

- (i) Hatua ya Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ambapo uhakiki umekamilika na kusubiri namba ya Tangazo la Serikali; na
- (ii) Hatua ya Maandalizi ya Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo kwa ajili ya uhakiki na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba kufafanua hatua hizo za utekelezaji ili kuliwezesha Bunge kufuatilia ipasavyo. Katika kufanya hivyo, nitangulie kubainisha kuwa Wizara zinazohusika na Sheria Ndogo hizo ni saba ambazo ni:-

- (i) Ofisi ya Rais TAMISEMI iliyokuwa inahusika kwa Sheria Ndogo 14 zilizobainika kuwa na jumla ya hoja 36;
- (ii) Wizara ya Afya iliyohusika na Sheria Ndogo 3 ambazo zilibainika kuwa na jumla ya hoja 6;
- (iii) Wizara ya Madini iliyohusika na Sheria Ndogo 1 ambayo ilikuwa na hoja 2;

- (iv) Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo iliyohusika na Sheria Ndogo moja ambayo ilikuwa na hoja 8;
- (v) Wizara ya Maliasili na Utalii iliyohusika na Sheria Ndogo 2 ambayo ilikuwa na hoja 2;
- (vi) Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi iliyohusika na Sheria Ndogo 1 ambayo ilikuwa na hoja 15; na
- (vii) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iliyohusika na Sheria Ndogo 1 ambayo ilikuwa na hoja 49.

Mheshimiwa Spika, ili kuliwezesha Bunge kupata taswira ya mwitiko katika utekelezaji, Taarifa hii imefafanua hatua zilizofikiwa katika utekelezaji. Kwa rejea ya mjadala Jedwali Na. 1 linafafanua hatua kwa kila Wizara. Hata hivyo, naomba sasa kufafanua hatua hizo kama ifuatavyo:

2.3.1 Hatua ya Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo iliyohakikiwa na kusubiri Namba ya Tangazo la Serikali

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kurekebisha dosari katika Sheria Ndogo, unataka mamlaka inayohusika, iandae Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo. Kwa kawaida Rasimu hiyo hupelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki. Baada ya hatua hiyo, Sheria Ndogo hupewa Namba na kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi unaonesha kwamba, mapendekezo kuhusu dosari katika Sheria Ndogo Nne, yamefanyiwa kazi kufikia hatua ya kusubiri kuchapishwa kwenye Gazeti la Serikali. Wizara zinazohusika na Sheria Ndogo hizo ni Wizara ya Afya na Wizara ya Madini. Kwa kufikia hatua hiyo ya juu katika utekelezaji, Kamati inapongeza mamlaka zinazohusika na Sheria Ndogo hizo.

Mheshimiwa Spika, Hatua iliyofikiwa na wizara hizo, inafanikisha dhamira ya Bunge kuondoa dosari katika Sheria Ndogo. Lengo ni kuondoa changamoto inayoweza kusababishwa na sheria ndogo katika hali halisi ya

utekelezaji. Kwa mfano, hatua ya marekebisho katika Sheria Ndogo chini ya Wizara ya Afya imetatusa changamoto inayogusa hali halisi.

Mheshimiwa Spika, kufafanua mfano huo, Kanuni za Usajili wa Maeneo ya Famasi zilitoa tafsiri ya duka la jumla la kuuza dawa tofauti na tafsiri iliyotolewa na Bunge katika Sheria Mama. Hatua nzuri ya utekelezaji wa mapendekezo inarudisha sheria ndogo katika wigo uliowekwa na sheria Mama. Hata hivyo, ingelifaa zaidi kama mamlaka zinazohusika zingelikuwa zimekamilisha hatua hiyo mapema.

2.3.2 Hatua ya Maandalizi ya Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo kwa ajili ya Uhakiki na Kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mapendekezo kuhusu Sheria Ndogo ishirini, hatua iliyofikiwa ni uandaaji wa Rasimu kwenye Mamlaka zinazohusika. Hatua hiyo, ni ya mwanzo wa mchakato ikisubiri hatua kuu zingine mbili.

Wizara zinazohusika na Sheria Ndogo hizo ni tano ambazo ni, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Wizara Maliasili na Utalii, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ofisi ya Rais TAMISEMI na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, hatua ya mamlaka hizo kuanza utekelezaji inatoa matumaini kuwa, dosari zilizopo zitarekebishwa. Hata hivyo, imechukua takriban miezi saba kwa mamlaka zinazohusika kuwa kwenye hatua ya Rasimu ya marekebisho.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uainishaji huo, Kamati ilibaini kuwa, zipo hoja ambazo hazijafanyiwa kazi kabisa hadi kufikia tarehe 7 Februari, 2022. Hoja hizo zilibainika katika Sheria Ndogo zilizozopo katika hatua ya Rasimu. Kwa mfano, dosari ya Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama,

2021 haijafanyiwa kazi. Sheria Ndogo hiyo, inaweka sharti la malipo ya Ada ya kuonesha sinema au video. Wakati huo, Kanuni za Filamu na Michezo ya Kuigiza zimeweka tozo ya kibali cha kuendesha shughuli za sinema.

Mheshimiwa Spika, kutozingatiwa kwa pendekezo la marekebisho ya sheria ndogo hiyo kunawabebesha mzigo wananchi wanaojishughulisha na uendesaji wa sinema na video. Bunge haliwezi kuacha mamlaka yake ya kutunga sheria yaliyokabidhiwa kwa mamlaka nyingine yatumiwe kubebesha mzigo wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni kuwa dosari yoyote inayobainika katika sheria Ndogo, ambayo inazuia ufanisi wa Serikali katika kuboresha maisha ya wananchi inastahili kurekebishwa haraka. Miezi saba ni kipindi kirefu kuendelea na dosari inayobebesha wananchi mzigo bila kurekebishwa.

SEHEMU YA TATU

3.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO AMBAZO ZILIWASILISHWA KATIKA MKUTANO WA TANO

3.1 Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 9 Novemba, 2021, katika Mkutano wa Tano, Serikali iliwasilisha Mezani nakala za Magazeti ya Serikali na nyongeza zake zikiwemo jumla ya Sheria Mia Moja na Thelathini (130). Mchanganuo wa sheria ndogo hizo ni kama ifuatavyo:-

- (i) Sheria Ndogo za Halmashauri (*By-Laws*) – 1
- (ii) Kanuni za Wizara (*Regulations*) – 19;
- (iii) Amri (*Orders*) – 14;
- (iv) Matangazo (*Notices*) – 94; na
- (v) *Rules* – 2.

3.2 Matokeo ya Uchambuzi

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchambuzi yanabainisha jumla ya dosari ishirini na moja zinazoripotiwa katika Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Tano wa Bunge. Kwa urahisi wa kufuatilia dosari hizo, Taarifa hii imeambatisha Jedwali la Uchambuzi wa Sheria Ndogo kwa rejea wakati wa mjadala na uamuzi. Naomba Jedwali hilo liingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge na hasa kuhusu kuweka mtiririko mzuri wa mchakato wa udhibiti wa Sheria Ndogo zilizochambuliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, mchanganuo wa dosari hizo unaonesha kuwa:

- (i) Jumla ya sheria ndogo moja imebainika kuwa na dosari ya kukinzana na masharti ya sheria inayotoa mamlaka ya kutungwa kwa sheria ndogo inayohusika na sheria nyingine za nchi;
- (ii) Sheria ndogo nane zimebainika kuwa na dosari ya kutoendana na misingi bora ya uandishi wa sheria (drafting

principles) na uandishi wa majedwali ya sheria ndogo inayohusika jambo linaloathiri utekelezaji wake; na

- (iii) Sheria Ndogo mbili zimebainika kuwa na dosari za kuweka masharti yasiyo na uhalisia hivyo, kutokuwa na urahisi wa utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, katika mchanganuo huo baadhi ya Sheria Ndogo zinajumuishwa katika aina zaidi ya moja ya dosari. Kwa sababu hiyo jumla ya idadi ya Sheria Ndogo inaweza isifikiwe kwa kujumlisha idadi katika mchanganuo huo. Pamja na hayo naomba kueleza

3.2.1 Kukinzana na Masharti ya Mama na Sheria Nyingine za Nchi

Mheshimiwa Spika, sheria ndogo hutungwa kwa madhumuni ya kufanikisha lengo kuu la Sheria Mama. Aidha, sheria ndogo zinatarajiwa kuendana na masharti ya Sheria nyingine za nchi. Hata hivyo, uchambuzi umeonesha kuwa baadhi ya sheria ndogo zilikuwa na maudhui yanayotofautiana na yale ya Sheria Mama au Sheria Nyingine za Nchi. Kwa mfano, Kanuni ya 2 ya sheria ndogo iitwayo *The Tanzania Medicines and Medical Devices (Laboratory Analysis of Medical and Non-Medical Products) Regulations, 2021* inavuka wigo wa Sheria mama. Kanuni hiyo imezipa maabara zilizo chini ya TMDA jukumu la kufanya uchunguzi wa kimaabara katika udongo, sampuli za binadamu na wanyama. Kwa masharti hayo, Kanuni hiyo inatoka nje ya lengo la Sheria mama ambalo ni udhibiti wa dawa, vifaa tiba, dawa za asili pamoja na sumu.

Mheshimiwa Spika, ikiwa Bunge lako tukufu litaruhusu utaratibu unaowekwa na Kanuni hiyo, basi litakuwa linabariki uvunjaji wa Sheria ya Tafsiri ya Sheria Sura ya 1, ambayo chini ya Kifungu cha 36(1) imeelekeza bayana kuwa Sheria Ndogo haipaswi kukinzana na Sheria Mama iliyoionda na ikiwa sheria ndogo itakinzana basi inakuwa na bitili.

3.2.2 Kutoendana na Misingi Bora ya Uandishi wa Sheria

Mheshimiwa Spika, Sheria za Bunge huandikwa kwa kuzingatia misingi ya uandishi wa Sheria. Misingi hiyo huwezesha kuweka mawazo ghafi katika ukamilifu unaoeleweka na wenye maana katika masharti ya sheria inayohusika. Bunge hili, huzingatia misingi hiyo kutokana na kazi nzuri ya Mwandishi Mkuu wa Sheria Nchini. Hivyo, sheria ndogo pia zinatarajiwa kuzingatia ipasavyo misingi ya uandishi wa sheria. Lakini, Sheria ndogo 8 zimebainika kuwa na dosari ya kutoendana na misingi ya uandishi wa sheria.

Mheshimiwa Spika, Mfano wa Sheria Ndogo yenye dosari hiyo ni *The Tanzania Medicines and Medical Devices (Fees and Charges) Regulations, 2021*. **Kipengele cha 65 hadi 68 vya Jedwali la Kwanza** la Kanuni hizo, vinahusu ada mbalimbali kwa huduma ya majaribio ya tiba kimaabara "*clinical trials*". Ada hizo zimeainishwa kwa katika viwango vya kuanzia dola za marekani 300, 500 na 1000. Uainishaji huo hauoneshi iwapo huduma inayokusudiwa kulipiwa viwango hivyo, ni kwa ajili ya watafiti wa tiba wa ndani au kutoka nje ya Tanzania. Dosari hiyo, inaweza kusababisha watafiti wadogo wa dawa wa ndani ya nchi watozwe kiwango kikubwa cha ada za utafiti kinyume na lengo lililokusudiwa.

3.2.3 Kukosa Uhalisia

Mheshimiwa Spika, Pamoja na mambo mengine, Utungaji wa Sheria ambao ni mzuri huzingatia uhalisia wa utekelezaji wa sheria inayohusika. Mojawapo ya mambo ya uhalisia yanayozingatiwa ni hali halisi ya walengwa wa sheria inayohusika. Lakini Sheria ndogo 2 zimebainika kuwa na changamoto ya kukosa uhalisia. Kwa mfano, **Kanuni ya 22(2) ya *The Tanzania Medicines and Medical Devices (Laboratory Analysis of Medical and Non Medical Products) Regulations, 2021*** inaweka masharti yanayokosa uhalisia.

Mheshimiwa Spika, Kanuni hiyo inaipa TMDA mamlaka ya kugawa dawa au vifaa tiba ilizochukuwa kama sampuli kutoka kwa wasambazaji au wazalishaji. Ugawaji huo unatakiwa hufanyika baada ya kubainika kuwa sampuli hizo hazina madhara. Tatizo la masharti hayo ni kutokuweka utaratibu wa sampuli hizo kurejeshwa kwa mzalishaji au msambazaji ili waendeleo kuzifanyia biashara au matumizi mengine yoyote kwa kadri walivyokusudia.

Mheshimiwa Spika, Ili tija ya Bunge kukabidhi madaraka ya kufafanua sheria kwa mamlaka nyingine ipatikane, matokeo ya matumizi ya madaraka hayo, yanapaswa kuzingatia dhamira ya Bunge katika sheria mama. Aidha, mamlaka hizo hazitarajiwi kuweka masharti yanayotofautiana na uhalisia wa mambo au kutozingatia misingi inayozingatiwa na Bunge lenyewe.

SEHEMU YA NNE

4.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

4.1 Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii imeonesha shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha mwaka mmoja. Madhumuni ya kufanya hivyo kama ilivyotajwa katika kanuni ya 136 (15) ya kanuni za Bunge, ni kuliwezsha Bunge kujadili na kutoa uamuzi. Kwa kuwa shughuli za Kamati hii zinahusu nafasi ya Bunge katika utungaji wa sheria, mjadala wake unahitaji umakini na nuzingatiaji wa mambo ya msingi. Aidha, kwa kuzingatia kuwa sheria ndogo zinagusa moja kwa moja maisha halisi ya ya wananchi, naliomba Bunge lako tukufu lifanyie kazi mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, ili kupata muungano wa uchambuzi na mapendekezo naomba kubainisha mtazamo wa jumla wa Kamati unaotokana na uchambuzi. Muhtasari wa mtazamo huo upo kwenye mambo sita kama ifuatavyo:-

4.1.1 Sheria Ndogo Kukinzana na Masharti ya Sheria Mama

Mheshimiwa Spika, sheria ndogo zinazokinza na sheria mama, hazisaidii ufafanuzi wa sheria kinyume na ilivyokusudiwa. Hali hiyo inaweza kuathiri tija na madhumuni ya Sheria mama. Aidha, sheria ndogo yenye dosari hiyo, haiendani na mantiki ya Bunge kukabidhi madaraka ya kufafanua sheria kwa mamlaka zingine. Kwa sababu hiyo, ni maoni ya Kamati kuwa upo umuhimu wa kurekebisha sheria ndogo zenye dosari hiyo ili ziendane na masharti ya sheria mama.

4.1.2 Sheria Ndogo kutozingatia Misingi ya Uandishi bora wa Sheria

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa sheria ndogo ni sehemu ya sheria za nchi, uandishi wake unapaswa kuzingatia misingi inayotumika katika sheria za Bunge.

Uandishi wa namna hiyo, unaisaidia sheria ndogo kuwa na nguvu ya kisheria na kufanikisha madhumuni ya sheria mama. Kupata uwezo huo, sheria ndogo zinapaswa kuendana na misingi ya uandishi wa sheria. Kwa sababu hiyo, Kamati ina maoni kwamba, marekebisho ya sheria ndogo zinazotofautiana na misingi ya uandishi yanahitaji kupewa msukomo.

4.1.3 Sheria Ndogo kuwa na Masharti yasiyozingatia Uhalisia

Mheshimiwa Spika, uhalisia wa mambo ikiwemo urahisi wa utekelezaji wa sheria ndogo ni jambo la msingi. Uhalisia huo ni pamoja na kuendana na hali halisi ya uchumi wa walengwa wa sheria ndogo inayohusika. Sheria ndogo zisizoendana na uhalisia, haziwezi kufanikisha dhima ya kuifafanua sheria mama. Kwa msingi huo, masharti yoyote ya Sheria ndogo yenye dosari ya kukosa uhalisia yanakinzana na kiini cha Sheria mama kuweka kifungu wezeshi cha kutungwa kwa sheria ndogo inayohusika. Kamati ina maoni kwamba, masharti ya sheria ndogo yasiyoendana na uhalisia hayapaswi kuendelea kuwepo kwenye sheria ndogo zilizochambuliwa.

4.1.4 Sheria Ndogo kukosa Usahihi na Ufasaha katika Uandishi wa Majedwali

Mheshimiwa Spika, majedwali katika sheria kurahisisha ufafanuzi wa masharti yake. Kasoro yoyote katika uandishi wa majedwali inaathiri ufasaha wa sheria inayohusika. Dosari katika uandishi wa majedwali ya sheria ndogo inatatiza ufasaha wa sheria ndogo na kuzuia isifanikiwe kufafanua sheria mama. Kamati ina maoni kwamba, sheria ndogo zenye dosari kuhusu usahihi na ufasaha katika uandishi wa majedwali, zinasababisha mkanganyiko katika utekelezaji. Kwa sababu hiyo, ni vizuri dosari hizo zirekebishwe na majedwali kama ni lazima yaandikwe inavyostahili.

4.1.5 Uchelewaji katika Kutekeleza Mapendekezo ya Kurekebisha Sheria Ndogo

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo yaliyopitishwa na Bunge kuhusu Sheria Ndogo zilizowekwa mezani wakati wa mkutano wa pili, yalitokana na kubainika kwa dosari katika sheria ndogo zinazohusika. Athari ya baadhi ya dosari hizo inagusa maisha halisi ya wananchi wanaowakilishwa katika Bunge hili. Kwa msingi huo, Bunge lisingeliweza kutarajia utekelezaji wa mapendekezo uchelewe. Aidha, hatua ya kutozingatia mapendekezo ya kuondoa dosari zilizobainika, inaendeleza madhara kwa wananchi kutokana na dosari zilizopo. Ni maoni ya Kamati kwamba, mamlaka zinazohusika na utungaji wa sheria ndogo, zinahitaji kuzingatia umuhimu wa kufanyia kazi ipasavyo mapendekezo ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasisitiza kuwa, Bunge linapokabidhi madaraka ya kutunga sheria ndogo kwa mamlaka zingine, linatarajia uzingatiaji wa madhumuni ya sheria mama. Aidha, Mapendekezo yanayotolewa Bungeni kwa ajili ya kurekebisha dosari, hayapaswi kuchukua muda mrefu kabla ya kufanyiwa kazi. Ni maoni ya Kamati kuwa mamlaka zinazohusika na sheria ndogo zinazobainika kuwa na dosari, zinahitaji kuzingatia ipasavyo umuhimu wa kurekebisha haraka dosari zinazobainika.

4.1.6 Kutokutekelezwa kwa Mapendekezo

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba msingi wa mapendekezo kuhusu kuondoa dosari zinazobainika, unalenga kuondoa changamoto zinazoweza kusababishwa na utekelezaji wa Sheria Ndogo. Kutokutekelezwa kabisa kwa mapendekezo kunaendeleza kero na changamoto kwa wanaguswa na utekelezaji wa Sheria Ndogo. Kamati ina maoni kuwa,

4.1.7 Ushirikishwaji hafifu wa Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria katika Mchakato wa Uwalishaji wa Majibu mbele ya Kamati

Mheshimiwa Spika, Ushirikishwaji wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika mchakato wa utungaji wa Sheria zote nchini ni wa kisheria. Kutokushirikishwa kwa Ofisi hii katika hatua za utungaji na marekebisho ya Sheria Ndogo kunasababisha sheria nyingi kuwa na dosari. Baadhi ya dosari hizo zinasababisha kero kwa wananchi jambo ambalo chombo cha uwakilishi wa wananchi kisingelipenda iwe hivyo. Kamati ina maoni kwamba, mamlaka zinazohusika na utungaji wa sheria ndogo, zinapaswa kuzingatia umuhimu wa kushirikishwa kwa Mwandishi Mkuu wa Sheria nchini kama linavyofanya Bunge lenye mamlaka ya asili ya utungaji wa sheria.

4.1.8 Ushirikishwaji wa Wadau katika Utungaji wa Sheria Ndogo

Mheshimiwa Spika, Utungaji wa sheria yoyote unahitaji ushirikishaji wa wadau. Utaratibu huo wa kushirikisha wadau unasaidia upatikanaji wa sheria jumuiifu, yenye uhalisia na inayotekelezeka. Kutoshirikisha wadau kikamilifu ni jambo linaloweza kusababisha baadhi ya mambo muhimu yasizingatiwe inavyostahili na hivyo kutatiza utekelezaji wa sheria. Ni Maoni ya Kamati kuwa, utungaji wa Sheria Ndogo usioshirikisha wadau kikamilifu unaweza kusababisha kukosekana kwa uhalisia, ugumu wa utekelezaji pamoja na kutokubalika kwenye jamii.

4.1.9 Utozaji wa ada zinazofanana unaotekelezwa na mamlaka zaidi ya moja.

Mheshimiwa Spika, utozaji wa ada unaofanywa na mamlaka zaidi ya moja katika chanzo kimoja, unaweza kuwa ni chanzo cha kuzorotesha ustawi wa shughuli zinazotekelezwa na wananchi. Kamati ina maoni kwamba,

utozaji wa ada zinazofanana katika chanzo kimoja unaweka ugumu wa uendeshaji wa shughuli za wananchi hususan wenye kipato cha chini.

4.2 Mapendekezo

Mheshimiwa Spika, sasa naliomba Bunge lako tukufu lizingatie maelezo ya jumla niliyoyatoa, ufafanuzi wa matokeo ya uchambuzi na maoni ya Kamati ili lijadili na kutoa uamuzi wa hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Tano wa Bunge. Ikumbukwe kuwa, hoja hii inahusu eneo muhimu la utekelezaji wa sheria ambalo lisipoangaliwa kwa umakini linaweza kusababisha kero katika jamii.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa hoja ili Bunge lako liazimie kama ifuatavyo:-

4.2.1 Kukinzana na masharti ya sheria inayotoa mamlaka ya kutungwa kwa sheria ndogo au sheria nyingine za nchi

KWA KUWA, zipo sheria ndogo zilizobainika kuwa na vifungu vinavyokinzana na masharti ya Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi, jambo linaloweza kuathiri tija ya utekelezaji wa Sheria mama inayohusika,

NA KWA KUWA, sheria ndogo inayokinzana na sheria mama au sheria nyingine za nchi, haiendani na masharti ya sheria ya tafsiri ya sheria, hali inayoisababisha kuwa batili kwa mujibu wa Kifungu cha 36 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria Sura ya 1,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zilizotunga Sheria Ndogo zenye kukinzana na masharti ya sheria mama na sheria nyingine za nchi, zirekebishe sheria ndogo hizo.

4.2.2 Kutozingatia Misingi ya Uandishi Bora wa Sheria

KWA KUWA, zipo sheria ndogo zilizowekwa mezani wakati wa mkutano wa Tano wa Bunge ambazo hazikuzingatia misingi ya uandishi bora wa sheria,

NA KWA KUWA, kutozingatiwa kwa misingi ya uandishi wa sheria ni jambo linaloondoa urahisi na kutabirika kwa sheria ndogo, na hivyo kuathiri tija sheria,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zilizokabidhiwa madaraka ya kutunga Sheria Ndogo zilikutwa na dosari ya kutozingatia misingi ya uandishi bora wa sheria, zirekebishe dosari hiyo.

4.2.3 Masharti Yasiyo na Uhalisia

KWA KUWA, zipo baadhi ya sheria ndogo zenye masharti yanayokinzana na uhalisia,

NA KWA KUWA, masharti hayo yanaweza kuathiri utekelezaji na tija iliyokusudiwa,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zinazohusika na kutungwa kwa Sheria Ndogo zilizobainika kuwa na masharti yasiyozingatia uhalisia, zifanye marekebisho haraka.

4.2.4 Dosari ya Uandishi wa Majedwali

KWA KUWA, baadhi ya Sheria Ndogo zina dosari katika uandishi wa majedwali, ilihali Kifungu cha 25 (2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kinatambua majedwali kuwa sehemu ya Sheria,

NA KWA KUWA, dosari hizo zinaathiri ukamilifu na kutatiza utekelezaji sheria ndogo inayohusika,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zilizotunga Sheria Ndogo na kubainika kuwa na dosari katika uandishi wa majedwali zifanye marekebisho.

4.2.5 Uchelewaji katika Kutakeleza Mapendekezo ya Kurekebisha Sheria Ndogo

KWA KUWA, kuchelewa kutekeleza mapendekezo ya kurekebisha sheria ndogo ni kuendeleza athari zinazotokana na dosari hizo,

NA KWA KUWA, athari hizo haziendani na madhumuni ya Bunge kukabidhi majukumu ya kufafanua sheria kupitia sheria ndogo, jambo linalotatiza malengo ya sheria mama,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zilizobainika zimechelewa kutekeleza mapendekezo ya kurekebisha Sheria Ndogo zilizokutwa na dosari, zikamilishe haraka mchakato wa marekebisho.

4.2.6 Kutokutekelezwa kwa Mapendekezo

KWA KUWA, yapo mapendekezo ya kurekebisha dosari katika sheria ndogo ambayo hadi kufikia tarehe 7 Februari, 2022, hayakuwa yamefanyiwa kazi kabisa,

NA KWA KUWA, kutozingatiwa kabisa kwa mapendekezo hayo ni kuendelea kuwabebesha mzigo wananchi wanaoguswa na Sheria ndogo zinazohusika,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zilizobainika kutokuwa zimeanza utekelezaji wa mapendekezo ya Bunge yaliyohusu kurekebisha dosari katika sheria ndogo:

- (i) zitekeleze mapendekezo hayo haraka; na
- (ii) zitoe taarifa kwa Kamati ya Sheria Ndogo kuhusu ya hatua inayofikiwa, kabla ya kuahirishwa kwa Mkutano wa Saba wa Bunge.

4.2.7 Ushirikishwaji Hafifu wa Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria katika Mchakato wa Uwalishaji wa Majibu mbele ya Kamati

KWA KUWA, imebainika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ndio yenye dhamana ya Uandishi wa Sheria.

NA KWA KUWA, Kamati imebaini ushirikishwaji mdogo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika eneo la Sheria Ndogo, hali inayopelekea kuendelea kuwepo kwa dosari nyingi katika Sheria Ndogo na kuleta usumbufu kwa watumiaji wake.

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Taasisi zinazotunga au kufanya marekebisho mbalimbali katika Sheria Ndogo, zishirikishe inavyostahili na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

4.2.8 Ushirikishwaji wa Wadau katika Utungaji wa Sheria Ndogo

KWA KUWA, baadhi ya sheria ndogo zimekosa mambo ya msingi kwa utekelezaji wake kutokana na ushirikishaji wa wadau usio wa kikamilifu.

NA KWA KUWA, upungufu huo umezuia upatikana wa mawazo jumuiifu na kutatiza utekelezaji wake kutokana na manung'uniko ya wadau,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zilizokabidhiwa madaraka ya kutunga Sheria Ndogo, zizingatie umuhimu wa kuwashirikisha wadau kikamilifu katika mchakato wa utungaji wa sheria hizo

4.2.9 Utozaji wa Ada zinazofanana Unaotekelezwa na Mamlaka zaidi ya Moja

KWA KUWA, zipo Kanuni ambazo kwa pamoja zinatoza ada za vibali vya kuendesha kumbi za sinema/video na michezo ya kuigiza;

NA KWA KUWA, utozaji huo unaweka ugumu wa utekelezaji wa shughuli hizo katika jamii ya watu wenye kipato cha chini, hivyo kuongeza kero kwa wananchi kinyume na matarajio ya kuboresha ustawi wao,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zinazohusika na Sheria Ndogo zilizobainika kutoza kwa pamoja ada zinazofanana katika chanzo kimoja:

- (i) zikamilishe mchakato wa kupitia Sheria Ndogo hizo ili kuhuisha viwango vya ada; na
- (ii) Zizingatie umuhimu wa kuweka masharti yasiyoweka ugumu wa utekelezaji wake kwa watu wenye kipato cha chini.

SEHEMU YA TANO

5.0 HITIMISHO

5.1 Shukrani

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na Bunge lako tukufu kwa kuweka utaratibu wa Taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo kuwasilishwa katika Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo kwa kazi kubwa na nzuri ya kuchambua Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Pili, Mkutano Tatu, Mkutano wa Nne na Mkutano wa Tano wa Bunge na hatimaye kufanikisha taarifa hii. Kwa heshima kubwa naomba kuwatambua majina yao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Dkt. Jasson Samson Rweikiza, (Mb) – Mwenyekiti;
2. Mhe. Kilumbe Shabani Ng'enda, (Mb) Makamu Mwenyekiti;
3. Mhe. Ramadhan Suleiman Ramadhan, (Mb);
4. Mhe. Idrissa Juma Abdul-Hafar, (Mb);
5. Mhe. Simai Hassan Sadiki, (Mb);
6. Mhe. Sylvia Francis Sigula, (Mb);
7. Mhe. Emmanuel Mageni Kasalali, (Mb);
8. Mhe. Ndaisaba George Ruhoro, (Mb);
9. Mhe. Edwin Enosy Swalle, (Mb);
10. Mhe. Judith Salvio Kapinga, (Mb);
11. Mhe. Santiel Erick Kirumba, (Mb);
12. Mhe. Jacob Tarimo Priscus, (Mb);
13. Mhe. Regina Ndege Qwaray, (Mb);
14. Mhe. Esther Edwin Malleko, (Mb);
15. Mhe. Amour Khamis Mbarouk, (Mb);
16. Mhe. Esther Lukago Midimu, (Mb);

17. Mhe. Minza Simon Mjika, (Mb);
18. Mhe. Khamis Ali Vuai, (Mb);
19. Mhe. Nicholas George Ngassa, (Mb);
20. Mhe. Humphrey Hesron Polepole, (Mb);
21. Mhe. Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, (Mb);
22. Mhe. Dkt. Medard Matogolo Kalemani, (Mb); na
23. Mhe. Eng. Dkt. Leonard Madaraka Chamuriho, (Mb).

Mheshimiwa Spika, Kwa moyo wa dhati kabisa nimshukuru Mhe. Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana (MB) – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) kwa uratibu ambao umeiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, niwashukuru Mawaziri na Naibu Mawaziri wa sekta mbalimbali kwa kufika mbele ya Kamati na kujibu hoja zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushiriki wao katika vikao vya uchambuzi wa Sheria Ndogo mbalimbali. Vilevile niwashukuru wadau mbalimbali waliofika mbele ya Kamati na kuwasilisha maoni yao na wale wote ambao waliwasilisha maoni yao kwa maandishi (*submissions*). Ushiriki wao katika vikao vya Kamati pamoja na maoni waliyowasilisha yamekuwa na manufaa kwa Kamati katika utekelezaji bora wa shughuli zake. Wadau hao ni:-

1. Shirikisho la Filamu Tanzania;
2. HAKIELIMU;
3. Chama cha Walimu Tanzania (CWT);
4. (*Association of Real Estate Professionals of Tanzania (AREPTA)*);
5. UWEZO TANZANIA;
6. Chama cha Wafamasia Tanzania (*The Pharmaceutical Society of Tanzania*);

7. Chama cha Wataalamu wa Mazingira Tanzania ((*Tanzania Environmental Experts Association*)(TEEA));
8. Chama cha Wavuvi Tanzania (*Tanzania Fisheries Union*)(TAFU));
9. Chama cha Wavuvi Wadogo wadogo, Minazi Mikinda (CHAWAWAMI); na
10. Chama cha Ushirika wa Wavuvi Mwalo wa Kigodeko (*Kigodeko Fisheries Cooperative*).

Mheshimiwa Spika, aidha napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi mahiri wa Katibu wa Bunge Bi. Nanelwa J. Mwiambi, *ndc* kwa ushirikiano wanaoipatia Kamati ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, nimshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, *ndc* akisaidiwa na Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Gerald S. Magili kwa usimamizi mzuri wa Shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu, niwashukuru Katibu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, Ndg. Mkuta Masoli, akisaidiwa na Msaidizi wa Kamati Bi. Imelda Ntimba kwa kuratibu vyema Shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

5.2 Hoja

Mheshimiwa Spika, Sasa naomba kutoa hoja kwamba, Bunge liipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo pamoja na maoni na mapendekezo yaliyotolewa katika Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.



Jasson S. Rweikiza (Mb)
MWENYEKITI

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo

18 Februari, 2022

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



BUNGE LA TANZANIA

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO

**JEDWALI LA UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA BUNGE KUHUSU SHERIA
NDOGO ZILIZOWASILISHWA WAKATI WA MKUTATO WA PILI WA BUNGE**

Orodha Ya Sheria Ndogo

The Pharmacy (Premises Registration) Regulations, 2020	1
The HIV and AIDS (Prevention and Control) Regulations 2020.....	3
Kanuni za Watumishi wa Taasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili za Mwaka 2020.....	3
Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru wa Madini ya Ujenzi) ya Halmashauri ya Wilaya ya Same, 2020.....	4
Sheria Ndogo za (Ada za Vibali vya Burudani za Halmashauri ya Wilaya ya Moshi), 2020.....	6
Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema 2020.	8
Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi, 2020	14
Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Njombe 2020	16
Sheria Ndogo za Ushuru wa Kituo cha Magari za Halmashauri ya Jiji la Mbeya, 2020.....	22
Sheria Ndogo za Hifadhi za Mazingira za Halmashauri ya Jiji la Mbeya, 2020	22
Sheria Ndogo za Afya na Usafi wa Mazingira za Halmashauri ya Jiji la Mbeya, 2020	25
Sheria Ndogo za Usimamizi wa Masoko za Halmashauri ya Jiji la Mbeya, 2020.....	26
Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, 2020	26
Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru) na Halmashauri ya Jiji la Mbeya, 2020	29
Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto, 2020	34
Sheria Ndogo za Kilimo na Hifadhi ya Chakula za Halmashauri ya Wilaya ya Itilima, 2020.....	36

JEDWALI NA. 1

Sheria Ndogo ya Uanzishaji wa Vikundi vya Watumiaji wa Maji za Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, 2020.....	36
The Mining (Mineral Rights Application by Tender) Regulations 2020.....	37
Kanuni za Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza, 2020	38
The Tanzania Wildlife Research Institute (Conduct of Wildlife Research) Regulations, 2020	46
The Wildlife Conservation (Administration and Management of Pasiansi Wildlife Training Institute) Regulations, 2020.....	46
The Valuation and Valuers Registration (Training Examination) Rules 2020	47
The Tanzania Teachers' Professional Board General, Regulations 2020.....	54

**JEDWALI LA UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA BUNGE KUHUSU SHERIA
NDOGO ZILIZOWASILISHWA WAKATI WA MKUTATO WA PILI WA BUNGE**

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
WIZARA YA AFYA					
1.	The Pharmacy (Premises Registration) Regulations, 2020 (GN NA. 269/17 Aprili, 2020)	<p>1. Kanuni ilirejea Kifungu cha 34 cha Sheria Mama kama moja ya Kifungu kinachotoa mamlaka ya kutungwa kwa Kanuni hii.</p> <p>Ilibainika kwamba, Kifungu cha 34 hakihusiki moja kwa moja na Mamlaka ya Wazari kutunga Kanuni hizi, badala yake kinaweka katazo la kufanya shughuli zinazohusu uuzaji, utoaji na ugawaji wa dawa bila usajili.</p> <p>2. Kanuni ya 2 ilikuwa inaweka inatoa tafsiri ya duka la jumla la</p>	<p>1. Ilipendekezwa kuwa Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kufuta Kifungu cha 34 ambacho hakihusiani na kuanzishwa kwa Kanuni hizi na kubakisha Kifungu cha 55(f) ambacho ndicho kinatoa mamlaka kwa Waziri kutunga Kanuni hizi.</p> <p>2. Ilipendekezwa kuwa Kanuni ya 2</p>	<p>1. Rasimu ya marekebisho ya Kanuni imeandaliwa ili kufuta maneno Imetungwa chini ya Kifungu cha 34 na 55(f) na badala yake kuweka maneno “Imetungwa chini ya Kifungu cha 55(f)”.</p> <p>2. Rasimu ya marekebisho ya Kanuni ya 2</p>	<p>1. Mapendekezo yamezingatiwa na Kanuni imewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p> <p>2. Mapendekezo yamezingatiwa na Kanuni</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>kuuza dawa (wholesale pharmacy) kwamba ni pamoja na kununua dawa kutoka kwa wazalishaji wa ndani (local manufactures) tofauti na tafsiri ya Sheria mama.</p> <p>Changamoto iliyobainika ni kwamba Tafsiri inayotolewa na Sheria Mama katika kifungu cha 2 haijaniisha ununuzi wa dawa kutoka kwa wazalishaji wa ndani (local manufactures) kama ilivyo katika tafsiri inayotolewa na Kanuni.</p>	<p>ifanyiwe marekebisho ili kuweka maana ya duka la jumla la kuuza dawa (wholesale pharmacy) kama inavyosomeka katika Kifungu cha 2 cha Sheria Mama.</p>	<p>imeandaliwa ambapo tafsiri ya maneno “wholesale pharmacy” imerejea tafsiri iliyowekwa kwa mujibu wa sheria mama.</p>	<p>imewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		3. Kanuni hazijaweka ukomo wa muda wa kusitisha cheti cha usajili tofauti na Sheria mama ambayo katika Kifungu cha 49 (5) inaweka ukomo wa muda wa kusitisha cheti, kwamba usivuke miezi kumi na mbili.	3. Ilipendekezwa Kanuni zifanyiwe marekebisho ili kuweka ukomo wa muda wa kusitisha cheti cha usajili katika Kanuni.	3. Wizara inasubiri mchakato wa marekebisho ya Sheria Mama ili kuweka muda wa kusitisha usajili husika.	3. Kutokutekelezwa kwa Pendekezo kuna tija.
2.	The HIV and AIDS (Prevention and Control) Regulations 2020 GN NA. 770 18 Septemba 2020	Kanuni ya 22 (2), 23 (2) (ii) na 24 (1) za Kanuni zinaonesha kwamba zinaanzisha Jedwali la Nne. Changamoto iliyobainishwa na Kamati ni kwamba Jedwali la Nne linalorejewa na Kanuni hizo halikuwepo.	Ilipendekezwa kuwa Sehemu ya Majedwali ifanyiwe Marekebisho ili kuweka Jedwali la Nne linalotajwa na Kanuni ya 22 (2), 23 (2) (ii) na 24 (1) ambalo halikuwepo.	Rasimu ya marekebisho ya imeandeliwa ili kuweka Jedwali la Nne lenye kichwa cha habari “Huduma za Uchunguzi (HIVST), Upimaji wa VVU, Uhakiki Ubora na Vitendanishi” .	Mapendekezo yamezingatiwa na Kanuni imewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.
3.	Kanuni za Watumishi wa Taasisi ya Tiba	1. Kanuni ilikuwa na dosari katika Jedwali la Kwanza	1. Ilipendekezwa Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi	1. Rasimu ya marekebisho ya imeandaliwa ili kurekebisha Jedwali la	1. Mapendekezo yamezingatiwa na Kanuni imewasilishwa katika Ofisi

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
	<p>ya Mifupa Muhimbili za Mwaka 2020</p> <p>GN NA. 819 25 Septemba, 2020</p>	<p>ambapo lilirejea kimakosa kuanzishwa chini ya Kanuni ya 67(b) badala ya Kanuni sahihi ya 67(a).</p> <p>2. Kanuni ilikuwa na dosari katika Jedwali la Pili ambapo lilirejea kimakosa kuanzishwa chini ya Kanuni ya 67(a) badala ya Kanuni sahihi ya 67(b).</p>	<p>lifanyiwe marekebisho kwa kufanya rejea sahihi ya Kanuni ya 67(a)</p> <p>2. Ilipendekezwa Jedwali la Pili la Kanuni hizi lifanyiwe marekebisho kwa kufanya rejea sahihi ya Kanuni ya 67(b).</p>	<p>Kwanza kwa kufuta maneno “limetungwa chini Kanuni ya 67(b)” na badala yake kuandika maneno “limetungwa chini ya Kanuni ya 67(a)”.</p> <p>2. Rasimu ya marekebisho ya Kanuni inayorekebisha Jedwali la Kwanza imeandaliwa ili kufuta maneno “limetungwa chini Kanuni ya 67(a)” na badala yake kuandika “limetungwa chini ya Kanuni ya 67(b)”.</p>	<p>ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p> <p>2. Mapendekezo yamezingatiwa na Kanuni imewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p>
OFISI YA RAIS – TAMISEMI					
4.	<p>Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru wa Madini ya Ujenzi) ya Halmashauri ya Wilaya ya Same, 2020</p>	<p>Kamati ilibaini Kifungu cha 2 kilikuwa kinatoa tafsiri ya neno “madini ya ujenzi” kwa kuainisha aina kumi na mbili (12) za madini, yakiwemo</p>	<p>Ilipendekezwa kuwa Jedwali la Kwanza lifanyiwe marekebisho ili kujumuisha kiwango cha ada ya madini ya chokaa.</p>	<p>Rasimu ya marekebisho ya Jedwali la Kwanza imendaliwa ili kuweka ada ya shilingi 6000/- kwa tani moja ya madini ya chokaa.</p>	<p>Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yameandaliwa ili kufikishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
	(GN NA. 460/12 Juni 2020)	<p>madini ya chokaa. Hata hivyo Jedwali la Pili halijainisha madini ya chokaa na ushuru unaapaswa kulipwa kwa madini hayo kama ilivyo kwa madini mengine kumi na moja (11).</p> <p>Kwa madini ya chokaa kutokuorodheshwa kwenye jedwali la pili;</p> <p>Kwanza: kunaweza kuondoa uhalali wa kutoza ushuru wa madini ya chokaa, jambo linaloweza kuikosesha Halmashauri mapato yanayokusudiwa.</p> <p>Pili: kunaweza kusababisha halmashauri kutoza</p>			kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		ushuru wa madini ya chokaa bila mwongozo wa viwango, jambo linaloweza kusababisha kero kwa wananchi.			
5.	Sheria Ndogo za (Ada za Vibali vya Burudani za Halmashauri ya Wilaya ya Moshi), 2020 GN NA. 529 10 Julai, 2020	1. Kamati ilibaini Sehemu D kipengele cha Kwanza cha Jedwali la Kwanza iliweka ada ya kibali cha kuonesha Sinema au video kuwa ni kuanzia shilingi 300,000/- hadi 1,000,000/-. Aidha, sharti la utozaji wa ada hiyo pia limewekwa katika Kanuni za Filamu na Michezo ya Kuigiza, 2020 ambazo katika Jedwali Tatu sehemu ya tano	1. Ilipendekeza Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo zikae kwa pamoja ili kuhuisha viwango vya ada za kumbi za kuonesha sinema vinavyotozwa na Wizara hizo kwa pamoja, ili kuondoa wa ugumu wa utekelezaji wa shughuli hizi katika jamii ya watu wenye kipato cha chini, jambo ambalo linaongeza kero kwa	1. Pendekezo halijatekelezwa kwa kuwa OR – TAMISEMI na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo hawajakaa tofauti na ilivyopendekezwa. Maelezo Ofisi ya Rais-TAMISEMI inatoa maelezo kuwa hakuna muingiliano katika utozaji wa ada kwa kuwa Bodi ya Filamu inatoza katika vibali na ukaguzi wa filamu na Halmashauri ya Wilaya ya Moshi inatoza vibali	1. Kikao kazi cha Ofisi Rais TAMISEMI, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, BASATA na Bodi ya Filamu mapema ili kupitia Kanuni zinazohusu utozaji wa tozo katika sekta ya sanaa na burudani. Kwa lengo la kuhuisha Kanuni ili kuondoa maeneno yenye mgongano.

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>limeweka ada ya kibali cha kuendesha shughuli za kuonesha filamu kuanzia shilingi 50,000/- hadi 500,000/- kwa mwaka.</p> <p>Hali hiyo ilionekana inaweza kuongeza ugumu wa shughuli hizi katika jamii ya watu wenye kipato cha chini, jambo ambalo linaongeza kero kwa wananchi kinyume na matarajio ya kuboresha ustawi wao.</p>	<p>wananchi kinyume na matarajio ya kuboresha ustawi wao.</p>	<p>vya kuonesha filamu.</p>	
		<p>2. Sehemu F ya Jedwali la Kwanza iliweka sharti la malipo ya ada ya shilingi 50,000/- kwa</p>	<p>2. Ilipendekezwa marekebisho yafanyike katika Sehemu F ya Jedwali la Kwanza</p>	<p>2. Rasimu ya marekebisho ya Sehemu F ya Jedwali la Kwanza imendaliwa kwa kuongeza maneno "uhai wa kibali utakuwa</p>	<p>2. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yameandaliwa ili kufikishwa katika Ofisi ya</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		ajili ya kibali cha waganga wadogo kutoka ndani ya Halmashauri ili waweze kuendesha shughuli zao pasipo kubainisha uhai wa kibali kama ni siku, wiki, mwezi n.k	ili kuainisha muda wa uhai kibali cha kuendesha shughuli za waganga wadogo.	ni mwaka mmoja”.	Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.
6.	Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema 2020. GN NA. 670 21 Agosti 2020	1. Kamati ilibaini Sehemu ya Tano (V) ya Jedwali la Kwanza inaweka viwango vya ada na ushuru wa mifugo, minada, bidhaa na magulio mengine pasipo kuainisha iwapo ada na ushuru huo ni kwa siku, wiki, mwezi au mwaka. Hali hiyo ingeweza kusababisha utozaji wa ada na ushuru usiokuwa wa kueleweka miongoni	1. Ilipendekezwa marekebisho yafanyike katika Sehemu ya Tano (V) ya Jedwali la Kwanza ili kuainisha muda mahsusi uliolengwa kwa ushuru na ada wa mifugo, minada, bidhaa na magulio mengine.	1. Rasimu ya Marekbisho imeandaliwa ili kufanya marekebisho katika sehemu ya V ya Jedwali la Kwanza kwa lengo la kuainisha muda mahsusi wa utozaji ada na ushuru kuwa ni “siku ya mnada”.	1. Mape Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yameandaliwa ili kufikishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>mwa wananchi, jambo ambalo linaweza kuwa kero kwa wananchi.</p> <p>2. Kamati ilibaini Sehemu ya XII kipengele cha 3 cha Jedwali la kwanza inaweka sharti la malipo ya ushuru kwa ukumbi unaochukua watu 100 - 200 kuwa ni shilingi 50,000/= kwa siku na ukumbi unaochukua watu 300 - 500 unapaswa kulipiwa shilingi 100,000/= kwa siku.</p> <p>Utaratibu wa utozaji haukuwa ukibainisha iwapo mmiliki wa ukumbi atalipa kwa kila siku au kwa siku ya kazi au ya tukio, jambo linaloweza</p>	<p>2. Ilipendekezwa marekebisho yafanyike katika Kipengele cha 3 cha sehemu ya XII ya Jedwali la Kwanza ili kuonesha utozaji unaochukua watu ni kwa kuzingatia tukio lililofanyika.</p>	<p>2. Rasimu ya marekebisho ya Kipengele cha 3 cha sehemu ya XII ya Jedwali la Kwanza imeandaliwa ili kubainisha muda unaochukuliwa kuwa ni "siku ya tukio".</p>	<p>2. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatia ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yameandaliwa ili kufikishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>kuwa kero kwa wananchi kama hiliwekwi sawa.</p> <p>Namna hiyo ya utozaji ushuru, haioneshi kuzingatiwa kwa uhalisia wa shughuli.</p> <p>3. Kamati ilibaini mkanganyiko katika Sehemu ya XII, Kipengele cha 6 cha Jedwali la Kwanza lililpokuwa linaweka sharti la malipo ya ada na ushuru wa picha jongevu na mnato ya shilingi 30,000/- kwa tukio moja kwa siku. Hata hivyo, mkanganyiko kuhusu tukio linalokusudiwa. Mfano, jambo linalojiri na kuvutia kupiga picha au</p>	<p>3. Ilipendekezwa Sehemu ya XII, Kipengele cha 6 cha Jedwali la Kwanza ifanyiwe marekebisho kwa kubainisha bayana wapiga picha wanaokusudiwa na Sheria Ndogo hizi ili kuondoa uwezekano wa wapiga picha ambao hawafanyi shughuli katika sherehe au hafla mbalimbali kuwa sehemu ya kulipa ada ya shilingi</p>	<p>3. Rasimu ya Marekebisho katika Sehemu ya XII, Kipengele cha 6 cha Jedwali la Kwanza imeandaliwa kwa kuongeza maneno “wapiga picha za kibiashara na wafanya biashara za picha”.</p>	<p>3. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yameandaliwa ili kufikishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>upigaji wenyewe wa picha, n.k. Kwa vyovyote, iwavyo, sharti hilo bado linaonekana kutokuwa na uhalisia kiutekelezaji.</p> <p>4. Kamati ilibaini Kipengele cha 17 sehemu XII katika Jedwali la Kwanza kinaweka sharti la malipo ya ada kwa kumbi za video na mipira, ambapo shilingi 200,000/- inatozwa kwa ukumbi mkubwa, shulingi 150,000/- kwa ukumbi wa kati, shilingi 100,000 kwa ukumbi mdogo mjini na shilingi 50,000 ukumbi mdogo vijijini.</p> <p>Changamoto</p>	<p>30,000/-</p> <p>4. Ilipendekezwa marekebisho yafanyike katika Kipengele cha 17 sehemu XII katika Jedwali la Kwanza ili kuonesha idadi ya watu kwa kila ukumbi na kuonesha muda mahsusi wa malipo ya ada zilizobainishwa.</p>	<p>4. Rasimu ya marekebisho ya Kipengele cha 17 sehemu XII katika Jedwali la Kwanza ya imeandaliwa ambapo inaonesha muda mahsusi wa malipo ada kwa ukumbi wa kuonesha ni "kwa mwaka"</p>	<p>4. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yameandaliwa ili kufikishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>iliyobainishwa ni kuwa Sheria ndogo haioneshi kipimo cha upi ni ukumbi mkubwa, upi wa kati na mdogo hali inayoweza kuchangia utozaji kwa kuzingatia utashi binafsi. Aidha, haijabainishwa ada hizi zinalipwa kwa kipindi cha muda gani (Wiki, Mwezi au Mwaka).</p> <p>5. Kamati ilibaini kuwa Kipengele cha 17 sehemu XII katika Jedwali la Kwanza kiliweka sharti la malipo ya ada kwa kumbi za video ambapo shilingi 200,000/- inatozwa kwa ukumbi mkubwa, shilingi</p>	<p>5. Ilipendekezwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo zikae ili kuhuisha viwango vya ada za kuonesha sinema vinavyotozwa na Wizara hizo kwa pamoja, ili kuondoa</p>	<p>5. Pendekezo halijatekelezwa kwa kuwa OR – TAMISEMI na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo hawajakaa tofauti na ilivyopendekezwa.</p> <p>Maelezo</p> <p>Ofisi ya Rais-TAMISEMI inatoa maelezo kuwa</p>	<p>5. Ofisi Kikao kazi cha Ofisi Rais TAMISEMI, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, BASATA na Bodi ya Filamu mapema ili kupitia Kanuni zinazohusu utozwaji wa tozo katika sekta ya sanaa na burudani. Kwa lengo la kuhuisha Kanuni ili kuondoa maeneno yenye mgongano.</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>150,000/-kwa ukumbi wa kati, shilingi 100,000 kwa ukumbi mdogo mjini na shilingi 50,000 ukumbi mdogo vijijini.</p> <p>Aidha, Sharti la utozaji wa ada ya ukumbi pia limewekwa katika Kanuni za Filamu na Michezo ya Kuigiza, 2020 ambazo katika Jedwali Tatu sehemu ya tano limeweka ada ya kibali cha kuendesha shughuli za kuonesha filamu kuanzia shilingi 50,000/- hadi 500,000/- kwa mwaka.</p> <p>Kamati iliona kwamba utozaji wa</p>	<p>wa ugumu wa utekelezaji wa shughuli hizi katika jamii ya watu wenye kipato cha chini, jambo ambalo linaongeza kero kwa wananchi kinyume na matarajio ya kuboresha ustawi wao.</p>	<p>hakuna muingiliano katika utozaji wa wa ada kwa kuwa Bodi ya Filamu inatoza katika vibali na ukaguzi wa filamu na Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema inatoza vibali vya kuonesha filamu.</p>	

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		namna hiyo ungeweza kuongeza ugumu wa shughuli hizi katika jamii ya watu wenye kipato cha chini, jambo ambalo linaongeza kero kwa wananchi kinyume na matarajio ya kuboresha ustawi wao.			
7.	Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi, 2020 GN NA. 671 21 Agosti 2020	1. Kamati ilibaini Sehemu A kipengele cha 3 katika Jedwali la Kwanza inaweka sharti malipo ya maegesho ya shilingi 500 kwa <i>ferry</i> kila itakapopaki pasipo kuonesha iwapo inahusisha <i>ferry</i> za serikali.	1. Ofisi ya Rais – TAMISEMI iwasilishe mbele ya Kamati taarifa waliyoiomba kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi kuhusu ufafanuzi iwapo ushuru wa maegesho unahusisha <i>ferry</i> za serikali.	1. Rasimu ya marekebisho ya Sehemu A kipengele cha 3 katika Jedwali la Kwanza imeandaliwa ili kufuta sharti la malipo ya maegesho ya shilingi 500 kwa <i>ferry</i> za serikali.	1. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yameandaliwa ili kufikishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>2. Sehemu E ya Jedwali la Kwanza iliainisha viwango vya Ada za shughuli za burudani, ambapo Taasisi zitakazofanya shughuli za burudani (kuendesha kumbi za kuonesha filamu) zinapaswa kulipa kiasi cha shilingi 100,000/- kwa mwaka na Michezo ya maigizo shilingi 5,000./= kwa siku katika taasisi na shilingi 10,000/= kwa siku katika Ukumbi.</p> <p>Sharti la utozaji wa ada hizo pia limewekwa katika Kanuni za Filamu na Michezo ya Kuigiza, 2020 ambazo katika Jedwali Tatu</p>	<p>2. Ilipendekezwa kuwa, Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo zikae kwa pamoja ili kuhuisha viwango vya ada za kuendesha kumbi kuonesha sinema vinavyototwa na Wizara hizo kwa pamoja, ili kuondoa wa ugumu wa utekelezaji wa shughuli hizi katika jamii ya watu wenye kipato cha chini, jambo ambalo linaongeza kero kwa wananchi kinyume na matarajio ya kuboresha ustawi wao.</p>	<p>2. Pendekezo halijatekelezwa kwa kuwa OR – TAMISEMI na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo hawajakaa tofauti na ilivyopendekezwa.</p> <p>Maelezo</p> <p>Ofisi ya Rais-TAMISEMI inatoa maelezo kuwa hakuna muingiliano katika utozaji wa wa ada kwa kuwa Bodi ya Filamu inatoza katika vibali na ukaguzi wa filamu na Halmashauri ya Wilaya ya Messenyi inatoza vibali vya kuonesha filamu.</p>	<p>2. Ofisi ya Rais – Kikao kazi cha Ofisi Rais TAMISEMI,Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, BASATA na Bodi ya Filamu mapema ili kupitia Kanuni zinazohusu utozwaji wa tozo katika sekta ya sanaa na burudani. Kwa lengo la kuhuisha Kanuni ili kuondoa maeneno yenye mgongano.</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>sehemu ya kumi limeweka tozo ya kibali cha kuendesha michezo ya kuigiza kuanzia shilingi 36,000/- hadi 500,000/-.</p> <p>Hali hii inaweza kuongeza ugumu wa shughuli hizi katika jamii ya watu wenye kipato cha chini, jambo ambalo linaongeza kero kwa wananchi kinyume na matarajio ya kuboresha ustawi wao.</p>			
8.	<p>Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Njombe 2020</p> <p>GN NA. 777</p>	<p>1. Sehemu ya Nne (IV) ya Jedwali la Kwanza Kipengele cha 10 iliweka sharti la malipo ya ada ya chanjo ya mifugo pasipo kuainisha ada husika, hali</p>	<p>1. Ilipendekezwa marekebisho katika Sehemu ya Nne (IV) ya Jedwali la Kwanza Kipengele cha 10 ili kuainisha kiwango cha ada ya chanjo</p>	<p>1. Rasimu ya marekebisho ya Rasimu ya marekebisho ya Sehemu ya Nne (IV) ya Jedwali la Kwanza Kipengele cha 10 imeandaliwa ili kuweka kiwango cha</p>	<p>1. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yameandaliwa ili kufikishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
	18 Septemba 2020	<p>inayoweza kuchangia utozaji usiozingatia muongozo.</p> <p>2. Sehemu ya Sita (VI) ya Jedwali la Kwanza kipengele cha 4 iliweka ada ya kuonesha Sinema au video kuwa ni shilingi 50,000/- na kipengele cha kipengele cha 6 kimeweka ada ya shilingi 60,000/- kwa kuonesha sinema au video.</p> <p>3. Sehemu ya Sita (VI) ya Jedwali la Kwanza iliainisha viwango vya Ada za shughuli za kuonesha sinema na video kuwa ni shilingi</p>	<p>kinachopaswa kulipwa katika.</p> <p>2. Ilipendekezwa marekebisho yafanyike katika Sheria Ndogo ili kufuta kipengele cha kipengele cha 6 katika Sehemu ya Sita (VI) ya Jedwali la Kwanza kilichoweka ada ya shilingi 60,000/- kwa kuonesha sinema au video.</p> <p>3. Ilipendekezwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo zikae kwa pamoja ili kuhuisha viwango vya ada za</p>	<p>shilingi 1,000/- kwa chanjo</p> <p>2. Rasimu ya marekebisho ya Sehemu ya Sita (VI) ya Jedwali la Kwanza kipengele cha 4 imeandaliwa ili kufuta Kipengele cha 6.</p> <p>3. Pendekezo halijatekelezwa kwa kuwa OR – TAMISEMI na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo hawajakaa tofauti na ilivyopendekezwa.</p>	<p>kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p> <p>2. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yameandaliwa ili kufikishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p> <p>3. Kikao kazi cha Ofisi Rais TAMISEMI, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, BASATA na Bodi ya Filamu kifanyike mapema ili kupitia Kanuni zinazohusu utozwaji wa tozo katika sekta ya sanaa</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>50,000.</p> <p>Aidha, ilibainika kwamba sharti la utozaji wa ada hiyo pia ipo katika Kanuni za Filamu na Michezo ya Kuigiza, 2020 ambazo katika Jedwali Tatu sehemu ya tano limeweka ada ya kibali cha kuendesha shughuli za kuonesha filamu kuanzia shilingi 50,000/- hadi 500,000/- kwa mwaka. Hali hii inasababisha waendesha shughuli hizi kuwa na mzigo mkubwa wa malipo ili kuendesha shughuli hizo.</p>	<p>kuendesha kumbi kuonesha sinema vinavyotozwa na Wizara hizo kwa pamoja, ili kuondoa wa ugumu wa utekelezaji wa shughuli hizi katika jamii ya watu wenye kipato cha chini, jambo ambalo linaongeza kero kwa wananchi kinyume na matarajio ya kuboresha ustawi wao.</p>	<p>Maelezo</p> <p>Ofisi ya Rais-TAMISEMI inatoa maelezo kuwa hakuna muingiliano katika utozaji wa wa ada kwa kuwa Bodi ya Filamu inatoza katika vibali na ukaguzi wa filamu na Halmashauri ya Wilaya ya Njombe inatoza vibali vya kuonesha filamu.</p>	<p>na burudani. Kwa lengo la kuhuisha ili kuondoa maeneno yenye mgongano.</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>4. Sehemu ya Sita (VI) ya Jedwali la Kwanza kipengele cha 1 na Kipengele cha 5(c) kwa pamoja viliweka sharti la malipo ya ushuru shilingi 1,000/- wa maegesho kwa pikipiki na basi ndogo zisizozidi abiria arobaini na wanne (44). Masharti ya utozaji viwango sawa yanakosa uhalisia ukilinganisha ukubwa na matumizi ya vyombo hivi vya usafiri.</p> <p>5. Sehemu ya Nane (VIII) ya Jedwali la Kwanza ilionesha aina mbili za ukomo kipindi cha ada ya matangazo</p>	<p>4. Ilipendekezwa Sehemu ya Sita (VI) ya Jedwali la Kwanza ifanyiwe marekebisho ili kutofautisha viwango vya ushuru malipo ya ushuru maegesho ya pikipiki na mabasi madogo ya abiria wasiozidi arobaini na wanne (44) ili kuleta uhalisia wa malipo kwa walipaji.</p> <p>5. Ilipendekezwa marekebisho yafanyike katika Sehemu ya Nane (VIII) ya Jedwali la Kwanza kwa</p>	<p>4. Rasimu ya marekebisho ya Sehemu ya Sita (VI) ya Jedwali la Kwanza kipengele cha 1 na 5(c) imeandaliwa ili kuweka ushuru wa pikipiki kwa siku kuwa ni shilingi 200.</p> <p>5. Rasimu ya marekebisho ya Sehemu ya Nane (VIII) ya Jedwali la Kwanza imeandaliwa ili kufuta sharti la malipo ya ada kwa kipindi cha</p>	<p>4. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yameandaliwa ili kufikishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p> <p>5. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yameandaliwa ili kufikishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>inayopaswa kulipa inayolipwa, ambapo <i>column</i> ya tatu ilionesha ni kwa kipindi cha mwaka na sehemu mahsusi ya kila aina ya tangazo inaonesha malipo ya ada kwa siku.</p> <p>6. Sehemu ya Tisa (IX) ya Jedwali la Kwanza kipengele cha 2 iliweka sharti la malipo ada ya shilingi 200,000/- kwa ajili ya kibali cha ujenzi wa jengo la ghorofa moja na kuendelea.</p> <p>Aidha, Sheria Ndogo ziliweka sharti la malipo ya shilingi 150,000/- kama ada za vibali vya ujenzi</p>	<p>kuonesha aina moja ya ukomo wa malipo ya ada za matangazo unaokusudiwa kama ni kipindi cha mwaka mmoja au kwa siku.</p> <p>6. Ilipendekezwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI iwasilishe mbele ya Kamati majibu ya taarifa ya ufafanuzi waliyoiomba kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Njombe wa ada ya vibali vya ujenzi vinavyoainishwa katika Sehemu ya Tisa (IX) ya Jedwali la Kwanza kipengele cha 2 kuonesha iwapo</p>	<p>mwaka na badala yake malipo hayo yatakuwa kwa kipindi cha siku.</p> <p>6. Rasimu ya marekebisho ya Sehemu ya Tisa (IX) ya Jedwali la Kwanza imeandaliwa ili kufuta kipengele cha 6 kinachoweka sharti la malipo ya shilingi 150,000/- kama ada za vibali vya ujenzi kwa taasisi binafsi.</p>	<p>Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. .</p> <p>6. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yameandaliwa ili kufikishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. .</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		kwa taasisi binafsi.	wanaomba vibali vya ujenzi wa ghorofa mfano wanaotoka katika taasisi binafsi pia wanapaswa pia kulipa ada ya kibali cha ujenzi wa ghorofa tofauti na kiwango cha shilingi 100,000/-.		

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
9.	<p>Sheria Ndogo za Ushuru wa Kituo cha Magari za Halmashauri ya Jiji la Mbeya, 2020</p> <p>GN NA. 833 2 Oktoba, 2020</p>	<p>Kipengele cha 9 cha Jedwali la Kwanza kiliweka sharti la malipo ya shilingi 1500/- kwa bajaji kila inapotoka katika eneo la stendi. Malipo haya hayana uhalisia kwa kuwa yamewekwa sawa na masharti ya kipengele cha 3 ya kiwango cha basi linalopakia abiria chini ya 20 ambalo kimsingi lina makusanyo makubwa tofauti na yanayokusanywa na bajaji kwa tripu moja inapotoka stendi.</p>	<p>Ilipendekezwa kuwa, Ofisi ya Rais – TAMISEMI iwasilishe mbele ya Kamati majibu ya taarifa ya ufafanuzi waliyoiomba kutoka Halmashauri ya Jiji la Mbeya kuhusu kufanana kwa viwango vya ushuru wa shilingi 1500/- kwa bajaj na basi inayopaki abiria chini ya ishirini (20) inapotoka eneo la stendi.</p>	<p>Rasimu ya Marekebisho ya Kipengele cha 9 cha Jedwali la Kwanza imeandaliwa kwa lengo la kurekebisha sharti la malipo ya shilingi 1500 ili kutofautisha viwango vya ushuru kati ya bajaj na basi linalopakia abiria chini ya 20.</p> <p>Maelezo</p> <p>Marekebisho hayo yamepunguza sharti la malipo ya ushuru wa shilingi 1500 hadi 500 kwa bajaj.</p>	<p>Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yameandaliwa ili kufikishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. .</p>
10.	<p>Sheria Ndogo za Hifadhi za Mazingira za Halmashauri ya Jiji la Mbeya, 2020</p> <p>GN NA. 836</p>	<p>1. Kifungu cha 6(4) kiliipa halmashauri mamlaka ya kupiga mnada mifugo iliyokamatwa iwapo mmiliki wake hajatokea kwa kipindi cha saa</p>	<p>1. Ilipendekezwa marekebisho yafanyike katika Kifungu cha 6(4) ili kuongeza sharti la kurejesha kwa mmiliki wa mifugo, kiasi cha fedha</p>	<p>1. Rasimu ya marekebisho ya Kifungu cha 6(4) imeandaliwa kwa kuongeza maneno</p> <p>“fedha zitakazobaki baada ya makato ya faini na gharama</p>	<p>1. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yameandaliwa ili kufikishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
	2 Oktoba, 2020	<p>ishirini na nne tangu mifugo yake ikamatwe.</p> <p>Hata hivyo Kifungu hakikuweka sharti kwa halmashauri, kurejesha fedha zitakazozidi baada ya kukata faini inayotakiwa na gharama nyingine iwapo mmiliki atapatikana mara baada mnada kuwa kufanyika.</p> <p>2. Kifungu cha 6(4) kiliweka sharti la kupiga mnada mifugo iliyokamatwa iwapo mmiliki hataonekana ndani ya msaa ishirini na nne. Hii inaweza kusababisha baadhi ya wamiliki wa mifugo ambao</p>	<p>zinazobaki baada ya makato ya faini na gharama nyingine.</p> <p>2. Kamati ilipendekeza Kifungu cha 6(4) kifanyiwe marekebisho ili kuongeza muda wa uuzwaji wa mifugo ili kutoa muda wa kutosha kwa mmiliki wa mifugo kupatikana</p>	<p><i>nyingine zitarejeshwa kwa mmiliki wa mifugo</i></p> <p>2. Rasimu ya marekbisho ya Kifungu cha 6(4) imeandaliwa kwa kufuta muda wa saa ishirini na nne na badala yake kuweka saa arobaini na nane.</p>	<p>kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p> <p>2. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yameandaliwa ili kufikishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>hawajapata mapema taarifa za kukamatwa mifugo, kupoteza mifugo yao kutokana na ufinyu wa muda wa tangu kukamatwa kwa mifugo na kupigwa mnada.</p> <p>3. Kifungu cha 17 kiliweka katazo la kukata mti au miti kwa matumizi yoyote ndani ya eneo la halmashauri pasipo na idhini ya halmashauri. Sharti halioneshi iwapo linahusu pia watu wenye mashamba binafsi ya miti au waliopanda miti katika makazi yao, iwapo pia wanahitaji kibali cha halmashauri ili</p>	<p>3. Ilipendekezwa marekebisho yafanyike katika Kifungu cha 17 ili kuainisha kwa ufasaha aina ya watu wanaotakiwa kupata idhini ya kukata miti ili kuondoa mkanganyiko unaoweza kujitokeza.</p>	<p>3. Rasimu ya marekebisho ya Kifungu cha 17 imeandaliwa kwa kuonesha kibali cha kukata miti ni kwa miti ya asili, inayomilikiwa na Halmashauri au iliyopandwa kwa maelekezo ya Halmashauri.</p>	<p>Gazeti la Serikali.</p> <p>3. Mapendekezo Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yameandaliwa ili kufikishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		kukata au kuvuna miti.			
11	<p>Sheria Ndogo za Afya na Usafi wa Mazingira za Halmashauri ya Jiji la Mbeya, 2020</p> <p>GN NA. 837 2 Oktoba, 2020</p>	<p>1. Kifungu cha 32 na Kifungu cha 37 kwa pamoja vilikuwa na maudhui yanayofanana kuhusu marufuku ya kutupa taka katika maeneo ambayo hayajatengwa kwa ajili ya kutupa takataka.</p> <p>2. Kifungu cha 15 kiliweka wajibu kwa wauza chakula kutunza chakula katika sanduku la mbao lneye kioo pasipo kuonesha masanduku ya vyakula yanayotengenezwa kwa <i>aluminium</i></p>	<p>1. Kamati ilipendekeza Sheria Ndogo ifanyiwe marekebisho ili kufuta cha 37 kuondoa kujirudia kwa maudhui.</p> <p>2. Ilipendekezwa marekebisho yafanyike katika Kifungu cha 15 kwa kufuta neno la mbao ili kuruhusu aina nyingine za masanduku ya kuhifadha chakula.</p>	<p>1. Rasimu ya Marekebisho imeandaliwa ili kufuta kifungu cha 37.</p> <p>2. Rasimu ya marekebisho ya Kifungu cha 15 imeandaliwa ili kufuta maneno "la mbao"</p>	<p>1. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yameandaliwa ili kufikishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. .</p> <p>2. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yameandaliwa ili kufikishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. .</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
12.	Sheria Ndogo za Usimamizi wa Masoko za Halmashauri ya Jiji la Mbeya, 2020 GN NA. 838 2 Oktoba, 2020	Kifungu cha 3 cha Sheria Ndogo kilitafsiri neno Mkurugenzi pasipo kuonesha maneno pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza kazi za Mkurugenzi chini ya Sheria Ndogo hizi.	Kamati ilipendekeza Kifungu cha 3 kifanyiwe marekebisho ili kuongeza maneno pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza kazi za Mkurugenzi chini ya Sheria Ndogo hizi	Rasimu ya marekebisho ya Kifungu cha 2 imeandaliwa ili kuongeza maneno "Pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi chini ya Sheria Ndogo hizi" katika tafsiri ya neno Mkurugenzi.	Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yameandaliwa ili kufikishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.
13.	Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, 2020 GN NA. 839 2 Oktoba, 2020	1. Sehemu C kipengele cha 12 cha Jedwali la Kwanza iliweka ushuru wa miwa kuwa ni shilingi 3,000/- na sehemu D kipengele cha 11 kinaweka sharti la malipo ya 3% kwa miwa. Jedwali halikufafanua:- i) Ujazo wa miwa unaokusudiwa	1. Ilipendekeza Sehemu C kipengele cha 12 cha Jedwali la Kwanza ifanyiwe marekebisho ili kuainisha bayana malipo sahihi yanayokusudiwa kutozwa kwa kuzingatia ujazo au tozo kwa kuonesha wazi iwapo tozo zote zinatozwa kwa pamoja.	1. Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeripoti kwamba, Rasimu ya marekebisho ya Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama imeandaliwa ili kuainisha kuanisha malipo sahihi yanayokusudiwa kutozwa katika miwa kama inavyoonekana kwenye kiambatisho Na. 10.	1. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yameandaliwa ili kufikishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>kwa tozo zilizowekwa;</p> <p>ii) Iwapo tozo zote mbili zinatozwa kwa pamoja chanzo kimoja.</p> <p>2. Sehemu ya F ya Jedwali la Kwanza kipengele cha 7 iliweka sharti la malipo ya ada ya kuonesha Sinema au video kuwa ni shilingi 30,000/-.</p> <p>Aidha Sharti la utozaji wa ada hiyo pia limewekwa katika Kanuni za Filamu na Michezo ya Kuigiza, 2020 ambazo katika Jedwali Tatu sehemu ya tano limeweka tozo ya kibali cha</p>	<p>2. Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo zikae kwa pamoja ili kuhuisha viwango vya ada za kuonesha sinema vinavyotozwa na Wizara hizo kwa pamoja, ili kuondoa wa ugumu wa utekelezaji wa shughuli hizi katika jamii ya watu wenye kipato cha chini, jambo ambalo linaongeza kero kwa</p>	<p>2. Pendekezo halijatekelezwa kwa kuwa OR – TAMISEMI na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo hawajakaa tofauti na ilivyopendekezwa.</p> <p>Maelezo</p> <p>Ofisi ya Rais-TAMISEMI inatoa maelezo kuwa hakuna muingiliano katika utozaji wa wa ada kwa kuwa Bodi ya Filamu inatoza katika vibali na ukaguzi wa filamu na Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama inatoza</p>	<p>2. Ofisi ya Rais – TAMISEMI izingatie Kikao kazi cha Ofisi Rais TAMISEMI,Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, BASATA na Bodi ya Filamu kifanyike mapema ili kupitia Kanuni zinazohusu utozwaji wa tozo katika sekta ya sanaa na burudani. Kwa lengo la kuhuisha Kanuni ili kuondoa maeneno yenye mgongano.</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>kuendesha shughuli za kuonesha filamu kuanzia shilingi 50,000/- hadi 500,000/- kwa mwaka. Hali hii inasababisha waendesha shughuli hizi kuwa na mzigo mkubwa wa malipo ili kuendesha shughuli hizo.</p> <p>3. Kipengele cha 18 cha Jedwali la Kwanza kiliweka sharti la malipo ya ada ya shilingi 5,000/- kwa tukio kwa mtu atakayepiga picha.</p> <p>Sharti hilo, linatoa mkanganyiko kuhusu tukio linalokusudiwa. Mfano, jambo linalojiri na kuvutia kupiga picha au</p>	<p>wananchi kinyume na matarajio ya kuboresha ustawi wao.</p> <p>3. Ilipendekezwa marekebisho yafanyike katika Kipengele cha 18 cha Jedwali la Kwanza kwa kubainisha bayana wapiga picha wanaokusudiwa na Sheria Ndogo hizi ili kuondoa uwezekano wa wapiga picha ambao hawafanyi shughuli katika sherehe au hafla</p>	<p>vibali vya kuonesha filamu.</p> <p>3. Rasimu ya Marekebisho ya Kipengele cha 18 cha Jedwali la Kwanza imeandaliwa ili kuonesha wapiga picha wanaokusudiwa ni wale wanaopiga picha za kibiashara na kwenye sherehe.</p>	<p>3. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yameandaliwa ili kufikishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. .</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		upigaji wenyewe wa picha, n.k. Kwa vyovyote, iwavyo, sharti hilo bado linaonekana kutokuwa na uhalisia kiutekelezaji.	mbalimbali kuwa sehemu ya kulipa ada ya shilingi 5,000/-.		
14.	Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru) na Halmashauri ya Jiji la Mbeya, 2020 GN NA. 909 16 Oktoba 2020	1. Sehemu ya 13 ya Jedwali la Kwanza kipengele cha 1 na 2 viliweka ada ya uimbaji kwenye matamasha kuwa ni shilingi 100,000/- na ada ya uimbaji katika makongamano ni shilingi 80,000/- kwa kila kongamano. Viwango vya ada vilivyowekwa havijazingatia hadhi ya msanii na au malipo anayolipwa msanii mmoja hadi mwingine (wasanii	1. Ilipendekezwa kwamba Ofisi ya Rais – TAMISEMI iwasilishe mbele ya Kamati majibu ya taarifa ya ufafanuzi waliyoionba kutoka Halmashauri ya Jiji la Mbeya kuhusu ada ya shilingi 100,000/- uimbaji katika matamasha na ada ya shilingi 80,000/- kuimba katika kila kongamano. Ufafanuzi ulenge kuonesha uzingatiaji wa hadhi ya msanii	1. Rasimu ya Marekebisho ya Sehemu ya 13 ya Jedwali la Kwanza kipengele 1 na 2 imeandaliwa ili kuonesha wasanii wanokusudiwa kulipa ada iliyotajwa ni wasanii wakubwa wenye hadhi ya kitaifa.	1. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatia ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yameandaliwa ili kufikishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>wadogo).</p> <p>2. Sehemu ya 13 kipengele cha 6 na 7 vya Jedwali la kwanza viliweka masharti ya malipo ya shilingi 70,000/- kusajili vibanda vya filamu na malipo ya shilingi 100,000/- kwa ajili ya kibali cha kuonesha sinema na michezo ya kuigiza.</p> <p>Aidha, sharti la utozaji wa ada hiyo pia imewekwa katika Kanuni za Filamu na Michezo ya Kuigiza, 2020 ambazo katika Jedwali Tatu sehemu ya tano limeweka tozo ya kibali cha</p>	<p>(mkubwa na mdogo) anayetumbuiza kwa kulinganisha na ada husika.</p> <p>2. Ilipendekezwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo zikae kwa pamoja ili kuhuisha viwango vya ada za kumbi kuonesha sinema vinavyotowza na Wizara hizo kwa pamoja, ili kuondoa wa ugumu wa utekelezaji wa shughuli hizi katika jamii ya watu wenye kipato cha chini, jambo ambalo linaongeza kero kwa wananchi kinyume na matarajio ya kuboresha ustawi</p>	<p>2. Ofisi ya Rais - TAMISEMI inalichukua suala hili kwa ajili ya kulifanyia kazi zaidi na Bodi ya Filamu ili kuondoa mkanganyiko unao onekana kujitokeza baada ya kutungwa kwa Kanuni za Filamu na Michezo ya Kuigiza za Mwaka 2020.</p> <p>Maelezo</p> <p>Imechukua takriban miezi sita tangu Bunge kupitisha mapendekezo tarehe 28 Juni, 2021 hadi tarehe 4 Januari, 2022, Ofisi ya Rais – TAMISEMI ikiwa inalifanyia kazi suala hili.</p>	<p>2. Adha kwa waendesha shughuli za kuonesha filamu inaendelea kuwa kero kwa wananchi kutokana na kasi ndogo ya kutekeleza mapendekezo.</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>kuendesha shughuli za kuonesha filamu kuanzia shilingi 50,000/- hadi 500,000/- kwa mwaka na sehemu ya kumi ya Jedwali la Kwanza imeweka tozo ya kibali cha kuendesha michezo ya kuigiza kuanzia shilingi 36,000/- hadi 500,000/-.</p> <p>Hali hii inasababisha waendesha shughuli hizi kuwa na mzigo mkubwa wa malipo ili kuendesha shughuli hizo.</p>	<p>wao.</p> <p>3. Ilipendekezwa marekebisho yafanyike katika Sehemu ya 13 Kipengele cha 18 cha Jedwali la</p>	<p>3. Rasimu ya marekebisho ya Sehemu ya 13 Kipengele cha 18 cha Jedwali la Kwanza imeandaliwa ili kuonesha wapishi wanaokusudiwa</p>	<p>3. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yameandaliwa ili kufikishwa katika Ofisi ya</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>moja kwa siku kwa wapishi wa vyakula.</p> <p>Sheria haijabainisha aina ya wapishi wanokusudiwa kulipa ada hii iwapo ni wale wa vikundi au mpishi mmoja mmoja.</p> <p>4. Sehemu ya 13 Kipengele cha 19 katika Jedwali la Kwanza, kiliweka sharti la malipo ya ada ya shilingi 30,000/- kwa tukio kwa mtu atakayepiga picha jongevu na mnato.</p> <p>Sharti hilo, lilionesha mkanganyiko kuhusu tukio linalokusudiwa. Mfano, jambo linalojiri na kuvutia kupiga picha au</p>	<p>Kwanza ili kubainisha bayana wapishi wa aina gani wanaokusudiwa na Sheria Ndogo hizi ili kuondoa uwezekano wa kutoza makundi yasiyohusika.</p> <p>4. Ilipendekezwa Sehemu ya 13 Kipengele cha 19 katika Jedwali la Kwanza ifanyiwe marekebisho ili kubainisha wapiga picha wanaokusudiwa na Sheria Ndogo hizi ili kuondoa uwezekano wa wapiga picha ambao hawafanyi shughuli katika sherehe au hafla mbalimbali kuwa</p>	<p>kulipa ada ni wale wanaofanya shughuli katika sherehe na matukio ya kibiashara.</p> <p>4. Rasimu ya marekebisho ya Sehemu ya 13 Kipengele cha 19 katika Jedwali la Kwanza imeandaliwa ili kuonesha wapiga picha wanaokusudiwa ni wale wanaopiga picha kwenye sherehe na matukio ya kibiashara.</p>	<p>Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali .</p> <p>4. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yameandaliwa ili kufikishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali..</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>upigaji wenyewe wa picha, n.k. Kwa vyovyote, iwavyo, sharti hilo bado linaonekana kutokuwa na uhalisia kiutekelezaji.</p> <p>5. Sehemu ya 16 kipengele cha 8 cha Jedwali la kwanza kiliweka ada ya shilingi 100,000/- kwa mambo mengine ya kiutamaduni pasipo kuainisha mambo hayo.</p> <p>Ilionekana kuwa uandishi wa namna hiyo unaweza ukalazimisha shughuli za utamaduni ambazo ni ndogo kulipa kiwango kikubwa</p>	<p>sehemu ya kulipa ada ya shilingi 30,000/-.</p> <p>5. Ilipendekezwa Sehemu ya 16 kipengele cha 8 cha Jedwali la kwanza ifanyiwe marekebisho kwa kuondoa ujumla wa shughuli za utamaduni na badala yake kuainisha bayana aina za shughuli za utamaduni zinazokudusiwa kutozwa ada ya shilingi 100,000/-.</p>	<p>5. Rasimu ya marekebisho imeandaliwa kwa kufuta kipengele cha 9 katika Sehemu ya 16.</p>	<p>5. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yameandaliwa ili kufikishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. .</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>cha ada.</p> <p>6. Sehemu ya 16 kipengele cha 9 cha Jedwali la Kwanza kiliweka ada ya shilingi 100,000/- kwa maombi ya kibali cha tangazo la harusi. Pasipo kufafanua ni kibali cha namna gani kinachokusudiwa.</p>	<p>6. Ilipendekezwa kwamba Ofisi ya Rais – TAMISEMI iwasilishe mbele ya Kamati majibu ya taarifa ya ufafanuzi waliyoionba kutoka Halmashauri ya Jiji la Mbeya kuhusu kibali cha cha harusi kinachokusudiwa kulipiwa ada ya shilingi 100,000/-.</p>	<p>6. Rasimu ya mapendekezo ya Sehemu ya 16 kipengele cha 9 cha Jedwali la Kwanza imeandaliwa kwa kufuta kipegele cha 9.</p>	<p>6. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yameandaliwa ili kufikishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali..</p>
15.	<p>Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto, 2020</p> <p>GN NA. 1024 11 Disemba, 2020</p>	<p>1. Sehemu ya Nne ya Jedwali la Kwanza imeweka sharti la malipo ya shilingi 15,000/- kwa kibali cha kufanya shughuli za sinema . Sharti hilo pia lipo katika Kanuni za Filamu na Michezo ya Kuigiza, 2020 ambapo Jedwali Tatu</p>	<p>1. Ilipendekezwa kwamba Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo zikae kwa pamoja ili kuhuisha viwango vya ada za kumbi kuonesha sinema vinavyotowza na Wizara hizo kwa</p>	<p>1. Pendekezo halijatekelezwa kwa kuwa OR – TAMISEMI na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo hawajakaa tofauti na ilivyopendekezwa.</p> <p>Maelezo Ofisi ya Rais-TAMISEMI inatoa maelezo kuwa</p>	<p>1. Ofisi Kikao kazi cha Ofisi Rais TAMISEMI, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, BASATA na Bodi ya Filamu kifanyike mapema ili kupitia Kanuni zinazohusu utozwaji wa tozo katika sekta ya sanaa na burudani. Kwa lengo la kuhuisha Kanuni ili kuondoa maeneno yenye</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>sehemu ya tano limeweka tozo ya kibali cha kuendesha shughuli za kuonesha filamu kuanzia shilingi 50,000/- hadi 500,000/-.</p> <p>2. Sehemu ya 4 kipengele cha 8 cha Jedwali la Kwanza kinaweka Ada za shughuli za jando na unyago kuwa ni shilingi 20,000/- kwa tukio. Kimsingi shughuli zinazowekewa ada ni za kijamii zenye lengo la kutoa mafunzo ya maisha kwa vijana na</p>	<p>pamoja, ili kuondoa wa ugumu wa utekelezaji wa shughuli hizi katika jamii ya watu wenye kipato cha chini, jambo ambalo linaongeza kero kwa wananchi kinyume na matarajio ya kuboresha ustawi wao.</p> <p>2. Ilipendekezwa Sehemu ya 4 kipengele cha 8 cha Jedwali la Kwanza ifanyiwe marekebisho kwa kufuta ada za jando na unyago kwa kuwa hazina lengo la uingizaji wa kipato badala yake zina lengo la kutoa mafunzo mbalimbali</p>	<p>hakuna muingiliano katika utozaji wa wa ada kwa kuwa Bodi ya Filamu inatoza katika vibali na ukaguzi wa filamu na Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto inatoza vibali vya kuonesha filamu.</p> <p>2. Rasimu ya Marekebisho ya Sehemu ya 4 kipengele cha 8 cha Jedwali la Kwanza imeandaliwa ili kufuta ada za shughuli za jando na unyago.</p>	<p>mgongano.</p> <p>2. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yameandaliwa ili kufikishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		ambazo hazina uhusiano wa moja kwa moja wa uingizaji kipato.	ya kimaisha na kijamii kwa vijana.		
16.	Sheria Ndogo za Kilimo na Hifadhi ya Chakula za Halmashauri ya Wilaya ya Itilima, 2020 GN NA. 1006 20 Novemba, 2020	Kifungu cha 16(d) kiliweka sharti la kulazimisha mfugaji kujiunga na vyama vya ufugaji. Masharti haya ni kinyume na Ibara ya 20 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 inayoweka sharti kuwa ni hiari kujiunga na vyama au mashirika.	Ilipendekezwa marekebisho yafanyike katika Kifungu cha 16(d) ili kuondoa takwa la lazima kwa wafugaji kujiunga na vyama wafugaji badala yake kuweka takwa la uhamasishaji wa kujiunga na vyama vya wafugaji kwa lengo la kuondoa ukinzani wa sheria ndogo na Ibara ya 20 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977.	Rasimu ya marekebisho ya Kifungu cha 16(d) imeandaliwa ili kufuta sharti la ulazima wa kujiunga na vyama vya ufugaji na badala yake kuweka maneno “kila mfugaji atahamasishwa kujiunga na vyama vya ufugaji”	Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yameandaliwa ili kufikishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.
17.	Sheria Ndogo ya Uanzishaji wa Vikundi vya Watumiaji wa Maji za Halmashauri ya	Kifungu cha 3 cha Sheria Ndogo kimetafsiri neno Mkurugenzi pasipo kuonesha maneno pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa	Ilipendekezwa marekebisho yafanyike katika Kifungu cha 3 kwa kuongeza maneno pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa	Rasimu ya marekebisho ya Kifungu cha 3 imeandaliwa ili kwa kuongeza maneno “Pamoja na Afisa yeyote	Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yameandaliwa ili kufikishwa katika Ofisi ya

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
	Wilaya ya Mkalama, 2020 GN NA. 1029 11 Disemba, 2020	kutekeleza kazi za Mkurugenzi chini ya Sheria Ndogo hizi.	kutekeleza kazi za Mkurugenzi chini ya Sheria Ndogo hizi	atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi chini ya Sheria Ndogo hizi katika tafsiri ya ya neno Mkurugenzi.	Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.
WIZARA YA MADINI					
18.	The Mining (Mineral Rights Application by Tender) Regulations 2020 GN NA. 484 26 Juni 2020	1. Kanuni ya 5(2) ya Kanuni hizi inafanya rejea ya Jedwali la Kwanza badala ya kufanya rejea sahihi ya Jedwali la Pili inayohusu Fomu NO.TBF.2. 2. Jedwali la Pili la Kanuni hizi linafanya rejea ya Kanuni ya 4 badala ya kufanya rejea sahihi ya	1. Ilipendekezwa kwamba Kanuni ya 5(2) ifanyiwe marekebisho kwa kufuta maneno “Jedwali la kwanza” na badala yake kuandika maneno “Jewali la Pili” . 2. Ilipendekezwa marekebisho yafanyike katika Jedwali la Pili kwa kufuta “Kanuni ya 4”	1. Rasimu ya marekebisho ya Kanuni 5(2) imeandaliwa ili kufuta maneno “Jedwali la kwanza” na badala yake kuandika maneno “Jewali la Pili” . 2. Rasimu ya marekebisho ya Jedwali la Pili imeandaliwa ili kufuta rejea ya Kanuni ya 4 na	1. Mashauriano na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali yameshafanyika na kukubaliana ili kuondoa makosa ya kiuchapaji kwa njia ya kufanya marekebisho ya makosa ya kiuchapaji (Rectification of Printing Errors). Marekebisho hayo yatatangazwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 11 Februari, 2022. 2. Mashauriano na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali yameshafanyika na kukubaliana ili kuondoa

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		Kanuni ya 5 (2) inayoanzisha Jedwali la Pili.	na badala yake kurejea Kanuni ya 5 (2)	badala yake kuandika rejea ya Kanuni ya 5.	makosa ya kiuchapaji kwa njia ya kufanya marekebisho ya makosa ya kiuchapaji (Rectification of Printing Errors). Marekebisho hayo yatatangazwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 11 Februari, 2022.
WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO					
19.	Kanuni za Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza, 2020 GN NA. 488 26 Juni 2020	1. Kanuni ya 5 inaweka sharti kwa Serikali, Wakala au Taasisi yoyote ya Serikali kuomba kibali iwapo wanakusudia kutayarisha filamu au shughuli nyingine yoyote iliyo chini ya Kanuni za Filamu na Michezo ya Kuigiza. Masharti ya Kanuni ya 5 yanakinzana na	1. Ilipendekezwa kuwa Kanuni ya 5(1) ifanyiwe marekebisho ili kuondoa sharti kwa Taasisi ya serikali kuomba kibali wanapokusudia kutayarisha filamu au shughuli nyingine yeyote chini ya Kanuni za Filamu na Michezo ya Kuigiza.	1. Rasimu ya marekebisho ya Kanuni ya 5(1) imeandaliwa ili kuondoa masharti ya Serikali, Wakala au Taasisi yoyote ya Serikali kuomba kibali cha Bodi inapokusudia kutayarisha filamu.	1. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho imeandaliwa ili iwasilishwe katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>Kifungu cha 15 (1) (a) cha Sheria Mama kinachoondoa ulazima wa kibali kwa shughuli za filamu zinazofanywa na Serikali au Taasisi zilizo chini yake.</p> <p>2. Kanuni ya 16 imeainisha maudhui mabaya ambayo yanaweza kusababisha kutokutolewa kwa kibali cha kutayarisha, kusambaza, kuonesha filamu au michezo wa kuigiza.</p> <p>Baadhi ya masharti yaliyowekwa hayana uhalisia kwa kuwa, filamu hutayarishwa katika maonesho (<i>scenes</i>) yenye</p>	<p>2. Ilipendekezwa Kanuni ya 16 ifanyiwe marekebisho kwa kuandikwa vizuri ili isioneshe kama inakataza kuonesha aina fulani ya matukio katika filamu.</p>	<p>2. Rasimu ya marekebisho ya Kanuni ya 16 imeandaliwa kwa kufuta neno “yanahusisha” ambalo lilikuwa linaleta utata, na badala yake limewekwa neno “yanahamasisha”, kwa lengo la kuondoa dhana kwamba waandaaji wa filamu au michezo ya kuigiza wamezuiwa kuigiza vitendo vibaya vinavyotendeka katika jamii.</p>	<p>2. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho imeandaliwa ili iwasilishwe katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>matukio mbalimbali kama vile wizi, uchawi, unyanyasaji, utumiaji wa dawa za kulevya, ulevi n.k. ambayo muunganiko wake huweza kutoa mafunzo yaliyokusudiwa na filamu inayohusika.</p> <p>Hivyo, kuzuia maudhui kama hayo kunaweza kusababisha dhima na dhamira ya filamu katika jamii isifanikiwe.</p> <p>3. Kanuni ya 23 inaweka sharti kwa mtu yeyote, chama, shirikisho au asasi inayotaka kufanya shughuli ya usambazaji wa filamu kwa njia ya</p>	<p>3. Ilipendekezwa marekebisho yafanyike katika Kanuni ya 23 kwa kuweka tafsiri ya maneno “mitandao ya kijamii” na aina ya usambazaji</p>	<p>3. Rasimu ya marekebisho imeandaliwa kwa kuweka tafsiri ya maneno “mitandao ya kijamii” kama yalivyotafsiriwa katika Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki za</p>	<p>3. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho imeandaliwa ili iwasilishwe katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>mitandao ya kijamii, kuwa atapaswa kujisajili na kupata kibali chini ya Kanuni hizi. Hata hivyo, Kanuni haijaweka maana ya maneno "Mitandao ya Kijamii"</p> <p>4. Kanuni ya 30 (2) inatoa fursa kwa mtu yeyote, chama, shirikisho au asasi yoyote inayojihusisha na shughuli yoyote ya filamu, na mwakilishi au mrithi yeyote wa mtu, chama, shirikisho au asasi yoyote inayojihusisha na shughuli yoyote, kuwasilisha malalamiko yake katika Bodi ya filamu iwapo atanyimwa au</p>	<p>unaokusudiwa.</p> <p>4. Kamati ilipendekeza marekebisho katika Kanuni ya 30(2) ili kuondoa uwezo wa Bodi kushughulikia malalamiko yanayotokana na ucheleweshwaji wa vyombo vingine ambavyo havipo chini ya Bodi.</p>	<p>Maudhui ya Mitandaoni (Tangazo la Serikali Na. 538/2020).</p> <p>4. Rasimu ya marekebisho ya kifungu cha 30(2) imeandaliwa ili kuwaruhusu wadau kuwasilisha malalamiko yao kwenye kamati maalum ya kushughulikia malalamiko ya wadau na haki za wasanii iliyoainishwa Katika Kanuni ya 32.</p> <p>Maelezo</p> <p>Hatua iliyofikiwa haitatui tatizo la Bodi kushughulikia malalamiko yanayotokana na</p>	<p>kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p> <p>4. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho imeandaliwa ili iwasilishwe katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>kucheleweshewa huduma au haki kutoka kwa mtu, chama, shirikisho, asasi binafsi, taasisi ya umma, wakala wa Serikali au mdau mwingine yeyote wa tasnia ya filamu.</p> <p>Kanuni zinapanua wigo wa kushughulika na mashauri ya malalamiko yanayotoka katika vyombo, watu au taasisi ambazo kimsingi hazipo chini ya mamlaka ya Bodi ya Filamu.</p> <p>5. Kanuni ya 34 (1) inaeleza kuhusu fursa ya kukata rufaa kwa Waziri mwenye dhamana dhidi ya uamuzi wa Bodi ya</p>	<p>5. Ilipendekezwa Kanuni ya 34(1) ifanyiwe marekebisho ili kuonesha nyaraka inayopaswa</p>	<p>ucheleweshwaji wa huduma au haki vyombo vingine ambavyo havipo chini ya Bodi.</p> <p>5. Rasimu ya marekebisho ya Kanuni ya 34(1) imeandaliwa kwa kuongeza kanuni mpya ya (2) inayotoa utaratibu wa kuwasilisha rufaa kwa Waziri kwa njia tatu:</p>	<p>5. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho imeandaliwa ili iwasilishwe katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>Filamu, pasipo kuonesha utaratibu unaotumika kuandaa rufaa husika.</p> <p>6. Kanuni hazijaweka utaratibu wa kuomba vibali kwa njia ya mtandao (<i>electronic application</i>). Kukosekana kwa utaratibu huu kutaongeza gharama na kusababisha usumbufu kwa waombaji ambao watalazimika kufika katika ofisi za Bodi.</p>	<p>kutumika katika kuwasilisha rufaa kwa Waziri mwenye dhamana ili kuwa na utaratibu unaofanana.</p> <p>6. Ilipendekezwa kwamba Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuweka utaratibu wa uombaji na utoaji wa vibali kwa njia ya mtandao (<i>electronic application</i>).</p>	<p>yaani barua ya kawaida kupitia posta au barua pepe au njia nyingine yoyote itakayomwezesha Waziri kupokea hati inayoainisha hoja zote zinazokatiwa rufaa pamoja na vielelezo muhimu kwa ajili hiyo.</p> <p>6. Rasimu ya marekebisho imeandaliwa kwa kuongeza kanuni ndogo ya (4) kanuni ya 8 ili kuweka utaratibu wa uombaji na utoaji wa vibali kwa njia ya mtandao (<i>electronic application</i>).</p> <p>Maelezo</p> <p>Hatua inayoripotiwa inaonekana kuweza kutatua tatizo la kutooneshwa kwa utaratibu wa uombaji vibali kwa njia ya</p>	<p>kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p> <p>6. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho imeandaliwa ili iwasilishwe katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>7. Kipengele cha 14 cha Jedwali la Kwanza kinaorodhesha utafiti wa mambo ya filamu katika mambo yanayopaswa kuombewa kibali cha Bodi ya Filamu.</p> <p>Kwa kawaida, katika maendeleo ya taaluma, upo utaratibu wa kuandika tasnifu baada ya utafiti wa kitaaluma ambao unaweza kuwa ni utafiti kuhusu filamu katika fani za sanaa au nyinginezo.</p>	<p>7. Ilipendekezwa marekebisho yafanyike katika Kipengele cha 14 cha Jedwali la Kwanza ili kubainisha utafiti unaokusudiwa kuombewa kibali cha bodi ya filamu ili kuondoa uwezekano wa mkanganyiko unaoweza kujitokeza katika utafiti unaokusudiwa.</p>	<p>kielektroniki. Hata hivyo, kanuni ndogo ya (4) mpya inayotajwa haibainishi kuongezwa katika Kanuni ipi.</p> <p>7. Rasimu ya marekebisho ya Kipengele cha 14 katika Jedwali la Kwanza imeandaliwa ili kuongeza maneno <i>“isipokuwa tafiti zinazohusiana na masuala ya kitaaluma.</i></p>	<p>7. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho imeandaliwa ili iwasilishwe katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>Pamoja na masharti hayo yaliyobainishwa na Kanuni hizo, hakuna ufafanuzi unaoonesha kama tafiti za kitaaluma hazibanwi na masharti ya Kanuni hizi.</p> <p>8. Kipengele cha 3 cha Jedwali la Tatu kinaweka ada ya kuhakiki tangazo la filamu au mchezo wa kuigiza, pasipo kuzingatia kuwa kipande cha sinema kinachotangazwa (<i>trailer</i>) kinakuwa tayari kimeshalipiwa ada ya uhakiki iliyotozwa katika filamu nzima.</p>	<p>8. Ilipendekezwa Kipengele cha 3 cha Jedwali la Tatu kifanyiwe marekebisho kwa kuondoa sharti malipo ya ada ya kuhakiki tangazo la filamu (<i>trailer</i>) au mchezo wa kuigiza ili kuepusha waigizaji kulipa gharama mara mbili.</p>	<p>8. Rasimu ya marekebisho ya Kipengele cha 3 cha Jedwali la Tatu imeandaliwa ili kufuta tozo zote za uhakiki wa matangazo ya filamu ambayo huandaliwa kuhamasisha wadau kununua au kuhudhuria maonesho.</p>	<p>8. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho imeandaliwa ili iwasilishwe katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII					
20.	The Tanzania Wildlife Research Institute (Conduct of Wildlife Research) Regulations, 2020 GN NA. 628 14 Agosti, 2020	Kanuni ya 13 ya Kanuni hizi inahusu ada ya utafiti kuhusu Masuala ya Wanyamapori. Katika ufafanuzi wa Ada, Kanuni ya 13 (1) imebainisha ada moja kwa moja katika kanuni hiyo, lakini Kanuni ya 13 (2) imefafanua ada kwa kutumia jedwali la tatu. Uandishi huo ambapo baadhi ya ada zinatajwa moja kwa moja kwenye kanuni na nyingine kutajwa kwenye Jedwali haulingani na desturi ya uandishi wa sheria uliozoeleka nchini.	Ilipendekezwa Kanuni ya 13 ifanyiwe marekebisho kwa kuelekeza ada zote zinazotajwa na Kanuni hiyo katika Jedwali la Tatu ili: i) Kurahisisha rejea ya Jedwali ii) Kuendeanana na desturi ya uandishi wa sheria iliyozoeleka nchini	Rasimu ya marekebisho ya Kanuni ya 13 imeandaliwa kwa kufuta Kanuni ndogo (1) na badala yake ada hizo zinahamishwa katika sehemu H ya Jedwali la Tatu.	Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo imewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.
21.	The Wildlife Conservation (Administration and Management of	Kanuni ya 37 imejumuisha kwa pamoja mambo yanayoweza kupelekea ukiukwaji wa taratibu za	Ilipendekezwa marekebisho katika Kanuni ya 37 ili kutenganisha ukiukwaji wa taratibu za mitihani	Rasimu ya marekebisho ya Kanuni ya 37 imeandaliwa kwa kuifuta na kuiandika upya ili kutenganisha ukiukwajiwa taratibu za	Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo imewasilishwa katika

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
	<p>Pasiansi Wildlife Training Institute) Regulations, 2020</p> <p>GN NA. 946 6 Novemba, 2020</p>	<p>mitihani yanayosababishwa na mtumishi wa Taasisi na Mwanafunzi.</p> <p>Kanuni haijatanganiwa masuala ya ukiukwajiwa taratibu za mitihani yanayoweza kufanywa na mtumishi na yale yanayoweza kufanywa na mwanafunzi ili kuwa na mtiririko mzuri.</p>	<p>unaofanywa na mfanyakazi unaofanywa mwanafunzi.</p> <p>na ule na</p>	<p>mitihani yanayoweza kufanywa na mtumishi</p>	<p>Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p>
WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI					
22	<p>The Valuation and Valuers Registration (Training Examination) Rules 2020</p> <p>GN NA. 682 28 Agosti 2020</p>	<p>1. Kanuni ya 2 inatafsiri neno "<i>abscondment</i>" ambalo halijatumika kokote kwenye Kanuni.</p>	<p>1. Ilipendekezwa Kanuni 2 ifanyiwe marekebisho kufuta tafsiri ya neno <i>abscondment</i>.</p>	<p>1. Rasimu ya marekebisho ya Kanuni 2 imeandaliwa kwa kufuta neno "<i>abscondment</i>" ambalo halijatumika katika Kanuni.</p>	<p>1. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo imeandaliwa ili iwasilishwe katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>2. Madaraja ya mitihani yaliyopo katika kanuni ya 9 (i) (a) & (b) yanakinzana na madaraja yaliyowekwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi.</p> <p>3. Kanuni ya 9(3) inaweka sharti la mtahiniwa kuendelea na (<i>module</i>) daraja jingine la mtihani baada ya kukamilisha daraja moja. Kanuni haijaweka fursa ya kuendelea na daraja la mbele wakati anakamilisha mitihani ya marudiao ya ngazi ya chini.</p>	<p>2. Ilipendekezwa Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuhuisha maudhui ya Kanuni ya 9(i)(a) & (b) na Jedwali la Kwanza.</p> <p>3. Ilipendekezwa Kanuni ya 9(3) ifanyiwe marekebisho ili kuruhusu ufanyaji wa daraja zaidi ya moja na kuondoa kigezo cha kufaulu daraja moja ndio iwe kigezo cha kwenda daraja jingine, badala yake mtahiniwa aruhusiwe kuendelea akiwa anarudia mitihani ya daraja lililotangulia.</p>	<p>2. Rasimu ya Marekebisho ya Fomu husika Na.3 ya Jedwali la Kwanza imeandaliwa ili kuongeza daraja kutoka matatu hadi matano kama yalivyotajwa.</p> <p>3. Rasimu ya marekebisho ya Kanuni 9(3) imeandaliwa ili kuweka masharti yatayakayo mwezesha mtahiniwa kuendelea na ngazi ya juu wakati anakamilisha mitihani ya marudio ya ngazi ya chini.</p>	<p>2. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo imeandaliwa ili iwasilishwe katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p> <p>3. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo imeandaliwa ili iwasilishwe katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>4. Kanuni ya 9(5) imeipa bodi Mamlaka ya kuhusu muda ambao mtahiniwa atakamilisha mafunzo yake.</p> <p>5. Kanuni ya 16 aya (g) kuhusu kushindwa kumaliza mitihani kwa muda uliopangwa. Mitihani ya taaluma kama zilivyo taaluma nyingine hayana ukomo wa muda.</p> <p>6. Kanuni ya 19(2) haijabainisha muda mahsusi wa kutangaza matokeo</p>	<p>4. Ilipendekezwa Kanuni ya 9(5) ifanyiwe marekebisho ili kuweka ukomo wa miaka mitano (5) kwa mtahiniwa kukamilisha mafunzo ya taaluma ya uthamini.</p> <p>5. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuondoa masharti ya aya (g)</p> <p>6. Ilipendekezwa Kanuni 19 (2) ifanyiwe</p>	<p>4. Rasimu ya marekebisho ya Kanuni ya 9(5) imeandaliwa ili kuongeza muda wa kumaliza masomo kutoka miaka 2 hadi 5 katika Jedwali la Pili 5.0(b).</p> <p>5. Rasimu ya marekebisho ya Kanuni ya 16 (g) imeandaliwa ili kufuta ukomo wa muda katika ufanyaji wa mitihani.</p> <p>6. Rasimu ya marekebisho ya Kanuni ya 19(2) imeandaliwa kwa kuweka kipindi cha</p>	<p>4. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo imeandaliwa ili iwasilishwe katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p> <p>5. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo imeandaliwa ili iwasilishwe katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p> <p>6. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>ya mitihani mara baada ya kuwa imesahishwa.</p> <p>7. <i>Review Classes</i> chini ya Kanuni ya 24(4) imekaa kwa utaratibu wa kulazimisha uwepo wa muhusika (<i>physical presence</i>).</p> <p>8. Kanuni haijaonesha sharti la kushirikisha wadau kabla ya kuanza mafunzo kuhusu mitaala, mfumo wa ithbati na</p>	<p>marekebisho ili ioneshe muda mahsusi wa kutangaza matokeo ili kutoa fursa kwa watahiniwa kutumia matokeo hayo kwa ajili ya mipango yao mbalimbali</p> <p>7. Ilipendekezwa marekebisho yafanyike katika Kanuni ya 24(4) ili kuweka utaratibu wa kushiriki mafunzo kwa njia ya mtandao kuwezesha usomaji rahisi popote nchini.</p> <p>8. Ilipendekezwa marekebisho ili Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuweka sharti la kuitaka bodi</p>	<p>kutangaza matokeo kuwa si zaidi ya miezi sita tangu tarehe ya kufanya mtihani.</p> <p>7. Marekebisho yamefanyika kuruhusu njia mbalimbali za kisasa kutumika kuendesha mafunzo kadiri itakavyoonekana inafaa.</p> <p>8. Mapendekezo hayajatekelezwa kwa kuwa Taratibu za uendeshaji wa shughuli za Bodi Board's Code of</p>	<p>Ndogo imeandaliwa ili iwasilishwe katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p> <p>7. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo imeandaliwa ili iwasilishwe katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p> <p>8. Kutokutekelezwa kwa pendekezo hakuna athari katika utekelezaji wa kanuni.</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		mfumo wa mitihani.	kushirikisha wadau kabla hawajaanza mafunzo yao.	Conducts) zinaitaka Bodi kushirikisha Wadau katika kuandaa Kanuni zozote za Bodi kabla ya kuzitangaza (sehemu ya II <i>Purpose</i>).	
		9. Kanuni haijabainisha idadi na aina ya masomo kwa kila daraja.	9. Ilipendekezwa marekebisho Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuonesha masomo ya msingi kwa kila daraja.	9. Mapendekezo yamefanyika kwa kuainisha masomo ya msingi kwa kila daraja katika syllabus (VRB Training and Examination Curriculum).	9. Marekebisho yaliyofanyika yana tija katika Utekelezaji wa Kanuni.
		10. Kanuni haijaweke utaratibu wa namna ya kutambua watanzania wenye usajili mbadala (<i>equivalent external qualifications</i>) na watu wengine kutoka mataifa ambao wanaweza kuwa na majukumu hapa	10. Ilipendekezwa Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kutambua watu wenye sifa zinazofanana zinazotolewa na vyombo vya nje.	10. Mapendekezo hayajatekelezwa kwa kuwa, pendekezo hili linaendelea kujadiliwa katika mapendekezo ya marekebisho ya Sheria Sura 138 pamoja na Kanuni hizi ili kutoa fursa kwa Watanzania wenye utaalamu mbadala na wengine wenye usajili	10. Kutokutekelezwa kwa pendekezo hakuna athari katika utekelezaji wa Kanuni.

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>nchini.</p> <p>11. Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi limefanya rejea ya kuanzishwa chini ya Kanuni ya 3(2), wakati Kanuni yote ya 3 imebeba maudhui yote ya Jedwali la Kwanza.</p> <p>Uandishi huu unatoa picha finyu kuhusu jedwali linalorejewa ambalo lina maudhui pana zaidi inayojitokeza katika Kanuni ya 3</p> <p>12. Jedwali la Pili linaoneshwa kuwa limeanzishwa chini ya Kanuni ya 32(2) ambayo haipo. Kosa hilo la uandishi</p>	<p>11. Ilipendekezwa marekebisho yafanyike katika Jedwali la Kwanza kwa kufuta Kanuni ya 3(2) katika sehemu ya fomu ya maombi (Application Form (Form No.1)) na badala yake kufanya rejea ya Kanuni ya 3.</p> <p>12. Ilipendekezwa marekebisho yafanyike ya kufuta Kanuni ya 32(2) inayorejewa katika Jedwali la Pili na</p>	<p>wa mataifa mengine kusajiliwa na Bodi.</p> <p>11. Rasimu ya marekebisho ya Jedwali la Kwanza imeandaliwa kwa kufuta rejea ya Kanuni ya 3(2) na badala yake kuweka rejea ya Kanuni ya 3.</p> <p>12. Rasimu ya Marekebisho ya Jedwali la Pili imeandaliwa kuifuta Kanuni ya 32(2) kwa kuwa Kanuni hiyo haipo na badala yake Jedwali</p>	<p>11. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo imeandaliwa ili iwasilishwe katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p> <p>12. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo imeandaliwa ili iwasilishwe katika Ofisi ya</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		linaning'iniza Jedwali katika mtiririko wa uandishi. Aidha, Kanuni ya 34 (2) inarejea Jedwali la Pili ambalo haioneshi kuanzishwa chini ya Kanuni hii.	badala yake kuweka Kanuni ya 34 (2)	la pili litaonesha kuanzishwa chini ya Kanuni ya 34(2).	Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.
		13. Jedwali la Tatu la Kanuni hizi limefanya rejea ya Kanuni mbalimbali zinazolianshisha bila kujumuisha Kanuni ya 28 (3), 29 (4), na 30(4) sehemu ya Kanuni zilizobeba maudhui ya Jedwali hilo.	13. lilipendekezwa marekebisho yafanyike katika Jedwali la Tatu kwa kuongeza Kanuni ya 28(3), 29(4), na 30(4) zinazoanzisha Jedwali hilo.	13. Rasimu ya marekebisho ya Jedwali la Tatu yameandaliwa li kujumuisha Kanuni ya 28(3), 29(4) na 30(4) kuwa pia zinaanzisha Jedwali hili.	13. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo imeandaliwa ili iwasilishwe katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.
		14. Sehemu ya nane ya Jedwali la Tatu inaweka sharti kwa mtahiniwa anayetaka kufanya mitihani ya	14. Ilipendekezwa marekebisho yafanyike katika Kanuni ili kuweka mazingira	14. Rasimu ya Marekebisho ya sehemu ya nane ya Jedwali la Tatu yameandaliwa itarekebisha ili kuweka	14. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo imeandaliwa ili iwasilishwe katika Ofisi ya

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>bodi kupata mafunzo kwa muda usiopungua miezi sita, pasipo kuweka mazingira yanaweza kufupisha kipindi cha mafunzo ili kushughulikia mazingira ya dharura.</p> <p>15. Kanuni hazijaonesha mfano wa <i>Experience Report/Log book</i>.</p>	<p>yanayoweza kutoa fursa ya kupunguza muda wa masomo pasipo kuathiri masomo yanayotolewa ili kukidhi mazingira ya dharura.</p> <p>15. Ilipendekezwa yafanyike marekebisho katika Kanuni ili kuongeza mfano wa <i>Experience Report/Log book</i> katika Jedwali</p>	<p>mazingira yanaweza kufupisha kipindi cha mafunzo ili kushughulikia mazingira ya dharura ambapo sharti la kufanya mafunzo si chini ya kipindi cha miezi sita limefutwa.</p> <p>15. Rasimu ya marekebisho imeandaliwa kwa kuongeza mfano wa <i>Experience Report/Log book</i> mara baada ya Fomu Na. 5 katika Jedwali la Kwanza.</p>	<p>Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p> <p>15. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo imeandaliwa ili iwasilishwe katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p>
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA					
23.	The Tanzania Teachers' Professional	1. Kanuni ya 3 inatafsiri maneno " <i>Professional</i> "	1. Ilipendekezwa kwamba Kanuni ya 3 ifanyiwe	1. Rasimu ya Marekebisho ya Kanuni ya 3 imeandaliwa ili	1. Ni vema Kanuni ya 3 irekebishwe kwa kuboresha tafsiri ya

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
	<p>Board General, Regulations 2020.</p> <p>GN NA. 686 28 Agosti 2020</p>	<p><i>Standards</i>” kwa kurejea uainishaji uliotajwa katika Kanuni zenyewe. Hata hivyo Kanuni haijainisha viwango hivyo.</p>	<p>marekebisho kwa kuboresha tafsiri ya neno Professional standards ili ianische viwango vinavyohusika.</p>	<p>kuboresha Tafsiri ya maneno “<i>professional standards</i>” kwa kuweka rejea ya kifungu cha 71(2)(e) cha Sheria kinachotoa mamlaka ya kutungwa kwa kanuni kuhusu <i>Professional Standards</i>. Aidha, kanuni kuhusu <i>Professional standards</i> zitatungwa kwa mujibu wa kifungu cha 71(2)(e) cha Sheria.</p> <p>Maelezo</p> <p>Taarifa ya utekelezaji inaonesha kuwa kilichongezeka ni rejea ya Kifungu cha Sheria Mama kinachotoa mamlaka ya kutungwa kwa sheria ndogo hiyo, jambo ambalo halikuwa sehemu ya pendekezo.</p>	<p>maneno “<i>professional standards</i>” . Utekelezaji wa pendekezo hili hauna madhara bali ni ufafanuzi zaidi.</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>2. Kanuni ya 4 inaanziha Kamati ya usajili na utoaji wa leseni na Kamati ya maadili na nidhamu kinyume na masharti ya Kifungu cha 8 cha Sheria Mama, kinachoipa mamlaka Bodi pale iyakapoona inafaa inaweza kuanzisha Kamati hizo. Hata hivyo, Bodi inayopaswa</p>	<p>2. Ilipendekezwa kwamba marekebisho katika Kanuni ya 4 ili kufuta sharti la uanzishaji Kamati usajili na utoaji wa leseni na Kamati ya maadili na nidhamu ili kuendana na masharti ya Kifungu cha 8 cha Sheria Mama.</p>	<p>Kwahiyo basi ,pendekezo linalotaka kuboresha tafsiri ya maneno “professional standards” halijafanyiwa kazi jambo linalosababisha ugumu wa kueleweka kwa maneno professional standards katika sheria ndogo hiyo.</p> <p>2. Mapendekezo ya Kamati hayajatekelezwa kwa sababu Kanuni ya 4(1) haijaanzisha Kamati bali inatoa uwezo kwa Bodi kukasimisha baadhi ya majukumu yake kwa Kamati hizo. Hata hivyo, Wizara itafuta kanuni ya 4 (1) kwa sababu kifungu cha 8(1) cha Sheria kinatoa mamlaka kwa Bodi kuzipa Kamati baadhi ya majukumu yake.</p>	<p>2. Uamuzi wa kufuta Kanuni ya 4(1) ni wa msingi hata hivyo bado kuna umuhimu</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>kuanzisha Kamati hizo haijaundwa lakini Kamati zimeashaanzishwa.</p> <p>3. Kanuni ya 4(5) inaipa Kamati uwezo wa kualika mtu mwingine yeyote, masharti ambayo hayajawekwa katika Sheria Mama.</p>	<p>3. Ilipendekezwa marekebisho yafanyike katika Kanuni ya 4(5) ili kufuta uwezo wa Kamati kualika mtu mwingine yeyote.</p>	<p>3. Mapendekezo ya Kamati hayajatekelezwa na Wizara inashauri Kanuni ibaki kama ilivyo ili kusaidia Kamati kuweza kupata mtaalamu nje ya wanakamati kuisaidia Kamati katika suala mahsusi linalohitaji utaalamu ambao wanakamati hawana. Pia msingi wa kualika mtaalamu unatokana na kifungu cha 5(4) cha Sheria na pia kwa kuwa masharti kuhusu Kamati yanabainishwa kupitia Kanuni.</p>	<p>3. Ushauri wa Wizara unaegemea kwenye ruhusa iliyotolewa kwa Bodi na Kifungu Ushauri wa Wizara unaegemea kwenye ruhusa iliyotolewa kwa Bodi na Kifungu cha 5(4) cha Sheria Mama inawezesha Bodi kualika mtu yeyote kwa kuzingatia utalaamu ambao haupo miongoni mwao. Aidha, egemeo la ruhusa ni kutokana na Kifungu cha 9(1) cha Sheria ambacho kinaipa uwezo Bodi kukasimu majukumu yake kwa Kamati, hivyo basi utaratibu wa utekelezaji wa Bodi umechukuliwa na utaratibu wa Kamati ya Bodi.</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>4. Kanuni ya 6 inaweka majukumu ya Kamati ya Maadili na nidhamu pasipo kuainisha kwa ufafanuzi mzuri, hali inayoweza kuleta mgongano kati ya Kamati ya maadili na nidhamu na Kamati za muda za uchunguzi (Kamati za uchunguzi).</p>	<p>4. Ilipendekezwa Kanuni ya 6 ifanyiwe marekebisho ili kutofautisha majukumu ya Kamati ya Maadili na Nidhamu na yale ya Kamati ya Uchunguzi ili kuondoa uwezekano wa mgongano wa majukumu ya Kamati hizi.</p>	<p>4. Mapendekezo ya kamati hayajatekelezwa kwa kuzingatia kifungu cha 42 cha Sheria Mama. Kifungu hicho hakiitambui Kamati ya Uchunguzi kama Kamati ya Kudumu bali huandaliwa pale inapohitajika.</p> <p>Kwa upande mwingine Kamati ya Maadili na Nidhamu ni Kamati ya kudumu ambayo imeanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 8(2)(b) cha Sheria na majukumu yake yamefafanuliwa kwenye kwenye kanuni ya 6.</p>	<p>4. Kutokutekelezwa kwa pendekezo hakuathiri utekelezaji wa Kanuni</p>
		<p>5. Kanuni ya 8(2)(i) inataja "<i>Ordinary Certificate of Secondary Education</i>". Aina hii</p>	<p>5. Ilipendekezwa marekebisho yafanyike katika Kanuni 8(2)(i) ili kufuta maneno</p>	<p>5. Rasimu ya marekebisho ya Kanuni ya 8(2)(i) imeandaliwa ili kufuta maneno "Ordinary Certificate of Secondary" na badala</p>	<p>5. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yamewasilishwa katika Ofisi ya</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		ya cheti haipo katika aina za vyeti vinavyotambuliwa na Sheria za nchi.	“ <i>Ordinary Certificate of Secondary</i> ” na badala yake isomeke “ <i>Certificate of Secondary Education Examination</i> ”	yake kuandika “ <i>Certificate of Secondary</i> ” ili kuendana na majina sahihi ya vyeti kulingana na Sheria ya Baraza la Mitihani la Taifa, Sura ya 107.	Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.
		6. Kanuni ya 8(2)(ii) inataja <i>Certificate, Diploma na Degree in Teachers’ Education</i> . Madaraja haya hayapo nchini badala yake kuna <i>Certificate, Diploma na Degree in Education</i> .	6. Ilipendekezwa kuwa Kanuni ya 8(2)(ii) ifanyiwe marekebisho ili kufuta neno “ <i>teachers</i> ” na badala yake kuweka neno “ <i>Education</i> ”.	6. Rasimu ya marekebisho ya Kanuni ya 8(2)(b)(iii) imeandaliwa kwa kufuta maneno “ <i>Certificate, Diploma na Degree in Teachers’ Education</i> ” badala yake kuandika “ <i>The Certificate of Secondary Education; Certificate, Diploma or Degree in Education; and</i> ”	6. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yamewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.
		7. Kanuni ya 8(2)(b) haijabainisha kwa uwazi ngazi ya chini ya taaluma ya ualimu (<i>minimum</i>)	7. Ilipendekezwa Kanuni ya 8(2)(b) ifanyiwe marekebisho ili kuonesha kiwango	7. Mapendekezo ya Kamati yametokelezwa kwa kurekebisha kanuni ya 8 ili kuongeza sharti kuhusu kiwango cha chini cha taaluma ya	7. Inatarajiwa kwamba, Bodi itakayoundwa chini ya Kifungu cha 4 cha Sheria Mama itafafanua kiwango chini cha taaluma ya ualimu.

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p><i>qualification</i>)</p> <p>8. Kanuni ya 8(3) inazungumzia kuwasilisha vyeti vya taaluma kwa mamlaka zinazohusika (<i>relevant authorities</i>) kwa ajili ya uthibitisho wa vigezo</p>	<p>cha chini cha taaluma (<i>minimum qualification</i>).</p> <p>8. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kutafsiri neno <i>relevant authorities</i> na kubainisha taasisi au mamlaka ya kutoa tuzo au ulinganifu wa tuzo zenye dhamana</p>	<p>mwalimu kwa kadiri inavyoelekezwa kwenye kifungu cha 18(a) cha Sheria ambapo pia Bodi itatoa muongozo utaokaoainisha kiwango hicho cha taaluma.</p> <p>Mapendekezo ya Kamati yanaonekana yalikuwisha zingatwa kwenye kifungu cha 18(a) cha Sheria Mama ambacho kimeipa uwezo Bodi kufafanua kiwango cha chini cha taaluma ya ualimu.</p> <p>8. Rasimu ya marekebisho imeandaliwa ili kufafanua moja kwa moja na kwa ufasaha maneno "relevant authority" kwa ajili ya kuonesha mamlaka inayokusudiwa ni ile iliyotajwa katika Kanuni ndogo ya (2) ya</p>	<p>8. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yamewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>9. Kanuni ya 8(4) imetumia maneno <i>credential verification</i> pasipo kuweka tafsiri ya maneno haya ili kuonesha nini kinachokusudiwa.</p>	<p>kuondoa maneno <i>relevant authorities</i> ambayo hayajabainisha ni zipi.</p> <p>9. Ilipendekezwa marekebisho yafanyike ili kutafsiri neno <i>credential verification</i> kwa ajili ya kuondoa utata unaoweza kujitokeza kutokana na kinachokusudiwa.</p>	<p>Kanuni ya 8.</p> <p>9. Mapendekezo ya Kamati hayajatekelezwa kwa sababu maneno <i>credential verification</i> hayana utata wa maana, kwa kuwa yana maana ya kawaida (plain dictionary meaning).</p> <p>Yatokanayo</p> <p>Katika kikao cha tarehe 5 Februari, 2022 wameahidi kuwa Rasimu ya marekebisho itaandaliwa ili kuweka tafsiri ya maneno "credential verification"</p>	<p>Gazeti la Serikali.</p> <p>9. Maneno <i>credential verification</i> yanahitaji kufafanuliwa ili kueleweka vizuri.</p>
		<p>10. Kanuni ya 8(5)(b) inaelekeza muombaji kupatiwa</p>	<p>10. Ilipendekezwa marekebisho fayanyike katika</p>	<p>10. Rasimu ya marekebisho ya Kanuni ya 8(5)(b) imeandaliwa kwa</p>	<p>10. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>taarifa na msajili ndani ya siku thelathini kuhusu kukataliwa kwa maombi yake . Kanuni hii ni kinyume na masharti ya kifungu cha 19(4)(b) cha Sheria Mama kinachoelekeza taarifa kutolewa ndani ya siku thelathini baada ya kuwasilisha maombi.</p> <p>11. Kanuni ya 8(6) inaonesha kuwa cheti cha usajili kitapaswa kuwa na saini ya Mwenyekiti na Msajili pasipo kuonesha wazi iwapo ni Mwenyekiti wa Bodi au Kamati.</p>	<p>Kanuni ya 8(5)(b) ili kuonesha sharti la taarifa kukataliwa maombi kuwa itolewe ndani ya siku thelathini baada ya kuwasilisha maombi.</p> <p>11. Ilipendekezwa Kanuni ya 8(6) ifanyiwe marekebisho kuonesha kwa kuongeza maneno "wa Bodi" baada ya neno "Mwenyekiti".</p>	<p>kuongeza maneno "in a manner set out in section 19(4) of the Act" baada ya neno "determination" ili kuondoa kutokurudia maudhui.</p> <p>11. Rasimu ya marekebisho ya Kanuni ya 8(6) imeandaliwa ili kuonesha wazi kuwa Mwenyekiti anaye rejewa kwenye aya tajwa ni Mwenyekiti wa Bodi.</p>	<p>Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yamewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p> <p>11. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yamewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>12. Kanuni ya 9(2)(a),(b) imetumia neno “<i>subscribed</i>” lisilo sahihi kwa muktadha wa Kanuni hii.</p>	<p>12. Ilipendekezwa marekebisho katika Kanuni ya 9(2)(a)(b) kwa kufuta maneno “<i>subscribed fees</i>” na badala yake kuweka maneno “<i>Prescribed fees</i>”.</p>	<p>12. Rasimu ya marekebisho Kanuni ya 9(2)(a)(b) imeandaliwa ili kufuta neno “<i>subscribed</i>” na badala yake kuandika neno “<i>Prescribed</i>”.</p>	<p>Gazeti la Serikali.</p> <p>12. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yamewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p>
		<p>13. Kanuni ya 12(1) imetumia neno <i>revocation</i> ya cheti cha usajili ambalo halijatumika katika Sheria Mama ambayo katika Kifungu cha 32 imetumia maneno <i>cancellation</i> or <i>suspension</i>.</p>	<p>13. Ilipendekezwa Kanuni ya 12(1) ifanyiwe marekebisho kwa kufuta neno “<i>revocation</i>” na kutumia maneno “<i>cancellation</i> or <i>suspension</i>” ambayo yametumika katika Sheria Mama.</p>	<p>13. Rasimu ya marekebisho ya Kanuni imeandaliwa ili kufuta Kanuni ya 12(1) kwa kuwa maudhui ya kanuni hii yanaweza kuzingatiwa kwenye masharti ya msingi katika vifungu vya 32, 34 na 35 vya Sheria Mama</p>	<p>13. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yamewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>14. Kanuni ya 12(3) inaeleza kuwa mwalimu yeyote atakayekiuka masharti ya Kanuni ya 12(2) atakuwa ametenda kosa chini ya kanuni hizi. Hata hivyo, Kanuni hazioneshi makosa.</p> <p>15. Kanuni ya 13 inazungumzia kuhusu kurejesha (<i>surrender</i>) leseni na kuondolewa kwa jina kwa mujibu wa Kifungu cha 34, 35 na 37 vya Sheria Mama. Kifungu cha 34 na 35 vilivyorejewa havina uhusiano na masuala ya kuondoa jina (<i>deletion of name</i>).</p>	<p>14. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili makosa yawekwe katika Sheria Mama.</p> <p>15. Ilipendekezwa marekebisho yafanyike katika Kanuni ya 13 kwa kufuta rejea ya Kifungu cha 34 na 35 vya sheria mama.</p>	<p>14. Rasimu ya Marekebisho ya Kanuni ya 12(3) imeandaliwa ili kufuta kanuni ya 12(3) kwa sababu vifungu vya 58 na 59 vya Sheria Mama vimeainisha makosa na adhabu.</p> <p>15. Rasimu ya marekebisho ya Kanuni imeandaliwa ili kufuta rejea ya Kifungu cha 34 na 35 vya sheria mama ili vifungu visivyohusika.</p>	<p>14. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yamewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p> <p>15. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yamewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>16. Kanuni ya 13 inatumia neno <i>surrender</i> ambalo halijatumika katika sheria Mama</p>	<p>16. Ilipendekezwa marekebisho yafanyike katika Kanuni ya 13 kwa kufuta neno "<i>surrender</i>".</p>	<p>16. Mapendekezo ya Kamati hayajatekelezwa kwa sababu kwa kuzingatia marekebisho ya rejea ya kifungu cha 34 na 35 hitaji la urejeshwaji ni matokeo ya kufutwa.</p> <p>Maelezo</p> <p>Hakuna uhusiano kati ya pendekezo la kufuta neno "<i>surrender</i>" na hatua ya kuzingatia pendekezo la kufuta rejea ya Kanuni ya 34 na 35. Hata hivyo, kubakiza neno "<i>surrender</i>" hakuna madhara kwa utekelezaji wa sheria.</p> <p>Yatokanayo</p> <p>Rasimu ya marekebisho ya Kanuni ya 13 itaandaliwa ili kufuta neno "surrender".</p>	<p>16. Hatua iliyochukuliwa haitatui tatizo lililokuwa limebainiwa na Kamati. Bado kuna haja ya kuzingatia pendekezo.</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>17. Kanuni ya 14(2) inaipa mamlaka bodi kutunga, kusahisha mitihani pamoja na kutoa matokeo ya mitihani na vyeti. Majukumu haya hayajainishwa kama sehemu ya majukumu ya Bodi kwa mujibu wa Sheria Mama.</p>	<p>17. Ilipendekezwa marekebisho yafanyike katika Kanuni ya 14(2) ili kufuta jukumu la kutunga, kusahisha mitihani pamoja na kutoa matokeo ya mitihani na vyeti ili kuendana na sheria mama.</p>	<p>17. Mapendekezo ya Kamati hayajatekelezwa kwa sababu jukumu hili liko ndani ya majukumu ya Bodi katika kifungu cha 6 (1) (d) na (i) kwa kuwa ni sehemu ya udhibiti wa utaalamu wa ualimu. Vilevile hatua hiyo inajumuisha hitaji la masharti ya kifungu cha 36(2) cha Sheria.</p> <p>Maelezo</p> <p>Hatua hii imetokana na majukumu ya Bodi yanayotamkwa “<i>promote and regulate continuing professional development for teachers</i>” ambapo neno “<i>regulate</i>” limetafsiriwa kama kudhibiti na kuchukuliwa kuwa linaruhusu Bodi kuwa na jukumu la kutunga</p>	<p>17. Kutokutekelezwa kwa pendekezo la Kamati kunaendeleza kero ambayo haikukusudiwa na Bunge ilipotunga sheria Mama. Kero hiyo ni matokeo ya kuipa Bodi jukumu la kutunga, kusahisha mitihani pamoja na kutoa matokeo ya mitihani na vyeti.</p> <p>Bado kuna umuhimu wa kutekeleza pendekezo lililotolewa kuhusu kurekebisha kanuni ya 14(2).</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
				<p>mitihani.</p> <p>Aidha, hatua hiyo inachukuliwa kuwa inafanikisha utekelezaji wa masharti ya kifungu cha 36 (2) cha Sheria Mama ambacho kimeweka sharti la kufanya mtihani.</p> <p>Changamoto inayoendelea kuwepo ni Bodi kutunga mtihani ambalo si jukumu lake kwa maana neno "regulate" halina maana sawa na neno "examine" ambalo halijatumika. Kadhalika kutunga na kusahisha mitihani ni jukumu linalopaswa kufanywa na watu wenye sifa maalum, ambazo si vigezo vinavyotajwa katika muundo wa Bodi.</p>	

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		# 18. Kanuni ya 16 (b) inazungumzia sababu moja wapo ya kutohisha cheti cha usajili kuwa ni iwapo aliyesajiliwa atashindwa kufanya mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma. Hata hivyo, Kanuni haijaonesha wajibu wa mwajiri kulipia gharama za mafunzo ya kujiendeleza	18. Ilipendekezwa Serikali itafakari zaidi sharti la kumzuia mwalimu aliyeshindwa kuhuisha cheti kufundisha. Aidha Serikali ije na namna bora ya utaratibu wa ugharamiaji wa mafunzo kwa walimu hasa ukizingatia kuwa utaratibu wa	Yatokanayo Rasimu ya marekebisho ya Kanuni ya 14(2) itaandaliwa ili kufuta jukumu la kutunga, kusahisha mitihani pamoja na kutoa matokeo ya mitihani na vyeti ili kuendana na sheria mama 18. Rasimu ya Marekebisho ya Kanuni ya 16(b) imeandaliwa ili kuifuta na kuiandika upya kanuni ili kuipa Bodi mamlaka ya kutoa miongozo itakayobainisha viwango vya chini (minimum benchmark requirement) vitakavyozingatiwa katika mafunzo. Pia, Sehemu ya Sita itarekebishwa ili Serikali kupitia miongozo	18. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yamewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		kitaaluma.	mafunzo kwa kanuni hizi utaongeza gharama kubwa kwa walimu.	itakayotungwa na Bodi kutazingatia kuweka namna bora ya utaratibu wa ugharamiaji wa mafunzo kwa walimu.	
		19. Kanuni ya 18 inaeleza kuwa bodi itaweka utaratibu wa kufundisha chini ya usimamizi wa moja kwa moja. Hata hivyo utaratibu huo hauoneshwi/hauko wazi chini ya Kanuni hizi.	19. Ilipendekezwa marekebisho yafanyike katika Kanuni ya 18 ili ioneshe bayana mfumo wa kufundisha chini ya usimamizi wa moja kwa moja.	19. Rasimu ya marekebisho ya Kanuni ya 18 imeandaliwa kwa kuifuata na kuiandika upya Kanuni ya 18 ili kuipa Bodi mamlaka ya kuandaa muongozo kuhusu kufundisha chini ya usimamizi wa moja kwa moja ili kuendana na kifungu cha 28(1)(c) cha Sheria.	19. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatia ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yamewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.
		20. Kanuni ya 20 imeainisha sehemu ya maudhui ya Jedwali la Nne lakini haifanyi rejea ya Jedwali hilo kuhusu Ada ya Walimu wa	20. Ilipendekezwa Kanuni ya 20 ifanyiwe marekebisho ili ifanye rejea ya Jedwali la Nne	20. Mapendekezo hayajatekelezwa kwa sababu Jedwali la Nne ni Fomu ya Maombi ya Usajili wa walimu wa kigeni. Msingi wa ujazaji wa fomu hiyo umewekwa	20. Hatua iliyochukuliwa ina tija katika utekelezaji wa Kanuni.

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>Kigeni.</p> <p>21. Kanuni ya 20(1)(b) inaweka masharti ya usajili kwa walimu wasio na uraia wa Tanzania kuwa watapaswa kuwa na kibali cha ukaazi na kibali cha kazi. Masharti haya hayajaainishwa katika Sheria Mama na Mikataba ya Kikanda (mfano EAC).</p>	<p>21. Ilipendekeza marekebisho katika Kanuni ya 20(1)(b) kwa kufuta masharti ya usajili kwa walimu wasio na uraia wa Tanzania kuwa na kibali cha ukaazi na kibali cha kazi, ili kuendana na masharti ya sheria mama na Mikataba ya Kikanda.</p>	<p>kwenye kanuni ya 19 (1) ambayo tayari imerejewa kwenye Jedwali la Nne. Kanuni ya 20 inafafanua masharti ya usajili ambayo kimsingi hayahusiani na maudhui yaliyo kwenye fomu ya usajili iliyo kwenye Jedwali la Nne.</p> <p>21. Mapendekezo hayajatekelezwa kwa sababu Kanuni zinalenga kuwezesha utekelezaji mzuri zaidi wa Sheria, matakwa ya kuhakikisha uhalali wa kuishi na kufanya kazi ni muhimu ili kusajili walimu wa kigeni waliokidhi masharti ya Sheria za nchi. Vilevile takwa hili limewekwa kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 46(5) cha Sheria ya Elimu, kama</p>	<p>21. Hatua ya kutotekeleza pendekezo ina tija.</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>22. Kanuni ya 23(4) inaweka sharti la malipo ya ada kwa wanaotoa huduma ya mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma. Hata hivyo Kanuni hazijaonesha ada hizo.</p>	<p>22. Ilipendekewa marekebisho yafanyike katika Kanuni ya 23(4) ifanyiwe kuainisha ili iainishe ada zinazohusika.</p>	<p>ilivyorekebisha kupitia Sheria Na.1 ya mwaka 2015 (<i>Non Citizen Employment Regulation Act, Cap 436</i>). Pia Sheria za nchi zinatekelezwa kwa kuzingatia Sheria za kikanda.</p> <p>Yatokanayo</p> <p>Wizara imelichukua kwa ajili ya kulitafakari zaidi na kufanya mashauriano ndani ya serikali.</p> <p>22. Rasimu ya marekebisho ya Kanuni imeandaliwa ili kurekebisha Kanuni inayoanzisha Jedwali la Pili kwa kuongeza Kanuni ya 23(4) na kuongeza kipengele C katika Jedwali la Pili kwa lengo kuweka ada ya shilingi 1,000,000 kama malipo ya maombi ya</p>	<p>22. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yamewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>23. Kanuni ya 23(2) pamoja na masuala mengine, inaeleza kuhusu kukataliwa kwa maombi ya kutoa huduma ya mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma pasipo kuonesha sababu za kukataa maombi yanayohusika na haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi wa kukataliwa.</p>	<p>23. Ilipendekezwa marekebisho yafanyike katika Kanuni ya 23 ili kuweka masharti ya kubaibisha sababu za kukataa maombi.</p>	<p>kupatiwa ithbati .</p> <p>23. Rasimu ya marekebisho ya Kanuni imeandaliwa kwa kuongeza Kanuni ndogo mpya ya (3) ili kubainisha sababu za kukataa maombi .</p>	<p>23. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yamewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p>
		<p>24. Kanuni ya 24 inaweka orodha ya vitu ambavyo vitapaswa kuwasilishwa na mtoa huduma aliyepewa idhini ya kutoa mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma, kuwa</p>	<p>24. Ilipendekezwa marekebisho yafanyike katika Kanuni ya 24 ili kuongeza sharti la kumtaka mtoa huduma kuendesha kozi ambazo zimeandaliwa kwa mfumo wa alama na</p>	<p>24. Mapendekezo ya Kamati hayajatekelezwa kwa sababu Kanuni ya 26 na 29 (1) (e) inatoa fursa kwa Bodi kutathimini, kupanga na kuidhinisha programu na aina za mafunzo kulingana na mahitaji. Aidha, kanuni ya 29 (3) imetoa sharti la</p>	<p>24. Ni vema pendekezo likatekelezwa.</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>atapaswa kuwasilisha majina ya washiriki, kozi zitakazotolewa na mapendekezo. Hata hivyo Kanuni hazijaonesha hitaji la mhusika kutoa vyeti na kuweka mfumo wa masomo kwa alama kwa kila kozi (<i>academic credit system</i>).</p>	<p>kutoa vyeti kwa washiriki.</p>	<p>kutoa vyeti. Utoaji alama ni suala la kiutawala chini ya kanuni ya 26.</p> <p>Maelezo</p> <p>Hatua ya kutotekeleza pendekezo kuhusu kurekebisha Kanuni ya 24 inaweza kuzingatiwa kutokana na masharti ya Kanuni ya 29(3) inayoitaka Bodi au mtoa huduma kutoa cheti cha mafunzo. Lengo la cheti hicho ni kumtambua mwalimu aliyepata mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma ambalo ndio lengo la Sheria Kuu. Hata hivyo, maelezo kuhusiana na Kanuni ya 26 hayahusiani na utoaji alama kuwa suala la kiutawala.</p>	
		<p>25. Kanuni ya 29(1) imeacha baadhi ya</p>	<p>25. Ilipendekezwa marekebisho katika</p>	<p>25. Mapendekezo ya Kamati hayajatekelezwa kwa</p>	<p>25. Hatua iliyochukuliwa inatoa fursa kwa</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		maeneo muhimu katika mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma yatakayotolewa.	Kanuni ya 29(1) ili kuongeza masuala yanayohusu <i>Professionalism, Subject matter knowledge, Research skills, Psychosocial na Environmental management.</i>	sababu Kanuni ya 29 (1) (e) inatoa fursa kwa Bodi kuongeza maeneo mengine ya kujiendeleza kulingana na mahitaji. Maelezo Bodi ya Taaluma ya Walimu imepewa uwezo wa kubainisha maeneo mengine yote muhimu zaidi ya maeneo yalitotajwa na wadau ambayo baadae yalichukuliwa katika mapendekezo. Hata hivyo, katika kikao na Waziri wa Elimu, majibu ya Wizara pendekezo hilo lilipangwa kuzingatiwa na Wizara.	utekekelezaji mzuri wa Kanuni ya 29 (1) (e) unaozingatia mahitaji kulingana na wakati na muktadha unaohusika.
		26. Kanuni ya 29(4) inaweka sharti kwa walimu walipoatiwa vyeti vya usajili kuwasilisha vyeti	26. Ilipendekezwa marekebisho yafanyike katika Kanuni ya 29(4) ili kuweka utaratibu wa	26. Rasimu ya marekebisho imeandaliwa ili kurekebisha ya Kanuni 29(4) kwa kutambua njia ya kielektroniki katika	26. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yamewasilishwa

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>hivyo katika bodi kwa kumbukumbuku. Kanuni haijaonesha umuhimu wa kuwasilisha kwa njia ya mtandao ili kuondokana na mlundikano wa nakalamango nyingi kutokana na wingi wa walimu nchini.</p> <p>27. Kichwa cha habari cha sehemu ya VII kinazungumzia mashauri ya uchunguzi wa Kamati badala ya Bodi.</p> <p>28. Kanuni ya 30(1) na (2) inaweka utaratibu tofauti wa namna ya</p>	<p>kuwasilisha nakala za vyeti kwa njia ya mtandao.</p> <p>27. Ilipendekezwa marekebisho yafanyike katika Kichwa cha habari cha Sehemu ya VII kwa kufuta maneno “<i>proceedings of inquiry</i>” na badala yake kuandika maneno “<i>Proceedings of inquiry by the board</i>”.</p> <p>28. Ilipendekezwa marekebisho</p>	<p>uwasilishaji wa nakala za vyeti vya mafunzo .</p> <p>27. Rasimu ya Marekebisho imeandaliwa ili kuweka kichwa habari cha Sehemu ya VII kisomeke “<i>Proceedings of inquiry by the Board</i>”.</p> <p>28. Rasimu ya Mapendekezo marekebisho</p>	<p>katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p> <p>27. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yamewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p> <p>28. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>kutoa notisi ya kusudio la kufanya uchunguzi tofauti na utaratibu uliowekwa na Kifungu cha 45(1) cha Sheria Mama.</p> <p>29. Kanuni ya 32 inatoa fursa ya muhusika katika shauri kuwakilishwa na wakili tu, pasipo kuweka nafasi ya mtu asiye wakili.</p>	<p>yafanyike katika Kanuni ya 30(1) na (2) ili kuweka utaratibu wa kutoa notisi ya kusudio la kufanya uchunguzi unaoendana na uliowekwa na sheria mama. Aidha notisi ya kusudio la kufanya uchunguzi iliyo katika Kifungu cha 45(1) iundiwe Jedwali katika Kanuni.</p> <p>29. Ilipendekezwa marekebisho yafanyike katika Kanuni ya 32 ili kuruhusu nafasi ya watu wengine wa fani tofauti kuwakilisha.</p>	<p>imeandaliwa ili kuingiza kifungu kipya cha 30 kuhusu <i>Notice of Inquiry</i> pamoja na kuweka jedwali la Saba la <i>Notice of Inquiry</i>.</p> <p>29. Rasimu ya Marekebisho ya Kanuni ya 32 imeandaliwa ili kuongeza uwakilishi mwingine mbali na wakili, kwa kuongeza maneno "or such other personal representative" kati ya neno "advocate" na "shall".</p>	<p>Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yamewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali</p> <p>29. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yamewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>30. Kanuni ya 36(2) inazungumzia kuhusu utoaji wa uamuzi na kutumia kwamba mara baada ya kusikilizwa kwa shauri, uamuzi utatolewa mapema iwezekanavyo.</p>	<p>30. Ilipendekezwa marekebisho yafanyike katika Kanuni ya 36(2) ili kuonesha muda mahsusi wa kutoa uamuzi.</p>	<p>30. Rasimu ya marekebisho ya Kanuni ya 36(2) imeandaliwa ili kuweka muda wa siku 14 kwa ajili ya Bodi kuwasilisha uamuzi yake.</p>	<p>30. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yamewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p>
		<p>31. Kanuni ya 37(1) inaweka sharti la kukata rufaa dhidi ya uamuzi wa bodi kuwa ni siku 30 kinyume na kifungu cha 49(1) cha sheria mama kinachoweka muda wa siku 90</p>	<p>31. Ilipendekezwa marekebisho yafanyike katika Kanuni ya 37(1) kwa kufuta wa “muda wa siku 30” wa kukata rufaa na badala yake kuandika “siku tisini (90)” ili kuendana na sheria mama.</p>	<p>31. Rasimu ya marekebisho ya Kanuni ya 37(1) imeandaliwa ili kufanya marekebisho ya kanuni 37(1) kwa lengo la kuweka muda wa siku tisini wa kukata rufaa ilivyo kwenye kifungu cha 49(1) cha Sheria.</p>	<p>31. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yamewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p>
		<p>32. Kanuni ya 37(2) inaweka utaratibu wa kukata rufaa kuwa</p>	<p>32. Ilipendekezwa kwamba, Kanuni ya 37(2) ifanyiwe</p>	<p>32. Mapendekezo ya Kamati hayajatekelezwa kwa sababu Kanuni ililenga</p>	<p>32. Hatua ya kutotekeleza pendekezo haiweki uwezekano wa</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		mrufani atapaswa kueleza sababu za rufaa na anaweza kuonesha ushahidi wa sababu hizo. Kanuni haijaonesha <i>format</i> ya rufaa.	marekebisho ili kuweka Jedwali la muundo ya rufaa.	<p>kutokuweka muundo maalum wa rufaa ili kurahisisha utaratibu hata hivyo kanuni inarekebishwa ili kurejea kifungu cha 49 cha Sheria.</p> <p>Maelezo</p> <p>Pendekezo lililenga kumuongoza mrufani ili kurahisisha mchakato na majibu ya Wizara yaliafikiana na pendekezo. Hata hivyo, hatua inayoripotiwa inatofautiana na pendekezo na majibu yaliyotolewa na Wizara na hivyo, kubakisha tatizo la kutomuongoza mrufani.</p>	<p>kumuongoza mrufani jambo ambalo linakwamisha urahisi wa kushughulikia rufaa. Hivyo, pendekezo lizingatiwe.</p>
		33. Kanuni ya 37(3) inampa Waziri Mamlaka ya kuchagua Kamati	33. Ilipendekezwa kuwa Kanuni ya 37(3) ifanyiwe marekebisho kwa	33. Mapendekezo ya Kamati hayajatekelezwa kwa sababu Kanuni zimeleza kutekeleza	33. Pendekezo la kurekebisha Kanuni ya 37(3) bado linahitaji kutekelezwa.

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>mara baada ya kuwa amepokea rufaa. Mamlaka haya hayajabainishwa na Sheria Mama bali Mamlaka ya kushughulikia rufaa yamewekwa kwa Waziri pekee.</p> <p>34. Kanuni ya 37(5) inaweka hiari kwa Waziri kuzingatia ushahidi atakaona unafaa wakati wa rufaa. Kanuni haijazingatia kuwa haki ya kusikilizwa ni muhimu.</p> <p>35. Kanuni ya 38(1) imeweka utaratibu kuwa mhusika yeyote katika kesi anaweza kuondoa</p>	<p>kuondoa mamlaka ya kuteua Kamati ili kuendana na masharti ya Sheria Mama.</p> <p>34. Ilipendekezwa Kanuni ya 37(5) ifanyiwe marekebisho kwa kuongeza kanuni itakayompa Mrufani haki ya kusikilizwa.</p> <p>35. Ilipendekezwa marekebisho yafanyike katika Kanuni ya 38(1) ili kuonesha mwenye</p>	<p>kwa urahisi zaidi Sheria, kuteua Kamati ni utaratibu wa kumsaidia Waziri kufikia uamuzi iwapo ataona inafaa.</p> <p>34. Rasimu ya marekebisho ya Kanuni ya 37(5) imeandaliwa ili kufuta na kuiandika upya ili kuweka aya (a) inayoweka haki ya kusikilizwa kwa wahusika katika shauri.</p> <p>35. Rasimu ya Marekebisho ya Kanuni ya 38(1) imeandaliwa kwa kufuta maneno "Any party" na badala yake kuwandika</p>	<p>34. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatia ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yamewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p> <p>35. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatia ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yamewasilishwa</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>rufaa iliyowasilishwa. Kimsingi rufaa haiwezi kuondolewa na wahusika wote katika walio katika kesi, badala yake mwenye uwezo wa kufanya hivyo ni mrufani tu.</p> <p>36. Kanuni ya 38(2) inaelekeza kuwa maombi ya kuondoa rufaa yatawasilishwa kwa maandishi kwa bodi badala ya Waziri ambaye ndiye mwenye Mamlaka ya kusikiliza rufaa.</p> <p>37. Kanuni ya 38(3) inampa Waziri uwezo wa kuondoa uamuzi wake kuhusu rufaa iliyowasilishwa</p>	<p>uwezo wa kuondoa rufaa ni mrufani tu.</p> <p>36. Ilipendekezwa marekebisho ya Kanuni 38(2) yafanyike ili ionesha maombi ya maandishi kuondoa rufaa yatawasilishwa kwa Waziri.</p> <p>37. Ilipendekezwa marekebisho fayanyike katika Kanuni ya 38(3) kwa kufuta mamlaka ya</p>	<p>maneno “A party lodging an appeal” ili kumruhusu mkata rufaa pekee kuwa na uwezo wa kuondoa rufaa.</p> <p>36. Rasimu ya marekebisho ya Kanuni ya 38(2) imeandaliwa kwa kufuta neno “Board” na badala yake kuandika neno “Minister” ili kuonyesha maombi ya maandishi kuondoa rufaa yatawasilishwa kwa Waziri.</p> <p>37. Rasimu ya marekebebisho imeandaliwa ambapo inafuta Kanuni ya 38(3) ili kuondoa uwezo wa</p>	<p>katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p> <p>36. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yamewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p> <p>37. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yamewasilishwa</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		kwake kinyume na sheria mama ambayo haitoi fursa ya Waziri kuondoa uamuzi wake.	Waziri kubadili uamuzi aliokuwa ameutoa awali ili kuendana na sheria mama.	Waziri kuondoa uamuzi alioufanya kuhusu rufaa.	katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.
		38. Kanuni ya 39(1) inazungumiza mamlaka ya bodi kuitisha taarifa zaidi wakati wa kuzingatia maombi ya usajili. Hata hivyo kifungu hiki kimewekwa katika eneo la kanuni za masuala mengineyo badala kuwekwa katika maeneo yanayohusika na maombi ya usajili ili kuleta mtiririko mzuri wa uandishi.	38. Ilipendekezwa kuwa Kanuni ya 39(1) ifanyiwe marekebisho ili kuhamisha maudhui ya Kanuni ya 39(1) na yapelekwe katika Sehemu ya III na IV ili kuleta mtiririko mzuri wa uandishi	38. Mapendekezo ya Kamati hayajatekelezwa kwa sababu masharti ya kifungu cha 39 yanajitosheleza kuwepo katika sehemu ya masharti mengineyo kwa kuwa ni masharti ambayo yanatumika kwa maombi chini ya sehemu ya Tatu na Nne ya Sheria.	38. Hatua iliyochukuliwa inaridhisha kwamba kuna umuhimu wa Kanuni hiyo kuwa katika sehemu ya masharti mengineyo, kwa kuwa inahusu mambo yaliyo katika sehemu zaidi ya moja na haiwezi kugawanyika katika sehemu tofauti.
		39. Kanuni ya 40 imelekeza	39. Ilipendekezwa marekebisho	39. Rasimu ya marekebisho imeandaliwa kwa	39. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>mawasiliano yote kwa bodi yapitie msajili “<i>registrar</i>”. Neno “<i>registrar</i>” limetumika maeneo mengi katika Kanuni pasipo kuwekewa maana yake.</p> <p>40. Kanuni ya 41(2)(b) imetumia kimakosa neno “<i>been</i>” badala ya neno “<i>being</i>”</p>	<p>yafanyike katika Kanuni iongeze tafsiri ya neno “<i>registrar</i>”</p> <p>40. Ilipendekezwa Kanuni ya 41(2)(b) ifanyiwe marekebisho kwa kufuta neno “<i>been</i>” na badala yake kuandika neno “<i>being</i>” ili kuleta maana iliyokusudiwa.</p>	<p>kuweka tafsiri ya neno <i>Registrar</i> kama ilivyotafsiriwa kwenye Sheria mama.</p> <p>40. Rasimu ya marekebisho ya Kanuni ya 41(2)(b) imeandaliwa ili kufuta neno “<i>been</i>” na badala yake kuandika neno “<i>being</i>” kwa lengo la kuleta maana iliyokusudiwa.</p>	<p>ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yamewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p> <p>40. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yamewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p>
		<p>41. Sehemu ya Nne ya Jedwali la Kwanza inasomeka “<i>teachers education</i>” hivyo haioneshi viwango</p>	<p>41. Ilipendekezwa Sehemu ya Nne ya Jedwali la Kwanza ifanyiwe marekebisho kwa</p>	<p>41. Mapendekezo ya Kamati hayajatekelezwa kwa sababu Sehemu ya Nne ya Jedwali la Kwanza ipo sawa kwani kuna</p>	<p>41. Kutokutekelezwa kwa pendekezo hakuna athari katika utekelezaji wa Kanuni.</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>vya taaluma za walimu.</p> <p>42. Fomu ya usajili katika Jedwali la Kwanza haijaweka sharti la kuthibitisha uraia wa waombaji.</p>	<p>kufuta maneno “Teachers Education” na badala yake kuandika maneno “teaching Professional certificates”.</p> <p>42. Ilipendekezwa Fomu ya Usajili ifanyiwe marekebisho ili ionesha sharti la uthibitisho wa uraia wa muombaji.</p>	<p>sehemu ya kubainisha taarifa kuhusu taaluma ya ualimu ya mwombaji.</p> <p>42. Rasimu ya marekebisho ya Fomu ya Usajili katika Jedwali la Kwanza imeandaliwa ili kuweka hitaji la kuambatisha nyaraka za kuthibitisha uraia.</p> <p>Maelezo</p> <p>Hatua iliyochukuliwa inahusu kuweka maelezo mwisho wa sehemu ya Kwanza ya Jedwali la Kwanza baada ya mstari “<i>place of birth</i>” sharti linalotaka kuambatisha nakala ya kitambulisho cha Taifa</p>	<p>42. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yamewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>43. Jedwali la Pili la Kanuni hizi halijafanya rejea ya Kanuni ya 10(2)(b) ambayo ina maudhui ya kuanzishwa kwa Jedwali hilo.</p>	<p>43. Ilipendekezwa Jedwali la Pili lifanyiwe marekebisho kwa kuongeza Kanuni ya 10(2)(b)</p>	<p>au nakala ya cheti cha kuzaliwa ikiwa na ithibati.</p> <p>Hata hivyo, Rasimu ya marekebisho imetumia maneno '<i>citizen identity</i>' lakini ingefaa kutumia maneno "<i>national identity</i>"</p> <p>43. Rasimu ya mapendekezo ya marekebisho ya Jedwali la Pili imeandaliwa ili kufanya Jedwali hilo lirejee Kanuni ya 8 (2) (a) na 10 (2) (b) ya Kanuni kwa pamoja.</p>	<p>43. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yamewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p>
		<p>44. Jedwali la Pili halijaonesha viwango vya ada vinavyopaswa kulipa kwa vyeti vya walimu wa kigeni</p>	<p>44. Ilipendekezwa marekebisho yafanyike katika Jedwali la Pili kuainisha ada ya</p>	<p>44. Rasimu ya marekebisho ya Kanuni imeandaliwa kwa lengo la kurekebisha Jedwali la Pili ili kuainisha ada ya</p>	<p>44. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yamewasilishwa katika Ofisi ya</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		vilivyopotea na ada ya kuhuisha leseni za walimu wa kigeni.	vyeti vilivyopotea.	vyeti vilivyopotea.	Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.
		45. Sehemu ya 3(b) ya Jedwali la Nne haioneshi wazi aina za vigezo vya usajili kwa walimu wa kigeni.	45. Ilipendekezwa kuwa Sehemu ya 3(b) ifanyiwe marekebisho kwa kufuta maneno “Teachers Education” na badala yake kuandika maneno “teaching Professional Certificates” .	45. Mapendekezo ya Kamati hayajatekelezwa kwa sababu Maneno “teachers education” katika Sehemu ya 3(b) ya Jedwali la Nne yanalenga kupata ngazi ya elimu/taaluma na sio vyeti vya kitaalamu. Hivyo maneno yaliyopo yanajitosheleza.	45. Kutokutekelezwa kwa pendekezo hakuna athari katika utekelezaji wa Kanuni.
		46. Fomu ya usajili wa walimu wa kigeni haijaweka sharti la kuthibitisha uraia wa waombaji	46. Ilipendekezwa Fomu ya usajili wa walimu wa kigeni ifanyiwe marekebisho ili ioneshi sharti la uthibitisho wa uraia wa muombaji.	46. Rasimu ya marekebisho ya Fomu ya Usajili katika Jedwali la Tano imeandaliwa ili kuweka hitaji la kuambatisha nyaraka za kuthibitisha uraia kwa mwalimu kigeni.	46. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yamewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>47. Fomu ya Jedwali la Tano halijaweka sharti la kumtaka muombaji kuonesha ushahidi wa kisheria wa kusajiliwa.</p> <p>48. Fomu ya usajili haiweka sharti la kuthibitisha uraia wa muombaji.</p>	<p>47. Ilipendekezwa Fomu ifanyiwe marekebisho kuweka sharti la kuambatisha wasifu wa muombaji na cheti cha usajili.</p> <p>48. Ilipendekezwa kwamba marekebisho katika Fomu ya usajili ili iweka sharti la muombaji kuwasilisha</p>	<p>Maelezo</p> <p>Hatua iliyochukuliwa inahusu kuweka maelezo mwisho wa sehemu ya Kwanza ya Jedwali la Kwanza baada ya mstari “attach certified copies of birth certificate and passport”</p> <p>47. Mapendekezo ya Kamati hayajatekelezwa kwa sababu fomu tajwa inahusu maombi ya ithibati ya mtoa mafunzo endelevu ya walimu chini ya kanuni ya 23 ambapo usajili si kigezo katika maombi hayo.</p> <p>48. Mapendekezo ya Kamati yametekelezwa kwa kurekebisha fomu ya usajili ili kuweka hitaji la kuwasilisha kitambulisho cha taifa kwa ajili ya kuthibitisha uraia wa</p>	<p>kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p> <p>47. Kutotekelezwa kwa pendekezo hakuna athari kwa kwakua aya ya 5 ya Jedwali la Tano imeweka sharti la kuambatisha wasifu.</p> <p>48. Mapendekezo yapo katika mchakato wa kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo hii yamewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		49. Kanuni zinazungumzia uanzishaji wa rejesta mbalimbali za walimu kama vile rejesta ya walimu waliosajiliwa, rejesta ya walimu wa kigeni n.k. Hata hivyo rejesta hizo hazijabainishwa bayana.	49. Ilipendekezwa Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuziweka rejesta katika kanuni mahsusi katika kanuni hizi na zionekane katika sehemu ya majedwali ya Kanuni hizi.	mwombaji. 49. Mapendekezo ya Kamati hayajatekelezwa kwa sababu kwa mujibu wa kifungu cha 17 cha Sheria Rejesta ya Walimu wote ni moja tu ambapo vipengele vya kuzingatiwa hapo bodi itakapoandaa rejesta hiyo vimeainishwa chini ya kifungu tajwa. Vilevile kwa mujibu kifungu hicho cha 17, Rejesta iko katika dhamana ya Msajili na ni kwa matumizi ya kiutawala kwa kuwa maudhui ya rejesta hutolewa au au kuwekwa wazi kupitia chapisho katika Gazeti la Serikali kwa mujibu wa kifungu cha 20 cha	kuhakikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. 49. Kutokutekelezwa kwa pendekezo hakuna athari katika utekelezaji wa Kanuni.

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Pendekezo lililotolewa na Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
				Sheria. Hivyo siyo hitaji kuweka Rejesta katika Majedwali.	



Jasson S. Rweikiza (Mb)

MWENYEKITI

**Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria
Ndogo 18 Februari, 2022**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



BUNGE LA TANZANIA

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO

**JEDWALI LA UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO NANE (8) ZILIZOWASILISHWA KATIKA
MKUTANO WA TANO WA BUNGE, TAREHE 9 NOVEMBA, 2021**

#	Namba ya Tangazo la Serikali (Gn Number)	Jina la Sheria Ndogo (Name)	Sheria Inayotoa Madaraka (Enabling Law)	Mamlaka Inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi (Observations)	Maoni na Mapendekezo (Recommendations)
TOLEO NA. 36 LA TAREHE 3 SEPTEMBER, 2021						
1.	GN NA. 642 <i>(TS Na. 642)</i> 3 Septemba, 2021	The Tanzania Meteorological Authority (Cost Recovery on Meteorological Services) Regulations, 2021	THE TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY ACT, (SURA. 157) (Zimetungwa chini ya Kifungu cha 54(2)(i))	WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI	1. Kanuni ya 3 imetafsiri baadhi tu ya huduma za hali ya hewa zikiwemo <i>consultancy services, industrial activities, marine services, marine meteorological services</i> . Hata hivyo Kanuni imecha kuweka tafsiri ya huduma nyingine za hali ya hewa zinazotolewa na Mamlaka ya hali ya hewa. Hali hii inaweza kusababisha baadhi ya wanaotoa huduma zilizoachwa kutofahamu wigo	1. Kanuni ya 3 ifanyiwe marekebisho ili kuweka tafsiri ya huduma nyingine za hali ya hewa zinazotolewa na Mamlaka ya hali ya hewa kwa lengo la kuondoa uwezekano wa kusababisha kutofahamika wigo wa huduma zinazotolewa kwa shughuli inayohusika.

#	Namba ya Tangazo la Serikali (Gn Number)	Jina la Sheria Ndogo (Name)	Sheria Inayotoa Madaraka (Enabling Law)	Mamlaka Inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi (Observations)	Maoni na Mapendekezo (Recommendations)
					<p>wa huduma wanayoweza kupatiwa na Mamlaka kwa kutokana na shughuli wanazozitekeleza.</p> <p>2. Kanuni hazijaonesha uwezekano wa wachimbaji wadogo kupatiwa huduma za taarifa za hali ya hewa iwapo watahitaji kupatiwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli zao za uchimbaji wa madini.</p>	<p>2. Wizara itafakari ili kuona umuhimu kuwapa fursa Wachimbaji wadogo kupata huduma mahsusi za hali ya hewa badala ya kuwekwa katika kundi la ambalo linapatiwa huduma za hali ya hewa kwa ujumla.</p>
2.	GN NA. 643 (TS Na. 643)	The Tanzania Meteorological Authority	THE TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY ACT,	WIZARA YA UJENZI NA	Jedwali la Pili la Kanuni hizi linalohusu hati ya wito limerejea	Jedwali lifamiwe marekebisho ili kufuta Kanuni ya 18(2)

#	Namba ya Tangazo la Serikali (Gn Number)	Jina la Sheria Ndogo (Name)	Sheria Inayotoa Madaraka (Enabling Law)	Mamlaka Inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi (Observations)	Maoni na Mapendekezo (Recommendations)
	3 Septemba, 2021	(Complaints Handling Procedures) Regulations, 2021	(SURA. 157) (Zimetungwa chini ya Kifungu cha 54	UCHUKUZI	kimakosa kuanzishwa chini ya Kanuni ya 18(2) badala ya Kanuni ya 17(2) ambayo ndio mahsusi kuhusu hati ya wito (<i>summons</i>)	inayorejewa na badala yake irejewe Kanuni ya 17(2) .
TOLEO NA. 39 LA TAREHE 24 SEPTEMBER, 2021						
3.	GN NA. 680 (TS Na. 680) 24 Septemba, 2021	The Standards (Cooperation in Execution of Powers and Functions) Regulations, 2021	THE STANDARDS ACT, (SURA. 130) (Zimetungwa chini ya Kifungu cha 36(1) na (3)(f))	WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA	Tafsiri ya neno " <i>standards</i> " iliyo katika Kanuni ya 2 ifanye rejea ya kifungu cha Sheria mama kinachotafsiri neno " <i>standards</i> " badala ya kuweka tafsiri inayojirudia.	Marekebisho yafanyike ili kufanya rejea ya kifungu cha sheria mama badala ya kurudia tafsiri iliyotolewa katika sheria mama.
4.	GN NA. 681 (TS Na. 681) 24 Septemba, 2021	The Standards (Imports Registration and Batch Certification)	THE STANDARDS ACT, (SURA. 130)	WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA	Fomu Na. 10 katika Jedwali la Kwanza inarejea kuanzishwa chini ya Kanuni ya 18(2) ambayo haihusiani na	Fomu Na. 10 ifanyiwe marekebisho kwa kufuta Kanuni ya 18(2) inayorejewa na badala yake irejee Kanuni ya

#	Namba ya Tangazo la Serikali (Gn Number)	Jina la Sheria Ndogo (Name)	Sheria Inayotoa Madaraka (Enabling Law)	Mamlaka Inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi (Observations)	Maoni na Mapendekezo (Recommendations)
		Regulations, 2021	(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 36(1) na (3)(f))		kibali cha kuruhusi uingizaji wa bidhaa kutoka nje (<i>Import clearance permit</i>). Kanuni sahihi kuhusu kibali cha kuruhusi uingizaji wa bidhaa kutoka nje (<i>Import clearance permit</i>) ni 18(1)	18(1)
5.	GN NA. 682 (TS Na. 682) 24 Septemba, 2021	The Standards (Recall, Seizure and Disposal of Product) Regulations, 2021	THE STANDARDS ACT, (SURA. 130) (Zimetungwa chini ya Kifungu cha 36(1) na (3)(f))	WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA	1. Kanuni zimerejea kuanzishwa chini ya Kifungu cha 36(3)(f) pasipo kurejea Kifungu cha 36(1) ambacho kinaweka mamlaka ya jumla ya Waziri kutunga Kanuni. 2. Kanuni ya 2 imetafsiri neno " <i>product</i> " kuwa linajumuisha	1. Kanuni ifayiwe marekebisho ili kufanya rejea ya Kifungu cha 36(1). 2. Kanuni ya 2 ifanyiwe marekebisho ili kuondoa neno " <i>services</i> " katika

#	Namba ya Tangazo la Serikali (Gn Number)	Jina la Sheria Ndogo (Name)	Sheria Inayotoa Madaraka (Enabling Law)	Mamlaka Inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi (Observations)	Maoni na Mapendekezo (Recommendations)
					<p>huduma "services" zilizobuniwa kwa lengo la kutolewa au kuzinduliwa. Hata hivyo, Kanuni yote inazungumzia kuhusu bidhaa na si huduma kama ilivyotafsiriwa katika Kanuni ya 2.</p> <p>3. Kanuni hazioneshi utaratibu wa kutoa matangazo kwa umma kuhusu kurejesha bidhaa ambazo hazina viwango. Kutooneshwa kwa utaratibu huo, kunaweza kusababisha kuendelea kusambaa zaidi kwa bidhaa</p>	<p>tafsiri ya neno "product" ili kuendana na muktadha wa Kanuni hii.</p> <p>3. Kanuni zifanyiwe marekbisho ili kuongeza utaratibu wa utoaji wa matangazo kwa umma.</p>

#	Namba ya Tangazo la Serikali (Gn Number)	Jina la Sheria Ndogo (Name)	Sheria Inayotoa Madaraka (Enabling Law)	Mamlaka Inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi (Observations)	Maoni na Mapendekezo (Recommendations)
					<p>zisizofaa pasipo kufahamika katika jamii.</p> <p>4. Kanuni ya 3(2) inaweka wajibu kwa msambazaji au mzalishaji wa bidhaa kutoa taarifa kuhusu bidhaa zisizo na ubora. Hata hivyo, Kanuni hazioneshi namna ambavyo walaji pia wanaweza kutoa taarifa kuhusu bidhaa zisizo na ubora. Kukosekana kwa fursa hiyo kunaminywa wigo wa upatikanaji wa taarifa kuhusu bidhaa zisizo na</p>	<p>4. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuweka utaratibu wa namna ambavyo walaji pia wataweza kutoa taarifa kuhusu bidhaa zisizo na ubora.</p>

#	Namba ya Tangazo la Serikali (Gn Number)	Jina la Sheria Ndogo (Name)	Sheria Inayotoa Madaraka (Enabling Law)	Mamlaka Inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi (Observations)	Maoni na Mapendekezo (Recommendations)
					<p>ubora kwa kuwa walaji ndio wanaweza kuwa na taarifa nzuri kuhusu ubora wa bidhaa wanazotumia.</p> <p>5. Kanuni ya 5 inamtaka msambazaji au mzalishaji wa bidhaa kuandaa nyaraka zinazoweka utaratibu wa kupokea, kuchunguza na kushughulikia malalamiko yanayotokana na bidhaa zao.</p> <p>Hali hiyo inaweza kusababisha uwezekano wa msambazaji au</p>	<p>5. Kanuni zifanyiwe marekebisho ili kuonesha pia jukumu la kupokea, kuchunguza na kushughulikia malalamiko litafanyika na TBS kama msimamizi mkuu wa viwango vya bidhaa nchini.</p>

#	Namba ya Tangazo la Serikali (Gn Number)	Jina la Sheria Ndogo (Name)	Sheria Inayotoa Madaraka (Enabling Law)	Mamlaka Inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi (Observations)	Maoni na Mapendekezo (Recommendations)
					mzalishaji kupokea malalamiko ambayo yanayowagusa wao mwenyewe na hivyo kuondoa uwajibikaji.	
6.	GN NA. 685 (TS Na. 685) 24 Septemba, 2021	The Tanzania Medicines and Medical Devices (Laboratory Analysis of Medical and Non Medical Products) Regulations, 2021	THE TANZANIA MEDICINES AND MEDICAL DEVICES ACT (SURA. 219) (Zimetungwa chini ya Kifungu cha 122(1) (t) na (z))	WIZARA YA AFYA	1. Kanuni ya 2 imeonesha kuwa Kanuni hizi zitatumika kuweka utaratibu wa namna ya kuendesha shughuli za uchunguzi wa kimaabara katika udongo, sampuli za binadamu na wanyama. Hata hivyo jukumu la kushughulikia masuala hayo ni kinyume na lengo la Sheria Mama ambalo ni udhibiti wa dawa, vifaa tiba, dawa za	1. Kanuni 2 ifanyiwe marekebisho ii kuendana na majukumu ya TMDA yaliyowekwa kwa mujibu wa Sheria Mama.

#	Namba ya Tangazo la Serikali (Gn Number)	Jina la Sheria Ndogo (Name)	Sheria Inayotoa Madaraka (Enabling Law)	Mamlaka Inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi (Observations)	Maoni na Mapendekezo (Recommendations)
					<p>asili pamoja na sumu.</p> <p>Aidha, ni kinyume na Kifungu cha 122 (1) (t) (z) cha Sheria Mama ambacho kimempa Waziri mamlaka ya kutunga Kanuni za kuanzisha maabara za kupima dawa chakula , vipodozi na dawa za asili.</p> <p>2. Kanuni ya 21(2) inarejea Jedwali la Tano na Sita kuhusu <i>Certificate of analysis</i>. Hata hivyo, Jedwali la Tano na Sita hayapo katika Kanuni hizi. Hali hiyo inaweza</p>	<p>2. Kanuni ya 21(2) ifanyiwe marekebisho ili kufuta rejea ya majedwali na badala yake Kanuni hii itaweka rejea ya Kanuni ya 17(2) inayoanzisha Form</p>

#	Namba ya Tangazo la Serikali (Gn Number)	Jina la Sheria Ndogo (Name)	Sheria Inayotoa Madaraka (Enabling Law)	Mamlaka Inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi (Observations)	Maoni na Mapendekezo (Recommendations)
					<p>kuwa imetokana na kusahalika kwa Jedwali na Tano na Sita katika Kanuni hizi hali inayoweza kusababisha kutokamilika kwa tija iliyokusudiwa katika Kanuni hizi.</p> <p>3. Kanuni ya 22(1) inaelekeza kuwa sampuli pekee za bidhaa zilizohakikiwa katika Maabara ya Mamlaka ndizo zitaharibiwa kwa utaratibu wa Kanuni za Kuharibu Bidhaa. Kanuni hazioneshi utaratibu wa namna ya kuharibu sampuli za bidhaa ambazo zimehakikiwa na</p>	<p>No. 2 kuhusu certificate of analysis na Fomu Na. 3 kuhusu <i>Certificate of Conformity</i> katika Jedwali la Kwanza.</p> <p>3. Kanuni ifanyiwe marekbisho ili kuainisha utaratibu wa kikanuni wa kuharibu sampuli za bidhaa ambazo zimehakikiwa na maabara nyingine tofauti na Maabara ya TMDA.</p>

#	Namba ya Tangazo la Serikali (Gn Number)	Jina la Sheria Ndogo (Name)	Sheria Inayotoa Madaraka (Enabling Law)	Mamlaka Inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi (Observations)	Maoni na Mapendekezo (Recommendations)
					<p>maabara ambazo zimekasimiwa jukumu la kuhakiki sampuli kwa niaba ya Mamlaka.</p> <p>4. Kanuni ya 22(2) inaonesha kuwa iwapo sampuli zilizochukuliwa ili kufanyiwa uhakiki na zikabainika hazina madhara zitagawiwa kama msaada kwa taasisi za umma na vituo vya afya. Kanuni hazioneshi uwezekano wa sampuli hiso kurejeshwa kwa mzalishaji au msambazaji ili aendelee na utaratibu wa</p>	<p>4. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuonesha utaratibuwa kurejeshwa wa mmiliki sampuli zilizohakikiwa na kubainika hazina madhara kwa matumizi.</p>

#	Namba ya Tangazo la Serikali (Gn Number)	Jina la Sheria Ndogo (Name)	Sheria Inayotoa Madaraka (Enabling Law)	Mamlaka Inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi (Observations)	Maoni na Mapendekezo (Recommendations)
					<p>kuzifanyia biashara kama alivyokusudia.</p> <p>5. Kanuni ya 33(e) inafafanua kwamba ikiwa mjumbe wa Kamati ya Kitaalamu ya Maabara (Laboratory Technical Committee) atashitakiwa na kupatikana na hatia ya kosa lolote ambalo na kuhukumiwa kufungwa kifungo kinachozidi miezi sita, itasababisha kusababisha ujumbe wake kukoma. Kanuni haijaonesha makosa ya jinai kuwa ni lazima</p>	<p>5. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuonesha makosa yatakayosababisha mjumbe wa Kamati ya Kitaalamu ya Maabara (<i>Laboratory Technical Committee</i>) kukoma kuwa ni yale ambayo yanahusiana na majukumu yake.</p>

#	Namba ya Tangazo la Serikali (Gn Number)	Jina la Sheria Ndogo (Name)	Sheria Inayotoa Madaraka (Enabling Law)	Mamlaka Inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi (Observations)	Maoni na Mapendekezo (Recommendations)
					<p>yatokane/yahusiane moja kwa moja na majukumu yanayotekelezwa na mjumbe.</p> <p>6. Kanuni ya 62 inaweka utaratibu wa namna ya kushughulikia rufaa. Hata hivyo, Kanuni haioneshi muda ambao rufaa iiliyowasilishwa itashughulikiwa na pia sharti la mkata rufaa kujulishwa kuhusu uamuzi uliotolewa na Mamlaka.</p> <p>7. Fomu Na. 5 ya Jedwali la Kwanza inayoonesha mfano</p>	<p>6. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuweka muda wa kushughulikia rufaa na utaratibu wa kumjulisha mrufani kuhusu uamuzi uliotolewa.</p> <p>7. Fomu Na. 5 ifanyiwe</p>

#	Namba ya Tangazo la Serikali (Gn Number)	Jina la Sheria Ndogo (Name)	Sheria Inayotoa Madaraka (Enabling Law)	Mamlaka Inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi (Observations)	Maoni na Mapendekezo (Recommendations)
					wa Cheti cha Mafunzo imerejea kuanzishwa chini ya Kanuni ya 56 ambayo haihusiani na Cheti cha Mafunzo.	marekebisho kwa kufuta Kanuni ya 56 na kurejea Kanuni sahihi inayoanzisha Fomu hiyo.
7.	GN NA. 686 (TS Na. 686) 24 Septemba, 2021	The Tanzania Medicines and Medical Devices (Fees and Charges) Regulations, 2021	THE TANZANIA MEDICINES AND MEDICAL DEVICES ACT (SURA. 219) (Zimetungwa chini ya Kifungu cha 122(1) (i))	WIZARA YA AFYA	1. Kipengele cha 65 hadi 68 vya Jedwali la Kwanza vinazungumzia kuhusu ada mbalimbali kwa huduma ya majaribio ya maabara " <i>clinical trials</i> ". Hata hivyo ada inayowekwa ipo katika viwango vya dola za marekani pasipo kuonesha iwapo huduma inayokudusiwa ni ya	1. Kanuni ifanyiwe marebisho ili kuonesha kuwa viwango vilivyowekwa ni kwa ajili ya watafiti wa nje na wale wanafanya utafiti kwa kutumia wafadhili kutoka nje. Aidha, Kanuni iweke viwango vinavyopaswa kulipwa na watafiti wa ndani.

#	Namba ya Tangazo la Serikali (Gn Number)	Jina la Sheria Ndogo (Name)	Sheria Inayotoa Madaraka (Enabling Law)	Mamlaka Inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi (Observations)	Maoni na Mapendekezo (Recommendations)
					<p>ndani au kutoka nje ya Tanzania au ni kwa ajili ya Watanzania.</p> <p>2. Kanuni ya 3 imetafsiri maneno <i>Local Government Authority, innovator product, alteration or innovation fee, animal biological specimens, annual retention fee, ceiling Price, customer, domestic product, donation, medical supplier</i>. Hata hivyo, maneno hayo hayajatumika katika sehemu yoyote ndani ya Kanuni hizi.</p>	<p>2. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kufuta maneno yaliyowekwa katika tafsiri pasipo kutumiwa katika Kanuni hizi.</p>

#	Namba ya Tangazo la Serikali (Gn Number)	Jina la Sheria Ndogo (Name)	Sheria Inayotoa Madaraka (Enabling Law)	Mamlaka Inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi (Observations)	Maoni na Mapendekezo (Recommendations)
TOLEO NA. 44 LA TAREHE 23 OKTOBA, 2021						
8.	GN NA. 766 (TS Na. 766) 29 Oktoba, 2021	The Banking and Financial Institutions (Development Finance) Regulations, 2021	THE BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS ACT, (SURA 342) (Zimetungwa chini ya Kifungu cha 71)	WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO	<p>1. Jedwali la Nne limerejea kimakosa kuanzishwa chini ya Kanuni ya 19(1) badala ya Kanuni ya 18(1). Hali hiyo inasababisha kukosekana kwa mtiririko mzuri wa usomaji wa Kanuni hizi.</p> <p>2. Jedwali la Tano limerejea kimakosa kuanzishwa chini ya Kanuni ya 19(3) badala ya Kanuni ya 18(3). Hali hiyo inasababisha kukosekana kwa mtiririko mzuri wa</p>	<p>1. Jedwali la Nne lifanyiwe marekebisho kwa kufuta rejea ya Kanuni ya 19(1) na badala yake kurejea Kanuni ya 18(1).</p> <p>2. Jedwali la Tano lifanyiwe marekebisho kwa kufuta rejea ya Kanuni ya 19(3) na badala yake kurejea Kanuni ya 18(3)</p>

#	Namba ya Tangazo la Serikali (Gn Number)	Jina la Sheria Ndogo (Name)	Sheria Inayotoa Madaraka (Enabling Law)	Mamlaka Inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi (Observations)	Maoni na Mapendekezo (Recommendations)
					usomaji wa Kanuni hizi.	



Jasson S. Rweikiza (Mb)

MWENYEKITI

KAMATI YA SHERIA NDOGO

18 Februari, 2022